# DHAMIRA NA WAHUSIKA KATIKA FASIHI YA VIJANA: BUNILIZI YA *MAJILIO YA MKOMBOZI* NA *KIMBILIO LA SILONA*

**NA**

**INNOCENT NYACHWAYA OKWORO**

**C50/38697/2020**

**IDARA YA KISWAHILI**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2023**

# UNGAMO

Napenda kutamka kwa wazi kuwa tasnifu hii, niliyoandika na kuiwasilisha hapa, ni kazi yangu binafsi. Hakuna sehemu yoyote ya tasnifu hii ambayo imewahi kuwasilishwa katika chuo kingine chochote au taasisi nyingine yoyote. Yote yaliyomo katika tasnifu hii ni matokeo ya utafiti wangu, uchambuzi, na mchakato wa ubunifu wa kibinafsi.

Ninafahamu umuhimu wa kuheshimu haki za kisomi na maadili ya kitaaluma, na hivyo basi, nathibitisha kuwa tasnifu hii ni ya kipekee na haijachapishwa wala kuwasilishwa popote. Hii ni kazi yangu ya kibinafsi na ina nia ya kuchangia maarifa na uelewa katika utanzu wa fasihi ya vijana.

Kwa hiyo, nakubaliana kwa dhati na maelezo yaliyotolewa katika ungamo hili, na nawajibika kwa ukamilifu kuhusu uhalali wa tasnifu hii na ukweli wa taarifa nilizotoa.

Sahihi.................................................Tarehe 28.11.2023 .................................

**Innocent Okworo**

**(Mtahiniwa)**

**Nambari ya Usajili: C50/38697/2020**

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

Sahihi.................................................Tarehe 28.11.2023 .................................

**Prof. K.W Wamitila**

Sahihi.................................................Tarehe 28/11/2023 .................................

**Dr. Ayub Mukhwana**

## SHUKURANI

Ninapochambua nyuma ya pazia la utafiti huu uliojaa changamoto na maarifa, sina budi kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote waliogusa na kuchangia kwa namna moja au nyingine katika safari hii yenye umuhimu mkubwa.

Maulana, mchungaji wetu na kiongozi wa kiroho, nakushukuru kwa baraka zako zilizoniongoza na kunitia nguvu wakati wote wa utafiti huu. Neema yako imenipa ujasiri wa kujitosa kwenye kina cha maarifa bila woga.

Wasimamizi wangu wa utafiti Prof. Wamitila na Dkt Mukhwana, nawashukuru kwa mwongozo wenu wa kitaalamu ulionirahisishia njia yangu kuelekea kwenye malengo yangu. Msaada wenu umekuwa ni kama dira yenye thamani inayoniongoza katika bahari hii ya maarifa.

Waadhiri wa chuo kikuu Prof. Habwe, Prof. Kineene wa Mutiso, Prof Mwenda Mbatia, Prof. Iribe Mwangi, Prof Mbuthia, Prof. Rayya Timmamy, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt Leo Zanja, Dkt. Hannah Mwaliwa, Dkt. Mungania Basillio, Dkt. Mary Ndung'u na Dkt. Samson Ongarora., mnastahili shukrani kwa mchango wenu wa kina katika uchambuzi na maoni yenu ya thamani yaliyoimarisha uundaji wa utafiti huu. Ningeukosa mchango wenu, utafiti huu usingekuwa na ubora unaovutia.

Wanafunzi wenzangu, hongereni kwa ushirikiano wenu na mawazo yenu yenye mvuto. Ushirikiano na majadiliano yamezidi kuboresha na kuchangia kwa kiasi kikubwa kwenye ubunifu wa utafiti huu.

Familia yangu, nashukuru kwa uvumilivu wenu na uhamasishaji wa dhati. Ushirikiano wenu umenipa nguvu ya kuendelea mbele hata wakati wa changamoto si haba.

Wazazi wangu na rafiki wa dhati, asanteni kwa kuwa nguzo imara. Kila faraja, ushauri, na kila wakati wa furaha mliochangia umekuwa na thamani kubwa sana.

## IKISIRI

Tasnifu hii inajitahidi kuchunguza kwa kina Dhamira na Wahusika katika Fasihi ya Vijana: *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona* ikilenga kuonyesha jinsi dhamira na wahusika vinavyojitokeza na kuundwa katika muktadha wa fasihi ya vijana. Malengo ya utafiti yanazingatia kuchambua jinsi wahusika vijana wanavyoleta maana kwa dhamira na jinsi sifa za fasihi ya vijana zinavyoathiri uundaji wa hadithi.

Nadharia ya utanzu inatoa mwongozo wa utafiti, ikisisitiza jinsi fasihi ya vijana inavyoweza kutumika kutatua matatizo ya kijamii na kuunda jamii bora. Uchambuzi wa wahusika kama Getukwa na Ilonkundemi katika *Majilio ya Mkombozi* na Silona na Rafiki wake katika *Kimbilio la Silona* unafanywa kwa kuzingatia muktadha huu wa nadharia ya utanzu.

Lengo la utafiti ni kutoa mwanga juu ya jinsi dhamira inavyoonyeshwa na wahusika katika fasihi ya vijana na jinsi sifa za fasihi ya vijana zinavyoathiri mwelekeo wa hadithi.

Kupitia tasnifu hii, lengo ni kutoa ufahamu wa kina juu ya jinsi fasihi ya vijana inavyochora taswira ya dhamira na wahusika, na jinsi sifa za vijana zinavyoimarisha na kuchangia katika muktadha huu. Nadharia ya utanzu inaongoza njia yetu ya kuelewa na kuchambua matokeo ya utafiti, ikisaidia kutoa mwanga wa jinsi fasihi ya vijana inavyochangia katika ujenzi wa maana za kijamii.

# YALIYOMO

SURA YA KWANZA ........................................................................................................1

1.1 Usuli wa Mada ........................................................................................................1

1.2 Suala La Utafiti ........................................................................................................3

1.3 Maswali ya Utafiti........................................................................................................4

1.4 Malengo ya Utafiti ........................................................................................................4

1.5 Sababu za Kuchagua Mada........................................................................................5

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada........................................................................................6

1.7 Upeo na Mipaka........................................................................................................9

1.8 Msingi wa Nadharia........................................................................................................10

1.9 Mbinu za utafiti........................................................................................................16

SURA YA PILI........................................................................................................18

2.0 Utangulizi........................................................................................................18

2.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Kimbilio la Silona* (Mbatiah 2021) ........................................18

2.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* (Mbatiah 2016) ...................................21

2.3 Sifa Za Fasihi ya Vijana (FYV) Zinazojitokeza Katika Riwaya Teule ...........................27

SURA YA TATU ........................................................................................................31

3.0 Dhamira....................................................................................................31

3.1 Dhamira katika Riwaya ya *Kimbilio la Silona* ...........................................................31

3.1.1 Ndoa za Kulazimishwa na za Mapema ................................................................32

3.1.2 Mapenzi......................................................................................................37

3.1.3 Dhamira ya Utamaduni .............................................................................42

3.1.4 Dhamira ya Nafasi ya vijana wa kike katika Jamii.............................................45

3.1.5 Dhamira ya Elimu ya Vijana........................................................................49

3.2 Dhamira Katika Riwaya ya *Majilio ya Mkombozi*......................................................53

3.2.1 Dhamira ya Mapenzi.....................................................................................53

3.2.2 Dhamira ya Vijana na Ukombozi ......................................................................56

3.2.3 Dhamira ya Malezi ya Vijana ..........................................................................62

3.2.4 Muhtasari .......................................................................................................65

SURA YA NNE......................................................................................................66

4.0 Utangulizi.....................................................................................................66

4.1 Maelezo ya Wataalamu kuhusu wahusika katika Fasihi ya Vijana ..............................66

4.2 Wahusika katika Kimbilio la Silona na Majilio ya Ukombozi ......................................68

4.2.1 Wahusika na umri ..........................................................................................68

4.2.2 Wahusika na Mgogoro .....................................................................................70

4.2.3 Wahusika na Mtazamo........74
4.2.4 Wahusika na Dhamira........77
4.2.5 Wahusika na Lugha........79
4.2.6 Mazingira na Wahusika........81
4.3 Hitimisho........83
SURA YA TANO........84
5.0 Utangulizi........84
5.1 Muhtasari wa Utafiti........84
5.2 Matokeo ya utafiti........86
5.3 Mchango wa Utafiti........90
5.4 Changamoto za Utafiti........91
5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo........91
MAREJELEO........93

# DHAMIRA NA WAHUSIKA KATIKA FASIHI YA VIJANA: BUNILIZI YA *MAJILIO YA MKOMBOZI* NA *KIMBILIO LA SILONA*

## SURA YA KWANZA

### 1.1 Usuli wa Mada

Fasihi ya Vijana (FYV) ni utanzu wa kiutunzi wa kazi za kibunilizi ambao unatekeleza majukumu mengi ya kujenga fasihi, kuburudisha, kuelimisha na kuadilisha vijana kama sehemu ya kimsingi ya jamii. Utanzu huu umeanza kukua na kuimarika katika fasihi ya Kiswahili hivi kwamba katika hali yake ya sasa huu ni utanzu ambao una nafasi muhimu katika jamii. Pamoja na kwamba utanzu huu umefikia hadhi hii, ni muhimu, kwa mintarafu ya utafiti unaokusudiwa hapa, kutalii na kuielewa FYV katika fasihi ya Kiswahili. Pendekezo la utafiti huu linakusudia kuangazia dhamira na wahusika katika FYV kwa kurejelea riwaya teule za vijana za *Majilio ya Mkombozi* (2016) na *Kimbilio la Silona* (2021).

Simala na Chacha (2014) walieleza kuwa FYV inalenga vijana ambao wamebaleghe na hawawezi faidi kwa kusoma fasihi ya watoto (FYW) ama ya watu wazima. FYV inawalenga wahusika walio kati ya umri wa miaka kumi na miwili hadi kumi na tisa. Huu utanzu wa fasihi unalenga vijana kwa sababu wanaweza kuelewa maudhui mbalimbali yanayowahusu. Kwa mfano, maudhui yanayowalenga vijana na ambayo yamesababisha chimbuko la huu utanzu ni kama madhara ya dawa za kulevya, ukimwi, mimba za mapema, kuzingatia masomo kwa jinsia zote, tamaduni zizokuwa na tija, na athari hasi za teknolojia. Pia masuala ya uchafuzi wa mazingira, maisha ya mjini, uongozi mbaya, na ukosefu wa ajira nchini Kenya umechangia kukua kwa FYV ili kuwasaidia walengwa kupata elimu kuhusu masuala yanayowakumba na kuwapa mbinu mbalimbali wanazoweza kuzitumia ili kujikomboa.

Dhamira ni wazo kuu linalokuzwa katika kazi ya fasihi. Wasomi mbalimbali wameeleza maana ya dhamira na maoni yao ni muhimu katika hili pendekezo.

Njogu na Chimerah (1999) walieleza kuwa dhamira ni lengo la mwandishi wa kazi ya kifasihi. Wanatoa mfano kuwa, dhamira ya riwaya ya Walenisi ni ubainishaji wa ujenzi wa jamii mpya. Wamitila (2003) anasema kuwa mwandishi anapoanza kuandika riwaya au kazi yoyote ya fasihi huwa na lengo fulani. Msomaji huenda asiwe na bahati ya kukutana na msanii au mwandishi wa kumwuliza lengo au alichokusudia kukisema katika kazi yake ya fasihi. Msomaji huyo atalazimika kuisoma kazi hiyo kwa makini na kuangalia ni wazo gani analolikuza au kuliendeleza mwandishi katika kazi yake ya fasihi kuanzia mwanzo mpaka mwisho. Mara nyingi lengo au wazo hilo huweza kuakisika kwenye anwani ya kazi yake. Kwa hivyo, lengo au wazo hilo ndilo linajulikana kama dhamira. Pamoja na hayo ni kuwa dhamira huwa ni sehemu ya maudhui kwa maana maudhui yanaibuka katika uendelezaji na ukuzaji wa dhamira.

Manoti (2012) alieleza kuwa dhamira ni wazo kuu katika kazi ya kifasihi ambalo hujitambulisha tangu mwanzo hadi mwisho. Ali (2019) alieleza dhamira kuwa kiini cha kazi ya msanii. Pia alifafanua kuwa kuna aina mbili za dhamira ambazo ni dhamira kuu na ndogo ambazo zinawasaidia wasanii katika kujenga maudhui yao. Wasike (2020) akimrejelea Wamitila anasema kuwa dhamira ni maana mwandishi wa kifasihi au msomi wa kazi ya fasihi anayovumbua. Alizidi kueleza kuwa msomi au mlengwa wa kazi ya fasihi anaweza kuvumbua maana ya kazi ya kifasihi kwa kusoma kwa makini. Pia dhamira hujitokeza kutokana na mambo yanayohusiana na maudhui kama vile siasa, utamaduni, na uchumi.

Kwa mujibu wa Mutua na wenzake (2017) wahusika ni viumbe wanaokuwa na sifa maalum ambazo msanii hutumia kupitisha ujumbe wake kwa mlengwa. Mara nyingi wasanii wa kazi za fasihi ya Kiswahili huwateua wahusika kutoka kundi la wanadamu katika jamii lengwa.

Haji (2018) alieleza kuwa wahusika ni viungo muhimu katika kazi za fasihi kwa sababu huwasaidia waandishi kukuza matukio mbalimbali yanayojenga dhamira kuu na ndogo ambazo zinapitisha ujumbe kwa mlengwa. Kinoti (2019) yeye alieleza kuwa wahusika ni viumbe, vitu, ama watendi ambao wasanii hutumia kufanikisha malengo yao. Maguo na Alhabib (2021) walihoji kuwa wahusika ni nyenzo muhimu wasanii wa fasihi hutumia kwa ishara ili kupitisha ujumbe kwa walengwa.

Kwa jumla wahusika ni viungo muhimu katika kazi za fasihi ya Kiswahili. Aghalabu huwa ni wanaume na wanaweke ambao mwandishi huwateua na kuwatumia kiishara ili kufikisha ujumbe kwa mlengwa. Waandishi huteua wahusika walio na sifa maalum ili kufanikisha malengo yao.

## 1.2 Suala La Utafiti

Tafiti nyingi zimeshughulikia masuala ya vijana kama vile nafasi ya vijana katika jamii, maudhui anuwai yanayohusu maisha ya vijana, usawiri wa wahusika vijana katika kazi mbalimbali za fasihi, na changamoto zinazowakumba watu katika ujana wao. Hakuna ithibati zozote za kiusomi kwamba masuala haya yamewahi kuhusishwa na dhamira na usawiri wa wahusika katika riwaya za vijana wanaobaleghe.

Utafiti huu unakusudia kuonyesha na kufafanua dhamira zinazohusiana na vijana wanaobaleghe. Pamoja na hayo, unanuia kuonyesha usawiri wa wahusika vijana katika fasihi ya vijana. Utafiti huu unahoji tangu awali kwamba dhamira yoyote ile inayojitokeza au inayozungumziwa katika fasihi ya vijana, ni masuala yanayokitwa au yanahusiana na uhalisia wa maisha ya vijana. Vilevile utafiti huu unalenga kuonyesha jinsi ambavyo usawiri wa wahusika katika riwaya za vijana unabainisha sifa za kimsingi za FYV. Mbali na kuonyesha dhamira zinazohusiana na vijana wanaobaleghe na kuthathimini usawiri wa wahusika katika FYV, utafiti

huu pia unalenga kuonyesha jinsi dhamira na usawiri wa wahusika vijana unavyoakisika katika tungo za fasihi ya vijana kwa kurejelea kazi teule za *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona*. Hatimaye inatumainiwa kwamba mijadala itakayoibushwa katika utafiti huu kuhusiana na suala hili la dhamira na wahusika itabainisha moja ya wasifu wa kimsingi wa fasihi ya vijana ambao hujashughulikiwa kiusomi katika fasihi ya Kiswahili.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kujibu maswali ya utafiti yafuatayo:

1. Je, ni dhamira zipi zinazojitokeza kama wasifu wa kimsingi wa FYV katika fasihi ya Kiswahili?
2. Je, wahusika wanasawiriwa na kuakisika vipi katika FYV kwa kurejelea riwaya teule za *Kimbilio la Silona* na *Majilio ya Mkombozi*?
3. Je, dhamira na wahusika katika riwaya za vijana zinaakisi vipi sifa za kimsingi za FYV?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu una malengo ya kiutafiti yafuatayo:

1. Kueleza na kufafanua dhamira zinazojitokeza katika FYV kama sifa ya kimsingi inayohitaji kushirikishwa katika ufafanuzi wa FYV katika fasihi ya Kiswahili.
2. Kuonyesha usawiri na aina za wahusika katika fasihi ya vijana kwa kurejelea riwaya teule *Kimbilio la Silona na Majilio ya Mkombozi*.
3. Kuonyesha jinsi dhamira zinazohusiana na vijana wanaobaleghe na usawiri wa wahusika unaakisi sifa za kimsingi za FYV.

**1.5 Sababu za Kuchagua Mada**

Uteuzi wa mada hii ulichochewa na sababu kadha wa kadha. Kwanza, riwaya teule za *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona* ni miongoni mwa riwaya za vijana ambazo zimeandikwa kwa kuzingatia dhamira zinazowahusu vijana na wahusika waliomo ni vijana wanaobaleghe. Riwaya hizi zimeandikwa katika karne ya ishirini na moja ambapo zimeangazia masuala ya kisasa yanayowahusu vijana kama vile mapenzi, elimu, matumizi ya dawa za kulevya, uchafuzi wa mazingira na mambo mengine. Kwa sababu hii kazi hizi ni za muhimu katika kurejelea masuala ya vijana katika utafiti huu. Kwa hivyo riwaya hizi zitatupa data itakayotuwezesha kuonyesha vipengele vya dhamira na wahusika jinsi vinavyoakisika katika FYV.

Pamoja na hayo, watafiti wa masuala ya vijana katika fasihi ya Kiswahili hasa nchini Kenya hawajaliangazia suala la dhamira na wahusika katika riwaya za vijana wanaobaleghe jinsi ambavyo zinaakisi sifa za FYV hasa vijana wa miaka 11 hadi 19. Baadhi ya kazi za awali zimeangazia vijana kwa mitazamo mbalimbali. Kwa mfano, Mutua (2007) alichunguza suala la ukombozi wa vijana kwa kuangazia mitazamo yao na ile ya wazee katika tamthilia tatu teule (*Kitumbua Kimeingia Mchanga*, *Migogoro,* na *Natala*) Nalika (2012) aliangalia changamoto zinazowakumba vijana katika riwaya za *Vipanya vya Maabara*. Kihara (2016) alishughulikia nafasi ya vijana katika riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*. Kerre (2020) alitafiti kuhusu maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana akitumia kazi za kifani za *Chozi Langu* na *Dunia Mashaka*. Kwa hivyo katika kuendeleza kazi za watafiti wa awali ni muhimu kuangazia swala la dhamira na wahusika katika riwaya za vijana na jinsi vipengele hivi vinaakisi sifa za FYV katika Kiswahili.

Pia niliteua hii mada kwa sababu kazi yoyote ya fasihi ina lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira. Vipengele vya dhamira na wahusika ni muhimu katika kazi za kifasihi kwa kuwa ni

vigezo ambavyo hubeba ujumbe wa mwandishi. Uchunguzi wa vipengele hivi unasaidia kuelewa na kukuza kazi ya kifasihi. Kwa hivyo kuangalia vipengele hivi vile vinaakisika katika riwaya teule za vijana ni jambo muhimu kwa sababu husaidia katika kuangalia sifa bainifu za utanzu wa FYV.

Fauka ya hayo, uteuzi wa mada hii unalenga kuonyesha kuwa FYV ina umuhimu kwa kuonyesha masuala ya vijana wanaobaleghe na kuweka wazi changamoto ambazo vijana hawa hupitia wanapokumbana na hali halisi ya ujana. Kwa kuonyesha vipengele vya dhamira na wahusika katika riwaya za vijana ni malengo ya utafiti huu kwamba kutakuwa na badiliko jinsi ambavyo vijana watasawiriwa katika jamii na FYV ipate nguvu ili kazi nyingi ziandikwe na kukidhi mahitaji ya vijana.

Utafiti huu ni wa muhimu sana kwa waandishi wa fasihi, wahakiki wa fasihi, wachanganuzi wa masula ya vijana, waalimu wa fasihi, vijana na jamii kwa jumla kwa maana utasidia pakubwa kuelewa vipengele vya dhamira na wahusika katika riwaya za vijana katika FYV.

## 1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Lengo la utafiti huu ni kutathimini vipengele vya dhamira na wahusika vinavyoakisika katika riwaya za vijana na jinsi ambavyo vinabainisha sifa za FYV kwa kurejelea riwaya teule za Mbatiah *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona*. Ili kufikia lengo la utafiti huu nimepitia maandiko kuhushu dhana hii muhimu ya FYV.

Nkonge (2006) aliweza kuyashugulikia masuala yanayowahusu vijana kwa kurejelea riwaya za *Kichwa Maji* na *Nguvu ya Sala*. Katika hii tasnifu yake aliangazia mambo kama vile mapenzi, ndoa, malezi, uozo uliopo katika jamii na dini. Tasnifu ya Nkonge itanisaidia kuelewa jinsi maudhui haya yanakuza dhamira zinazowahusu vijana kisaikolojia, kitamaduni, na kijamii

ili kuchangia ukuaji wa FYV. Kwa mfano, tutaanagazia dhamira ya wasichana kulazimishwa kuolewa mapema kwa sababu wazazi wa kiume wanataka mali ya haraka. Kwa hivyo tasnifu yake inajenga misingi ya vile vipengele vya wahusika na dhamira tutakavyoangazia katika utafiti huu.

Mutua (2007) alikamilisha tasnifu yake ambapo aliangazia mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi. Alieleza kuwa vijana wa kiume walikuwa na mtazamo wa kuwasaidia wanawake kwa ujumla kupata ukombozi katika maisha yao. Pia alieleza kuwa vijana wa kike walikuwa na nia ya kusoma ili wapate kazi nzuri ili wajikuamue kutokana na mila potofu. Hawa vijana wa kike walizipinga tamaduni zilizokuwa na tija katika maisha yao kama vile kuchaguliwa wachumba na ndoa za mapema. Zaidi vijana wa kike walikuwa na nia ya kuwepo mabadiliko katika mahusiano yao na wanaume. Haya masuala Mutua aliyoyangazia yanaambatana na yale nitakayoangazia katika ufafanuzi wa dhamira katika riwaya za vijana. Katika *Majilio ya Mkombozi* swala la ukombozi limejitokeza na hili linaoana na yale Mutua aliyaangazia katika kazi yake. Yeye alitumia nadharia ya ufeministi kuangazia mitazamo ya vijana na wazee kuhusu ukombozi ila mimi nitatumia nadharia ya tanzu kueleza vigezo vinavyotambulisha FYV.

Nalika (2012) aliangazia matatizo yanayowakumba vijana kwa kuzingatia riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Katika kazi yake aliangazia maudhui na katika sura ya nne alieleza changamoto vijana haswa wa mjini nchini Kenya wanazozipitia. Nalika alionyesha kuwa vijana hukumbana na matatizo kama malezi, dawa za kulevya, umaskini, ukosefu wa ajira, ukosefu wa maadili, maradhi ya ukimwi, na ufisadi. Haya matatizo aliyoyaangazia ni ya manufaa kwa sababu ndiyo yanawasaidia wasanii kutunga tungo za kuwapa vijana matumaini na kujikomboa.

Kwa hivyo hata kama hayashuguliki na FYV moja kwa moja yana uhusiano mkubwa na mada ya utafiti huu kwa maana dhamira ni sehemu ya maudhui.

Wanjala (2015) aliangazia swala la utambulisho katika tasnifu yake ya uzamili. Alieleza kuwa malezi huathiri utambulisho wa vijana kwa njia nyingi sana ilivyojitokeza katika riwaya teule za *Asali Chungu*, *Anasa*, na *Fahari ya Mateso*. Tasnifu hii yake inatusaidia kuelewa sifa muhimu za FYV kwa sababu swala la utambulisho hujitokeza. Kila utanzu una vigezo vinavyouhusiana na utambulisho na hilo ni la muhimu sana katika huu utanzu wa FYV.

Kihara (2016) alieleza nafasi ya vijana katika jamii kwa kuangazia riwaya za *Pendo la Karaha* na *Kovu Moyoni*. Katika hii kazi yake alikuwa na lengo la kuchunguza harakati za vijana katika juhudi zao za ukombozi kutokana na matatizo yanayowakumba. Kihara alitambua dhuluma za mapenzi, ukosefu wa ajira, ubinafsi katika jamii, na dawa za kulevya kama baadhi ya matatizo yanayowakumba vijana. Kwa hivyo vijana hujaribu kujikomboa kutumia mbinu tofauti tofauti. Tasnifu ya Kihara ni ya manufaa mengi kwangu kwa sababu inaangazia suala la ukombozi ambalo ni la msingi kaitka ukuaji wa FYV nchini Kenya.

Kerre (2020) alishughulikia maswala ya vijana, licha ya kuwa hakujibana katika vijana wanaobaleghe, kwa kuangazia maudhui ya mabadiliko na ukuaji wao kwa kurejelea riwaya za *Chozi Langu* na *Dunia Mashaka Makuu*. Katika hii tasnifu yake alieleza kuwa kuna mabadiliko chungu nzima yanayowatambulisha vijana kama vile ya tabia, hali, hisia, na afya. Masuala ya kijamii kama malezi na tabaka huathiri mabadiliko ya vijana. Haya masuala aliyoyaeleza yananisaidia kuelewa vijana zaidi ili kutambua sifa zinazohusu tanzu inayowalenga. Yeye alitumia nadharia ya uhalisia kwa sababu alikuwa anashughulikia maudhui ya mabadiliko katika jamii ila mimi nitatumia nadharia ya tanzu kwa sababu ninazingatia utanzu unaowahusu vijana

moja kwa moja. Zaidi kuna uwiano wa karibu wa kazi hii na huu utafiti kwa sababu dhamira na usawiri wa wahusika unaingiliana sana.

Sanga (2021) alieleza kuwa fasihi ni zao la jamii na mabadiliko katika maisha ya wanajamii huathiri huu utanzu kwa njia mbalimbali. Kwa mfano alikiri kuwa mkengeuko wa uchumi huathiri sifa za tanzu ndogo za fasihi kama hadithi fupi. Alizidi kueleza kuwa vijana wameanza kukumbatia fasihi zaidi kuliko wazee kwa maana maudhui kama vile mapenzi ya kisasa, masuala ya uhalifu, ugaidi, na maisha ya wanafunzi wa vyuo vya anuai na vile vikuu huingiliana na maisha yao. Haya masuala Sanga ameyawasilisha ndiyo yamechochea ukuaji wa FYV nchini Kenya kwa sababu wanafasihi wanashughulikia mabadiliko katika jamii kwa kuandika tungo zinazowalenga wahusika na vijana ndio wengi zaidi.

### 1.7 Upeo na Mipaka

Utafiti huu utajishughulisha na ufafanuzi wa dhamira na wahusika katika riwaya za vijana na kubainisha jinsi vipengele hivi vinavyoakisi sifa za FYV kwa kurejelea riwaya teule za *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona*. Utafiti huu utaangalia dhamira zinazohusiana na riwaya za vijana. Baadhi ya dhamira katika riwaya za vijana ni mapenzi, ndoa za mapema, nafasi ya msichana katika masomo, ukombozi wa vijana, matumizi ya dawa za kulevya na matumizi ya teknolojia. Utafiti huu utajibana katika kuangalia jinsi dhamira inaakisi sifa za FYV kwa kutumia data kutoka kwa riwaya teule. Zaidi utafiti huu unajibana katika kuangalia usawiri wa wahusika vijana hasa wa umri wa miaka 12 hadi 21. Wahusika hawa ni wa kike na wa kiume kuonyesha kuwa jamii yote inawakilishwa. Katiaka usawiri wa wahusika utafiti huu utaangazia majina yao, maneno wanayoyasema, matendo yao, wahusika wengine wanasemaje kuwahusu, nafasi zao katika jamii, umuhimu wao, mitazamo yao, dhima zao, kukubalika kwao na usahili na uchangamano wao. Ili kufikia malengo haya, utafiti huu umejishughulisha na kusoma makala

yanayohusu dhamira na usawiri wa wahusika katia riwaya za vijana na zaidi umeangazia nadharia zinazohusishwa na maswala ya vijana na utanzu wa fasihi ya vijana.

Pamoja na kwamba imetajwa kuwa utafiti huu utajishughulisha na dhamira na wahusika katika riwaya za vijana katika FYV, hii haimaniishi kuwa utafiti huu umeangazia mambo yote yanayohusiana na dhamira na wahusika. Utafiti huu umejifunga katika utanzu wa riwaya na umeshughulikia kazi mbili tu za fasihi ya vijana za Mbatiah ambazo ni *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona*. Mifano na mkusanyiko wa data iliyohitajika imetolewa katika hizi riwaya mbili. Riwaya hizi zilichaguliwa kimakusudi kwa sababu zinaangazia masuala yanayowahusu vijana wa miaka 12 mpaka 21 na vijana hao ndio wahusika wakuu katika hizi kazi za kifani. Pamoja na hayo ni kuwa wahusika ni wa jinsia zote hivyo riwaya hizi teule zina data ya kuwakilisha jamii nzima.

**1.8 Msingi wa Nadharia**

Utafiti huu unatumia nadharia ya utanzu kwa sababu iko na misingi bora ya kuelewa na kuchanganua FYV. Nadharia ya tanzu huangazia sifa za tanzu zinazoifanya kuwa tofauti na nyingine japo kuna uhusiano fulani. Rowlett (2017) alieleza kuwa kila mfano wa nyenzo wa aina hubadili tanzu. Hili jambo ni la manufaa kwa sababu linasaidia msomi kuelewa sifa za FYV ambazo zimeufanya ukawa ni utanzu huru katika utanzu wa fasihi ya kijumla. Pia ni muhimu kuzingatia kuwa FYV ina tofauti chache ukilinganisha na fasihi ya watoto na ya watu wazima. Kwa mfano, wahusika, lugha, na maudhui huwa tofauti kidogo kwa hizi tanzu tatu za fasihi. Kwa hivyo, nadharia ya utanzu inaisaidia kuainisha uhusiano uliopo katika hizi tanzu ndogo tatu.

Zaidi, Dean (2018) alieleza kuwa nadharia ya utanzu ina uwezo wa kuyashughulikia matatizo mengi yanayohusiana na tanzu. Nadharia ya tanzu pia inasaidia kuonyesha maendeleo ya tanzu mbalimbali katika jamii. Kwa mujibu wa Rowlett (2017), nadharia ya utanzu ni mfumo

wa maelezo unaoshughulikia mwendelezo ya maandishi au matukio muhimu katika tungo mbalimbali. Zaidi ya mno, huu mfumo unaangazia mahusiano ya mifumo mingine katika tanzu mbalimbali. Haya maelezo ni muhimu kwa sababu yanasaidia kuelewa ukuaji wa FYV ambayo ni maendelezo ya fasihi ya watoto na watu wazima. Hizi fasihi mbili ndizo zimekuwa nguzo ya FYV. Kwa hivyo kutumia hii nadharia ya utanzu inaupa huu utafiti msingi bora wa kuelewa sifa muhimu za FYV.

Nadharia ya tanzu inasaidia kueleza vigezo ambavyo wasomi wanatumia kuanisha maandishi na sanaa katika makundi aina mbalimbali. Kuna tanzu chungu nzima za maandishi kama vile fasihi andishi na simulizi ambazo pia zina makundi madogo kama vile ngano, hadithi, vitendawili, riwaya, tamthilia, na ushairi. Haya makundi huchipuka katika jamii mbalimbali kulingana na mahitaji yaliyoko ila watunzi wa hizi tungo lazima wafuate vigezo mwafaka. Hii ni kumaanisha kuwa lazima wazingatie lile tatizo la kuainisha tungo zao katika makundi ambayo wasomi wameyakubali kutimika katika jamii nyingi ulimwenguni. Nadharia ya utanzu huwasaidia waandishi wa tungo mbalimbali kuelewa historia ya tanzu fulani na vigezo ambavyo wanafaa kuzingatia. Hili jambo ni la manufaa mengi maana linasaidia kuelewa historia ya FYV nchini Kenya na vile vigezo maalum ambavyo mwandishi wa riwaya teule nitakazozitumia alvyovizingatia.

Nadharia ya tanzu pia huangazia swala la mabadiliko ambalo linasababisha utunzi wa tungo mbalimbali. FYV imeweza kukua kwa sababu kuna mabadiliko mengi ambayo yamekuwepo katika jamii mbalimbali nchini Kenya ambayo yamewafanya waandishi wa fasihi kutambua maudhui mwafaka yakuangazia katika huu utanzu mgeni. Kwa mfano, lugha ya Kiswahili imekua kwa kasi sana na mamilioni ya watu wanaitambua katika ulingo wa kimataifa. Kwa hivyo, wasomi wengi wa Kiswahili wamegundua kuwa hiki ni chombo cha muhimu

kumfikia kijana wa Kenya na kumsaidia kutatua matatizo anayoyapitia katika maisha yake. Pia FYV imechipuka kwa sababu ya mabadiliko kadha wa kadha ambayo yanawahusu vijana moja kwa moja. Kwa mfano, maudhui ya uongozi wa kitaifa uwahusu vijana sana kwa sababu wao ndio wanaoadhirka vibaya wakati viongozi wanabuni miswaada inayowakandamiza. Kwa hivyo, mabadiliko katika jamii husababisha kujitokeza kwa tanzu nyingi za maandishi mbalimbali ikiwemo fasihi.

Waandishi wa fasihi hutunga tungo zao wakiwa na mlengwa wanayemkusidia kunufaika na kazi zao. Nadharia ya tanzu huwasaidia kumtambua mlengwa na yale ambayo ni ya manufaa kwao. Hii nadharia ni ya muhimu katika utunzi wa tungo za fasihi zinazowahusu vijana na hivyo itanisaidia kuchunguza jinsi mwandishi alivyoteua na kuangazia kundi la vijana katika vitabu vyake vya *Majilio ya Mkombozi* (2016) na *Kimbilio la Silona* (2021). Kundi la vijana ni la muhimu katika karne ya ishirini na moja kwa maana maisha yao ni tofauti ukilanganisha na yale ya watoto au watu wazima. Kwa sababu huu utafiti unaliangazia kundi la vijana ni muhimu kutumia nadharia ya tanzu kwa maana ndiyo inaeleza makundi ya walengwa katika tungo mbalimbali.

Nadharia ya tanzu pia ni muhimu katika kazi hii inayohusu FYV kwa sababu watunzi hutumia sifa maalum kakuza na kuendeleza dhamira na maudhui mbalimbali. Nadharia ya tanzu inawasaidia wasanii wanaojihusisha na FYV kuelewa uhusiano uliopo kati ya ile fasihi ya watoto na watu wa zima. Kwa mfano, huu utanzu unahitaji wasomi kuwateu na kuwasawiri wahusika vijana katika kazi zao za kifasihi ili kutimiza matakwa ya walengwa. Wanyela (2008) akimnukuu Bakhtin (1986) alieleza kuwa tanzu hutengamana kwa sababu zina miingiliano mikubwa katika kuyafikia malengo mbalimbali katika jamii. Wanyela (khj) aliwatambua Boas, Dell, Hymes, Radiri, na Bakhtin kama waanzilisha wa nadharia ya tanzu. Hii nadharia iliwasaidia

wanaanthropolojia kama Boas katika kazi kazi zao walipokuwa wanachunguza lugha asilia ya Marekena. Pia wanasayansi walianza kuitumia walipogundua umuhimu wake. Zaidi wanaenthrografia waliitumia nadharia ya tanzu kuchunguza umuhimu wa mazungumzo katika jamii. Hizi faida za huu utanzu ndizo zimeifanya hii nadharia kupata mahali maalum katika fasihi ya Kiswahili.

Watunzi wa tungo za FYV huangalia vipengele muhimu vya utanzu huu kabla ya kutunga kazi zao. Kwa mujibu wa Wanyela (khj) nadharia ya tanzu huwaleta pamoja watunzi na walengwa. Watunzi huchagua mada zinazowawezesha kujenga dhamira kubwa na ndogo na kuhakikisha kuwa zinafanikisha maudhui mbalimbali katika kazi za kifasihi. Zaidi nadharia ya tanzu huwasaidia watunzi wa kazi za kifasihi kutambua na kuelewa mtindo ulio bora katika kuwasilisha kazi na kufikisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Pia nadharia ya utanzu ni ya manufaa katika fasihi kwa maana inawasaidia watunzi kufahamu matarajio ya hadhira lengwa. Kwa mfano, katika FYV hadhira lengwa huwa ni vijana baleghe ambao hupitia changamoto nyingi kwa sababu ya mabadiliko mengi haswa ya hii karne ya ishirini na moja. Kwa hivyo watunzi huangazia haya masuala katika kazi na huandika kwa kusudi la kuwaelimisha walengwa. Pia huwapa tumaini katika maisha na kuwasaidia kujenga maisha yao ili yawe ya manufaa katika vipindi vya baada ya ujana.

Nadharia ya tanzu pia ina manufaa kwa msomaji kwa sababu inamfanya kuwa na uepesi wa kutambua kazi anayoisoma na kile anachokitarajia. Kwa mfano vijana wanapopata kazi za kifani za fasihi huwa na matarajio ya kukumbana na wahusika wanaowasilisha hali halisi ya maisha yao. Kwa hivyo, nadharia ya utanzu huwasaidia watunzi kutunga tungo zinazoafikiana na mahitaji ya walengwa. Zaidi nadharia ya tanzu inaongoza katika kazi hii kwa sababu tanzu mbalimbali huwa na sifa za kipekee zinazoweza kutambulisha kazi. Hizi sifa za kipekee hufanya

wasomi kugundua kazi za kifani na kuzianisha kulingana na makundi ambayo wameyakubali katika nyanja mbalimbali. Tanzu pia huwa na miundo ya hali ya juu na ambayo wasomi na walengwa wanaweza kueleza katika kazi za kifasihi. Kwa mfano FYV ina muundo ambao huangazia dhamira na maudhui yanayowahusu vijana katika maisha yao ya ujana. Kipindi cha ujana pia kina miaka maalum ambayo inaweza kuwatambulisha walenngwa ambao wasanii wa kazi za kifani huwalenga. Kwa hivyo hivi vigezo vya tanzu vinawalazimu waandishi wa tungo mbalimbali kujibana katika hali fulani ili kuwafikia walengwa kwa kuchagua dhamira, maudhui, na wahusika kwa njia kamilifu.

Kigezo cha lugha ni muhimu sana katika kazi ya kifasihi kwa sababu hiki ni chombo cha kupitishia ujumbe. Mtunzi hutumia lugha kujenga dhamira na maudhui kwa kuwasawiri wahusika katika mandhari maalum. Kwa hivyo lugha katika utanzu wowote ule huleta vipengele vingine pamoja na humsaidia mtunzi kuibua hisia mbalimbali katika mawazo ya msomi ama hadhira lengwa. Kwa mfano, katika FYV lugha ambayo waandishi wa riwaya wanaotumia aghalabu huwa changamano ikilinagnishwa na ile waandishi wa FYW hutumia. Pia hii lugha changamano huwasaidia watunzi kuwasawiri wahusika na kuwawasilisha kwa njia mwafaka ambayo wenzao katika maisha ya hali halisi wanaweza kuwaelewa na kujitambulisha nao.

Nadharia ya tanzu pia ni ya manufaa katika pendekezo la utafiti huu kwa sababu inasaidia kuonyesha jinsi maisha halisi katika jamii yanasababisha ukuaji wa tanzu ndogo za fasihi. Kwa mfano, mabadiliko ya teknolojia hufanya watunzi wa kazi za kifasihi kuwa na dhamira na maudhui mengi kuhusu vijana. Teknolojia imebadilisha maisha ya wanadamu pakubwa kwa njia mbalimbali ambazo zimewafanya watunzi kuangazia faida na athari zake kwa hadhira lengwa. Watunzi wa kazi za fasihi hujishughulisha na sifa za utanzu katika nyanja zao na hubuni kazi zinazokusudia kumfikia mlengwa moja kwa moja. Kwa hivyo hii nadharia ina manufaa mengi

katika kukuza na kudumisha dhamira na maudhui mbalimbali katika kazi za FYV kwa kutumia wahusika wakuu na wadogo.

Nadharia ya utanzu pia inapata nafasi kubwa katika hili pendekezo kwa sababu kazi za FYV hujitokeza kwa sababu ya masuala mengi ya kijamii. Kwa mfano, FYV inatoa majibu kuhusiana na yale mambo vijana wanapaswa kuyafanya ili kujikomboa na tamaduni zizokuwa na tija katika maisha yao. Kwa mfano ndoa za mapema huwathiri vijana haswa wa jinsia ya kike katika maisha yao ya sasa na ya baadaye. Watunzi wa kazi za fasihi wanaoelewa umuhimu wa utanzu hutunga tungo zinazoangazia maisha halisi katika jamii ya walengwa.

Nadharia ya tanzu inasaidia wasanii wa kazi za kifani na walengwa kugundua na kuelewa kuwa tanzu haiajasasishwa. Tanzu hubadilika badilika kulingana na mabadiliko yanayowakumba binadamu katika maisha yao ya kila siku. Hii ndio maana watunzi huzingatia sifa za tanzu za kazi yao ili kuleta muwala wa matini unaoeleweka kwa urahisi. Hiki kipengele kinaashiria kuwa mtunzi sharti atumia lugha inayomsaidia mlengwa kuelewa kazi fulani kwa uepesi bila ya kusumbuka kwa aina yoyote ile.

**Vipengele Vya Nadharia Ya Utanzu**

Nadharia ya utanzu ina vipengele vingi muhimu ambavyo vinafaa katika uchambuzi wa dhamira katika FYV. Kwa mfano, huu utanzu unashiria kuwa tanzu ni zaidi ya maandishi ya kifashi. Waandishi wa fasihi lazima washughulikie maswala ya kijamii kwa sababu hayo yana umuhimu mkubwa katika jamii yoyote. Hiki kipengele kitanisaidia kuangalia maswala ya kijamii ambayo yalisaidia mwandishi wa vitabu teule kushughulikia dhamira kama vile ndoa za mapema, mapenzi, utamaduni, na masomo ya vijana. Pia nadharia ya utanzu inazingatia kipengele kinachoeleza kuwa tanzu ni zaidi na fomu, mtindo, na maandishi. Wasomi wanaoshabikia nadharia hii wanaeleza kuwa watunzi wa tungo za fasihi lazima washughulikie yale mambo

yanayohusu jamii kwa wakati halisi. Huu usemi ni wa manufaa kwa sababu unasaidia waandishi kujumuisha mambo fulani muhimu yanayowahusu vijana. Kwa mfano kuna maudhui ya umaskini, ufisadi, na ukombozi dhidi ya uozo wa jamii ambayo nitayashughulikia katika sura ya tatu na ya nne.

Nadharia ya utanzu pia inaeleza ile dhana inayoashiria kuwa utanzu haujasasishwa. Tanzu nyingi za fasihi hujitokeza kulingana na matokeo fulani fulani katika jamii. Hii hoja ni muhimu kwa sababu fasihi ya vijana imechibuka kwa kuangazia yale matukio yanayotokea katika jamii mbalmbali. Kwa mfano kuna ya malezi ya vijana na haya malezi ni tofauti ya karne nne zilizopita.

**1.9 Mbinu za utafiti**

Utafiti huu ni utafiti wa kimaktabani ulio na mwelekeo wa kutoa taarifa. Katika utafiti huu njia ya ukusanyaji data ni kupitia usomaji wa maandishi anuwai yanayojumuisha vitabu vya kinadharia na maelezo kuhusiana na masuala ya vijana na fasihi ya vijana kwa jumla. Vilevile tasnifu za aina tofauti katika viwango vya uzamili na uzamifu zinazozungumzia masuala ya vijana zitasomwa. Pia matoleo na machapisho mengine yanayopatikana maktabani na katika mitandao ya kiusomi kuhusiana na masuala ya vijana, dhamira, wahusika na fasihi ya vijana yatapitiwa. Ukusanyaji data wa maktabani utafanyika kwa njia ya kusoma na kunukuu maelezo, kauli, madai, hoja mbalimbali, na maarifa yaliyowasilishwa katika kazi za kinadharia. Data hii ndiyo itatumika kutoa kauli, fafanuzi na hoja katika utafiti huu na kutoa idhibati na ushahidi.

Katika utafiti huu data zitazokusanywa ni pamoja na fafanuzi za fasihi ya vijana, fafanuzi za dhamira na wahusika, maelezo kuhusu sifa za FYV, fafanuzi na maelezo kuhusu nadharia za masuala ya vijana na utanzu wa fasihi ya vijana, makubaliano na mivutano ya uelewa wa fasihi ya vijana, na jinsi ambavyo dhamira na wahusika zinaakisika na kubainisha sifa za utanzu wa

FYV. Usomaji huo pia ulijishughulisha kukusanya data kutoka tafiti zilizofanywa kuhusu fasihi ya vijana na masuala ya vijana kwa lengo la kupata habari zaidi kuhusu mada kama vile kuelewa utambulisho wa vijana, mtazamo wa vijana katika jamii, changamoto wanazokumbana nazo, uhusika na usawiri wa wahusika katika kazi za fasihi, aina za dhamira na maudhui yanayohusiana na vijana. Data itakayokusanywa na usomaji huo itatumika kuonyesha ufafanuzi wa fasihi ya vijana, dhamira na wahusika katika riwaya za vijana, na jinsi ambavyo vipengele hivi vinaakisi sifa za FYV. Vilevile data hiyo itatumika kufafanua jinsi ambavyo vipengele hivi vinaakisi sifa za utanzu wa FYV kwa kurejele riwaya teule za *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona.*

# SURA YA PILI

## Sifa za Fasihi ya Vijana na Muhtasari wa Riwaya za Vijana za: *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona.*

## 2.0 Utangulizi

Sura hii itashughulikia sifa za Fasihi ya Vijana (FYV), muhtasari wa riwaya teule za vijana ili kuweka msingi wa uchunguzi wa dhamira na wahusika katika sura zifuatazo. Pamoja na hayo sura hii itajadili sifa za kiutanzu zinazohusishwa na FYV pamoja na kubainisha udhihirikaji wa sifa hizo katika kazi zinazorejelewa. Baadhi ya sifa ambazo tutazijadili ni pamoja na umri wa wahusika kuwa ni vijana kati ya miaka kumi na miwili hadi ishirini na mmoja, wahusika wakuu huwa ni vijana, kazi hizi hujihusisha na matatizo na changamoto zinazowakumba vijana na vijulanga, dhamira ya ukuaji na utambuaji, na migogoro kati ya vijana na wazazi wao. Riwaya za *Majilio ya Mkombozi* (2016) na *Kimbilio la Silona* (2021) zinaonyesha dhamira mbalimbali zinazowahusu vijana hasa wale wanaobaleghe na walio kati ya umri wa miaka kumi na miwili hadi miaka ishirini na moja. Dhamira hizi huwa zinatokana na masuala yanayowahusu vijana kama vile malezi, ushauri, elimu, mapenzi, afya, dawa za kulevya, na mengineyo. Nadharia ya tanzu ndiyo itakayotumika katika kubainisha dhamira zinazojitokeza.

## 2.1 Muhtasari wa Riwaya ya Kimbilio la Silona (Mbatiah 2021)

Riwaya hii inahusu mhusika mkuu wa kike kwa jina Silona. Ni kijana wa miaka kumi na saba. Babake silona anaitwa Machengo. Familia ya Silona ina watoto wengine na pia baba yake

alikuwa na wake wawili, wa kwanza aliitwa Nawila na wa pili ni Maria. Silona ana ndugu yake mkubwa anayeitwa Atweki wa Machengo na mke wake aliitwa Swafiru.

Maisha ya Silona yameangaziwa tangu Silona alipoachishwa shule kwa lazima kwa sababu ya kubakwa na mjomba wake na kupata mimba, anapotorokea kwa ndugu yake, anaporudishwa nyumbani kwao, anapotoroka nyumbani kwa babake huko Ugobo, kwenda misheni ya Gitego, hadi anaporudi na akaanza mradi wa kuwakomboa watoto wasichana kutokana na ubabe uliopo Ugobo.

Silona alishuhudhia dhuluma za babake kwa mama yake hasa kwa kuzidi kuwaambia apate watoto wengi la sivyo angeoa mke wa tatu. Katika hali hiyo Silona alikuwa na changamoto kwa sababu wazazi wake walikuwa wanaweka mikakati jinsi ambavyo angeolewa. Baada ya Silona kuona hali ya kukaa nyumbani kwao imekuwa ngumu alitafuta mbinu ya kujinasua kutoka kwa dhuluma zilizomkumba. Silona alifanikiwa kuongea na ndugu yake Atweki ambaye alijitolea kumrudisha shuleni ili aendelee na masomo yake ili atimize ndoto yake.

Silona alijaliwa kutoka nyumbani kwao kwa siri kuu na akaenda kuishi na ndugu yake Atweki. Huko ndiko alijaliwa kurudi shuleni licha ya kuwa baadaye alikumbana na changamoto kwa sababu idadi ya wanafunzi katika darasa lao ilizidi na akalazimika kuingia kidato cha nne kabla ya kumaliza kidato cha tatu. Pamoja na hayo ni kuwa Silona tena alikumbana na changamoto nyingine kwa sababu kuna mzee mmoja wa miaka sitini kwa jina Ngoteku aliyempenda kwa kuwa alikuwa msichana mrembo hivyo basi akataka kumwoa.

Silona akiwa kwa ndugu yake alijifunza mambo mengi kutoka kwa wifi yake aliyeitwa Swafiru. Kando na kujifunza kutoka kwa Swafiru alitumia maktaba ya Swafiru kusoma vitabu, majarida na magazeti yaliyomsaidia kujua mambo mengi. Huu wakati akiwa kwa kakake ndipo

alijifunza mapishi, uhusiano mwema na mambo ya ndoa. Pamoja na hayo ni kuwa Silona alifanya vyema shuleni na akawa nambari ya tatu.

Baada ya muda tunaelezwa kuwa Machengo, babake Silona, aligundua habari za maficho ya Silona kwa bahati. Kwa hivyo alifanya mpango wa kuenda kwa Atweki ili amrudishe Silona nyumbani. Hata baada ya juhudi zake hakufanikiwa kurudi na Silona nyumbani jambo ambalo lilimfanya akate kauli ya kuenda kwa baraza la *Wagambi*. Alipofika kwake alishauriwa na wazee asiende kwa *Wagambi* kwa maana itakuwa na aibu kwa maana Atweki alikuwa ni mtoto wake.

Siku moja Silona, Swafiru na watoto wake Filipo na Simoni walienda matembezi ili kuangalia mandhari. Walipotoka walimwacha Atweki akiwa amelala kwa sababu ya maruerue ya pombe aliyokuwa amekunywa siku iliyokuwa imepita. Hii ndiyo siku ambayo Ngoteku alikuja kuleta habari za posa za Silona. Hata hivyo mambo hayakumwendea vyema kwa maana Atweki alimwambia aache kucheza na watoto wa shule awaheshimu

Siku moja Silona akiwa anatoka kanisani alikutana na babake mdogo Ntibue. Alimwadaa na kumteka nyara ili amurudishe kwao nyumbani. Ntibue alifanikiwa kumrudisha Silona nyumbani kwa kutumia dawa za kumlaza na kuwa nusu maiti. Lengo la kumrudisha Silona nyumbani ni kutaka aolewe na mzee Ngoteku.

Silona alifanya mpango wa kutoroka nyumbani ili aepuke unyama wa kuolewa na mzee Ngoteku. Kupitia kwa usaidizi wa mamake mdogo, Maria, aliamua kutoroka na kutafuta usaidizi katika misheni ya Gitego. Safari ya kuenda mafichoni ilikuwa na changamoto si haba lakini Silona aliamua na akaenda huko. Akiwa katika misheni ya Gitego Silona alijikakamua na kutia bidii katika masomo yake na kufuzu vyema. Pamoja na hayo alijihusisha na shughuliza ziada kama vile muziki na utunzaji wa mazingira.

Baada ya Silona kuhitimu alikutana na kasisi Bagondi ambaye walipendana na wakafanya uamzi wa kuoana kwa kuasi sheria za kanisa lililowapa mafunzo. Silona na Bagondi walianza mpango wa kuwakomboa watu na kuwanasua kutoka kwa minyororo ya ukatili ya chama cha Watunza Siri Kanisani (WASKA) na wakaanzisha chama cha Watetezi wa Haki na Ukweli (WAHU).

Kupitia kwa Silona, mwandishi ameangazia masuala yanayowaathiri vijana wa kike katika jamii ambazo zina uababedume kama ile ya Ugobo anapozaliwa Silona. Masuala kama dhuluma, kubaguliwa kiuana, ubakaji, ndoa za mapema na za lazima, msongo wa mawazo, elimu ya msichana, urithi, na mapenzi yameangaziwa kwa kina. Pia mwandishi wa riwaya hii ameangazia matatizo yanayowakumba vijana wa kike hasa kutengwa kimasomo na kutokuwa na sauti katika jamii. Silona analelewa katika mazingira magumu ambayo mtoto wa kike hana sauti. Matatizo ya Silona yanaanza tu pindi anapolazimika kuacha shule baada ya kubakwa na kupata mimba ya babake mdogo Arunde. Mwandishi anasema kuwa masaibu ya mwaka jana yaliondoa mwanga wa matumaini maishani mwa Silona. Hata hivyo alipata funzo kwamba Ugobo ilikuwa ngome ya wanaume. Wanawake walikuwa ngomeni tu. Kazi yao ilikuwa ni kuwafurahisha wanaume ambao ndio wenye ngome. Silona alikuwa na miaka kumi na saba mamake anapomwambia kuwa ataolewa na mume atakayemtunza na babake ndiye angetengeneza kila kitu.

## 2.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* (Mbatiah 2016)

Riwaya hii inahusu vijana wawili wa Kiume; Getukwa, kifungua mimba katika familia ya Baikungi na Ilonkundemi, mtoto wa Ntoibuguta. Hii ni riwaya ya kisasa inayowahusu vijana wanaobaleghe na nafasi yao katika jamii. Riwaya hii inatuonyesha athari ya malezi kwa vijana baleghe. Zaidi inaonyesha mambo yanayofanyika nyumbani, shuleni, kanisani na jamii yote kwa

jumla. Kwa kiujumla hii ni riwaya inayoangazia wajibu wa wazazi, walimu na jamii kwa ujumla katika kuwaelekeza vijana wanaobaleghe. Mwandishi wa riwaya hii anazungumzia masuala yanayowahusu vijana kama vile malezi, athari ya dawa za kulevya, ushirikina, mimba za mapema, vifungo vya uhalifu, dhuluma, elimu, mapenzi kati ya vijana, utamaduni na mabadiliko yanayoletwa na vijana katika jamii.

Mwandishi ametumia wahusika vijana, kuonyesha jinsi wazazi hukosa kuwaelekeza vijana ipasavyo kwa mfano wazazi wa Ilonkundemi hawakumwelekeza vizuri. Zaidi riwaya hii inaonyesha jinsi vijana hujipata katika hali tata na ngumu wanapofeli kufuata ushauri wa wazazi wao na washauri wengine.

Tunaelezwa kuwa kulikuwa na mashindano ya mafahali yaliyofanyika katika uwanja wa Miwambo. Getukwa alileta fahali wao kwa jina la Mbogo naye Ilonkundemi akamleta fahali wa mjomba wake na huyo fahali aliitwa Kifaru. Ilonkundemi alitumia hila kupata ushindi kwa maana alimpa fahali wake Kifaru povu ambalo laamimika kuwa ni mazingaombwe. Kwa hivyo mchezo wa kupiganisha mafahali haukuleta burudani ila watu walienda nyumbani wakiwa wamesononeka naye Getukwa alihuzunika zaidi kwa sababu Mbogo alikuwa na macho mekundu kutokana na lile povu la mazingaombwe. Getukwa alifanya uamzi wa kuenda kumshitaki Ilonkundemi kwa alilolifanya, hivyo basi angesubiri baba yake atoke Nairobi ndipo apeleke mashtaka.

Getukwa alimweleza baba yake yote kuhusu aliyoyatenda Ilonkundemi na akakubali kupeleka mashataka mbele ya baraza. Baikungi alikutana na mke wake na wakazungumza kwa kina wakijaribu kutafuta sluhisho la ni kwa nini vita kutoka kwa Wapukorengonyi mchawi mkuu katika miwambo. Hata hivyo waliamua kuwa watapigana na maadui wao maana akutendaye mtende, simche akutendaye. Kesi ilifika kwa baraza na haki ilipatikana kwa sababu kulikuwa na

ushahidi wa kutosha. Ushindi ulirudishwa kwa Getukwa na Ilonkundemi akapigwa faini kwa sababu ya kutumia hila na kuleta mazingaombwe katika mchezo uliofaa kuleta burudani.

Msemangi kweli alikuwa ni mzee wa zaidi ya miaka mia moja licha ya kuwa miaka yake haijulikani vizuri. Mzee huyu alichukua muda wake na kueleza sababu za umaskini huko Miwambo. Sababu hizo ni pamoja na uchawi wa Wapukorengonyi maana watu wengi walitumia pesa nyingi kununua uchawi kutoka kwake na wachawi wengine. Sababu nyingine ni uganga kwa sababu watu waliporogwa walihitaji mganga awagangue. Pia utoaji wa kafara kwa sababu ya kuamini pepo wa nguvu mapembe. Zaidi kulikuwa na umasikini kwa sababu watu wa Miwambo walikataaa kujihushisha na kilimo biashara na kutunza mandahari mazuri ya Miwambo. Baikungu ni mmoja wa matajiri kwa sababu yeye alijihusisha na ukulima wa kahawa na kufuga ngombe wa gredi. Hata hivyo katika ukulima wa kahawa Wapukorengonyi alitumia hila kwa kuhonga ili apewe ushindi gushi.

Getukwa alichoshwa na utumizi wa hila wa Wapukorengonyi ili kupata ushindi kila mwaka. Aliamua kupiga ripoti kwa gavana wa miwambo ya kati. Lakini ili kupiga ripoti alihitaji ushahidi wa kutosha. Hivyo Getukwa alitafuta mbinu ya kupata data iliyohitajika. Alipata rafiki wake Nkundikelo akakubali kumsaidia ili waangamize ufisadi. Getukwa walipanga siku moja wakati Wapukorengonyi alienda harusi Nairobi wakaingia shambani kwake. Walihesabu mibuni na kujua idadi. La kushangaza ni kujua kuwa vizuu ndio walitumika kufanya kazi ya kupalilia na kutunza shamba. Wakati walipokuwa wakitoka shimoni kwa vizuu, Nkundikelo aliumwa na nyoka mwenye sumu mbaya. Getukwa alimbeba na kumpeleka nyumbani kwao ili apate matibabu kwa maana mamake alikuwa ni mganga wa kuangua walioteswa na wachawai. Zaidi ni kuwa baada ya vijana hawa kujua siri ya vizuu waliamua kutunza siri hiyo ili waweze kukamilisha uchunguzi wao.

Baada ya Nkundikelo kugongejeka baada ya kuumwa na nyoka hatimaye alipona na baada ya muda mpango wao uliosimama ghafla uliendelea. Waliweza kupata data ya uuzaji kahawa kwa kuenda katika ofisi ya kiwandani na kusema kuwa wao ni wanafunzi wanaofanya utafiti. Baada ya kupiga hii hatua Getukwa aliamua kumwandikia Gavana wa Miwambo ya Kati barua ilia toe malalamishi yake. Getukwa alisukumwa na wazo kuwa alikuwa ni kijana wa kuleta mabadiliko kwa kupigana na uovu, udanganyifu, ufisadi na uchawi. Tarehe ya kukaguliwa kwa mashamba ya kahawa Getukwa aliandika barua kuhusu ufisadi katika chama cha ushirika cha wakulima wa Miwambo. Gavana hakukawia alipopata barua alijibu upesi na kuahidi kukomesha ufisadi. Gavana alimtuma ofisa wakakutana na Getukwa ambaye ndiye mwandishi wa barua. Katika mazungumzo yao walikubaliana kufanya ukaguzi kwa njia ipasayo ili kuondoa ufisadi. Siku ya ukaguzi ilifika na ofisa alikuja jinsi alivyohaidi. Ukaguzi wa kina ulifanyika, ukweli ukajitenga na uongo. Shamba la Baikungi lilikuwa bora zaidi kuliko lile la Wapukorengonyi. Ofisa alirudi ofisini akaandika ripoti iliyochukulia Gavana kusema kuwa wale wakaguzi wapigwe kalamu ili kukomesha ufisadi.

Ilonkundemi aliingilia kufanya biashara baada ya masomo yake kuenda arijojo. Alifanya biashara ya kuuza mahindi na maharagwe katika soko la Miwambo. Biashara hii ilimfanya kuwa tajiri na pia akawa kijana aliyejitegemea na kuwasaidia wazazi wake. Licha ya kuwa babake alimwonya kuepuka na fitina hasa kusumbua familia ya Baikungi kijana huyu hakukoma kwa maana alisikiza sana habari za mjomba wake na kupuuza baba yake. Ilonkundemi walipanga na mjomba wake jinsi ya kumpa hasara Baikungi, ili walipize kisasi kwa sababu ya kufichua siri ya ufisadi wao. Ilonkundemi alienda na kunyunyuzia dawa ili ng’ombe wa Baikungi wakufe. Hata hivyo alipata majeraha mabaya usiku huo na kuumizwa zaidi na fisi waliokuwa wakitafuta

windo. Ng’ombe ishirini wa gredi wa Baikungi walikufa na habari hizo zilienea kijijini kama moto, polisi na madaktari wa mifugo waliitwa ili kufanya uchunguzi.

Siku moja Ntoibuguta alienda kwa Baikungi ili kuomba msamaha kwa niaba ya mwanawe na kusema kuwa mjomba wake alikuwa tayari kulipa hasara iliyotokea. Hata hivyo Shahiruzode alikataa na kusema kuwa ikiwa Wapukorengonyi angelipia lazima alipe maradufu la sivyo kesi ingeelekea mahakamani.

Maisha ya watu wa Miwambo yalizidi kuwa magumu kwa sababu ya imani juu ya Nguvumapembe. Watu walilazimika kuongeza kutoa kodi na kuongeza beberu mmoja licha ya kuwa hali ilikuwa ngumu na umaskini ulikuwa umezidi kijijini. Watu wengi walikosa huduma muhimu kama vile kuchota maji na kuenda malishoni kwa maana hawakutoa beberu na hivyo wangemchokoza Nguvumapembe. Waliopuuza na kuenda kuchota maji usiku waliuwawa na walinzi wa wakala wa Nguvumapembe. Wapukorengonyi aliandaa mchango ili apate hela za kulipa fidia ya shilingi ya milioni tano kwa hasara ya kuwaaua ng’ombe wa Baikungi. Watu wengi wageni wakubwa walikuja na wakachanga shilingi milioni tatu na laki tano za kumsaidia Wapukorengonyi kulipa fidia.

Siri ya Getukwa na rafiki yake Nkundikelo ilijulikana. Hivyo waliamua kusema kuwa waliingia katika shamba la Wapukorengonyi. Shahiruzode aliwapongeza sana kwa ujasiri wao na kusema kuwa ni hatua ambayo ilichangia kuondoa ufisadi licha ya ajali iliyotokea. Kwa upande mwingine babake Nkundikeleo aliwakemea na kusema kuwa hayo yalikuwa ni makosa makubwa sana kujaribu kuingia shambani mwa mchawi hatari. Marafiki hawa walifurahi kwa sababu walipata ushindi hakika. Waliendelea kujitayarisha kwa mitihani iliyokuwa mbele yao maana walikuwa kidato cha nne.

Tetesi za mwana wa Miwambo zilizidi kuenea kijijini kote na kuwasisimua watu wengi kwa sababu walijua kuwa mwana wa Miwambo angewasaidia kwa kuwaondolea kodi ya Nguvumapembe. Lakini wengi walishangaa kwa kukosa kujua mwana wa Miwambo ni nani na dalili yake ni gani? Babake Ilonkundemi alimwonya ajitenge na uongo kuwa yeye ndiye mwana wa Miwambo. Padre Yoluche alienda kwa Baikungi ili apate msaada awe na nguvu ya kuwalinda mayatima waliomtegemea. Baikungi alitoa msaada wa laki moja kwa sababu alisukumwa na wazo kuwa ni vyema kusaidia maskini na wasiojiweza. Baikungi alimwuuliza msimamo wake kuhusu mwana wa miwambo naye alisema kuwa mkombozi ambaye angekuja kusaidia watu ni Yesu Kristo. Getukwa naye alijua kuwa Ilonkundemi alikuwa anawadanganya wanakijiji kuwa yeye ndiye mwana wa Miwambo. Lakini alijisemea kuwa siku moja watakuja kujua ukweli halisi kuhusu mwana wa Miwambo. Getukwa aliamua kujiandaa na kujishughulisha na mtihani wa kitaifa maana ulikuwa umekaribia sana.

Getukwa alikuwa na matarajio makubwa lakini mambo hayakumwendea vizuri. Alipata ugonjwa wa kumkosesha usingizi na kupigana na jinamizi usiku kucha. Alipewa dawa za usingizi lakini hazikusaidia hali ambayo ilichukulia mama yake kuagua ili apata shida ilikuwa wapi. Baada ya Shahiruzode kumaliza shughuli majibu yalikuwa kuwa Getukwa ana dalili za mwito ili akatimize unabii wa Syontangi. Wazazi wa Getukwa waliamua kuenda kwa Musemangikweli ili awategulie kile kitendawili cha maini. Mhenga Msemangi kweli alikuwa amesubiri siku hii kwa hamu na hatimaye ilitimia. Alifurahi kuwa mwana wa Miwambo alikuwa amejulikana na kuanza kazi. Alitoa maelezo na kuwapa wazazi wake silaha ili wampelekee Getukwa apambane na Nguvumapembe hadi ushindi upatikane. Msemangikweli hakuwa na haja ya uhai tena maana alikuwa ametimiza haja yake. Aliwahidi akifa wasimzike lakini wachome nyumba yake na kuunganisha shamba lake na la Baikungi. Baikungi alipeleka ujumbe kwa

baraza la wazee kuwa Getukwa ndiye mwana wa Miwambo. Wazee walifurahi na wakahidi kutangaza huo ukweli ili uongo usienee kuwa Ilonkundemi, mpwa wa mchawi, ndiye mwana wa Miwambo.

Harakati za ukombozi wa Miwambo zilianza kwa kasi sana baada ya Getukwa kukubali mwito. Kwa upande mwingine Ilonkundemi aliendelea kuwa mkaidi na kujawa kiburi zaidi kwa sababu ya utajiri wake. Alimtusi Emira na kutusi familia yake kwa sababu Emira alikataa urafiki wake. Babake Ilonkundemi alimkana na kusema kuwa awe anajitetea maana amekataa kusikia maonyo yake. Getukwa alianza kazi ya ukombozi kwa kutakasa sehemu za huduma kama vile visima, misitu na viwanja vya Miwambo. Pia alipiga marufuku kodi ya kila boma ya kutoa kwa Nguvumapembe. Zaidi Getukwa alipanga jinsi ya kuwakomboa wale vizuu waliokuwa katika shamba la Wapukorengonyi ili warudi makwao wakiwa wazima. Ni mpangao ambao ulikuwa na changamoto lakini kwa ushirikiano wa Padre Yoluche, maskauti, mamake Getukwa na Nkundikelo mpango wao ulifanikiwa. Wapukorengonyi aliendа mlimani kutafuta nguvu kwa bosi wake lakini mambo yalienda mrama hakupata. Alirudi kijijini na kushaurina na mpwa wake ambaye maisha yalimkalia magumu, wakapanga wakatoroka kijijini kisirisiri. Getukwa aliendelea kupata umaarufu kuwa mwana wa Miwambo. Ukombozi ulianza watu walimwamini na wakawa na ujasiri kuwa hawatarudi utumwani tena.

### 2.3 Sifa Za Fasihi ya Vijana (FYV) Zinazojitokeza Katika Riwaya Teule

Kuna sifa mbalimbali ambazo zinatambulisha kazi kuwa ni Fasihi ya Vijana (FYV). Riwaya teule zinaakisi sifa hizo muhimu za FYV ambazo tutaonyesha na kuthibitisha kwa kutoa mifano mwafaka katika kazi hizi teule. Sifa tutakazozifafanua ni pamoja na umuri wa wahusika kuwa ni vijana kati ya miaka kumi na miwili hadi 21, wahusika wakuu ni vijana, Kwanza kabisa wahusika wakuu ni vijana wanaobaleghe kati ya umri wa miaka 14 hadi 18. Kwa mfano, katika

riwaya ya *Kimbilio la Silona* mhusika ni Silona ambaye ni kijana wa miaka kumi na saba. Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* kuna wahusika wawili wakuu ambao ni vijana wanaobaleghe. Wahusika hawa ni Getukwa ambaye ana umri wa miaka kumi na mitano huku mpinzani wake ni Ilonkundemi ambaye ni kijana wa umri wa miaka kumi na saba.

Sifa nyingine ni kuwa FYV inaandikwa kwa kusudi la kuwalenga vijana. Dhamira za kazi hizi huwa zinafungamanishwa na vijana na ujana. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* dhamira ni kuonyesha changamoto ambazo wasichana wanaobaleghe wanazopitia hasa katika masomo yao. Pamoja na hayo riwaya hii imeangazia elimu, mapenzi, matumizi ya dawa za kulevya na utambulisho wa vijana. Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* dhamira ni kuonyesha jinsi ambavyo vijana wawili wanapigania utambulisho katika jamii na swala zima la kukomboa jamii. Pamoja na hayo, kazi hizi huangazia matatizo ambayo huwakumba vijana wanaobaleghe. Zaidi, kazi hizi huangazia tajriba za vijana wanaobaleghe. Ni wazi kuwa riwaya hizi teule zinawalenga vijana wanaobaleghe na ni sahihi kusema hivyo kwa sababu usawiri wa wahusika na dhamira zinazokuzwa zinaonyesha hilo kwa njia ya moja kwa moja. Dhamira zinazowahusu vijana wanaobaleghe ambazo zimekuzwa ni pamoja na mapenzi, ndoa za mapema, elimu, na vijana kuleta ukombozi katika jamii. Riwaya hizi teule zinawafaa vijana wanaobaleghe zaidi kwa sababu mwandishi ameandika akiwa na lengo la kuwafikia.

Matukio mengi yanamhusu mhusika mkuu hasa kujaribu kutatua mgogoro. Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* mhusika mkuu Silona ndiye anahusika na matukio mengi na kutatua migogoro mingi. Kwa mfano, Silona anahusika na kupata mimba ya mapema, kuachishwa shule kwa lazima, kuozwa mapema na kwa lazima, kuleta mabadiliko kama kijana na kupinga mila zinazowakandamiza vijana wanaobaleghe katika jamii yake. Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* tunaona mhusika mkuu Getukwa ndiye anahusishwa na matukio mengi. Getukwa

anajitolea mhanga na kupinga ufisadi ulioendelea katika ukulima wa mbuni. Getukwa pia alijitolea kupinga ukandamizaji wa mchawi Wapukorengoni aliokuwa ametumia kufanya watu wa Miwambo kuwa watumwa na masikini. Mwishoni Getukwa anamalizia kuwa mwana wa Miwambo, hili linampa nafasi nzuri ya kuleta ukombozi katika jamii yake. Kwanza anawaua walinzi wa Wapukorengonyi yaani nyoka wabaya aliowatumia kutisha watu wa miwambo. Pia anakomboa vizuu ambao Wapukorengonyi alikuwa anawatumia kama wafanyikazi katika shamba lake. Vilevile aliweza kutoa na kubatisha kodi ya kutoa kwa ajili ya Nguvumapembe.

Baadhi ya masuala ya kidhamira yanayobainika katika kazi za kumbo hili ni kuwepo kwa mgogoro baina ya vijana na watu wazima aghalabu kuhusu suala zima la utambulisho. Riwaya hizi zote mbili zinaakisi sifa hii kwa kina. Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* wazazi wa Silona wanahusika lakini wanakinzana na Silona. Kwa mfano, wazazi wake wanataka Silona aolewe na mzee Ngoteku lakini hili ni kinyume na Silona. Pia wanataka Silona aache masomo yake lakini Silona anataka kuendelea na masomo yake hadi chuo kikuu. Wazazi wake wanataka kumritisha Silona kazi ya uganga lakini hii ni kinyume na Silona. Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* pia tunaona vijana wanakinzana na wazazi wao. Ilonkundemi anakinzana na baba yake na kufuata masharti na maagizo ya mjomba wake ambaye ni mchawi. Jambo ambalo mwishowe linafanya baba yake kumkana kuwa si mtoto wake kwa sababu ya tabia mbaya alizoziiga na kutekeleza uharibifu katika jamii ya Miwambo kama vile kuwaua ng’ombe wa maziwa wa Baikungi na pia kumtusi Emira na familia yake kwa sababu ya hali ya ukata waliokuwa nao.

Sifa nyingine ni kuwa fasihi ya vijana huandikwa kwa sauti na mtazamo mwa kijana. Mwandishi huwa anamsawiri mhusika na matukio kuelezwa katika nafsi ya kwanza. Vile vile mtindo na mbinu zinazotumika huwa zinalenga kuwavutia vijana wanaobaleghe. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* mhusika mkuu anawasilisha matukio katika nafasi ya

kwanza hasa anapoeleza kusu safari yake katika misheni ya Gitego. Hali hiyo ni sawia katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* ambapo Getukwa anajieleza katika nafsi ya kwanza.

Mbali na hayo FYV huandikwa na mtu mzima ambaye amekomaa. Mtu mzima huandika akiwa na lengo la kushughulikia maswala yanayowahusu vijana. Katika riwaya tunazoangazia mwandishi ni mtu mzima na ameandika huko akilenga vijana akiwa na kusudi la kuburudisha, kuelimisha, kukanya, kuonya na kukuza tajriba ya vijana wanaobaleghe.

# SURA YA TATU

## DHAMIRA KATIKA RIWAYA ZA VIJANA: *MAJILIO YA MKOMBOZI* NA *KIMBILIO LA SILONA*

### 3.0 Dhamira

Msokile (1993) anaeleza dhamira kuwa ni wazo kuu katika kazi ya fasihi. Fauka ya hayo anasema kuwa dhamira ni sehemu ya maudhui. Wamitila (2002) anaeleza kuwa dhamira ni jumla ya maana anayoivumbua mwandishi wa kazi ya fasihi na pia ni jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake wa kazi ya fasihi. Naye Jilala (2016) anaeleza kuwa dhamira katika kazi ya fasihi ni mawazo yanayojitokeza kulingana na matokeo mbalimbali kama vile ya kijamii, kiwakati, na mabadiliko ya kihistoria.

### 3.1 Dhamira katika Riwaya ya *Kimbilio la Silona*

Katika sehemu hii, tutaangazia dhamira zinazojitokeza katika riwaya ya Mbatiah ya *Kimbilio la Silona* na kuonyesha namna dhamira hizo zinavyoendana na maisha halisi ya vijana wanaobaleghe. Wamitila (2008) anasema kuwa, kazi ya watunzi na wasanii wa fasihi ni kuchukua matukio na visa halisi katika jamii zao na kuyawasilisha kiubunifu katika kazi za fasihi kama vile riwaya, tamthilia, hadithi fupi na ushairi. Mbatiah ni miongoni mwa watunzi wa kazi za fasihi, hususani riwaya, ambaye amewasilisha dhamira zinazohusu maisha ya vijana wanaobaleghe hasa kati ya miaka 11 hadi 21. Baadhi ya dhamira tutakazozieleza kwa kina ni

pamoja na ndoa za kulazimishwa, ndoa za mapema, mapenzi, malezi, elimu na matumizi ya teknolojia.

### 3.1.1 Ndoa za Kulazimishwa na za Mapema

Dhamira hii imejitokeza katika riwaya ya *Kimbilio la Silona*, ndoa hii ni ya mapema tena ya kulazimishwa kwa sababu Silona analazimishwa aolewe na mzee Ngoteku ambaye kiumri ni sawa na baba yake ambaye amebwagia chumvi.

Katika jamii mbalimbali ndoa ina umuhimu sana kama vile kupata watoto, kupata mwenzi wa maisha wa kutekeleza majukumu mbalimbali na mengine mengi. Hivyo kutokana na umuhimu wa ndoa katika jamii mbalimbali ililazimu watoto wa kike kuozwa mapema wakiwa wadogo tu, pasipo na hiari yao, maadamu wazazi wameamua kumuoza mtoto huyo wa kike. Mtoto hana uwezo wa kupinga hata kama hakupenda kitendo hicho maana hiyo ni kupuuza na kuwadharau wazazi jambo ambalo lingeleta laana maishani mwake. Mwandishi katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* anaonyesha jinsi ambavyo Silona anapangiwa ndoa ya lazima na baba yake na hata mahari yakatolea licha ya kuwa Silona alikimbia.

*"Alikuwa msichana wa miaka kumi na saba. Pamoja na udogo wake, dharuba aliyopigwa na maisha ilimpevusha mapema. Sasa alianza kuyafikiria maisha yake. Vile angejitoa katika shimo alimotumbukizwa. Shogake Sonkisa alimuhurumia sana, lakini hakuweza kumsaidia. Mamake mzazi alijitia kutoelewa kilichomtia kitumbo maji. "utaolewa na mume atakayekutunza. Babako atatengeneza kila kitu," alimhakikishia." Uk 1*

Dondoo hili linaonyesha kwamba, Silona alilazimishwa kuozwa na baba yake kwa kushirikiana na mamake. Tendo hili la kuozwa lilifanyika akiwa na umri wa miaka kumi na saba bila ya uamuzi wake bali kwa lazima ya wazazi. Kwa hivyo hili ni tendo la ukatili wa kijinsia

kwa maana tendo hili la ndoa za mapema huwanyima wasichana nafasi ya kupata elimu na kuwa na uamuzi wao wenyewe katika maisha.

Tendo la ndoa za mapema na za lazima, pia humfanya kijana wa kike anayebaleghe kuathirika kisaikolojia na kuchanganyikiwa ni nini cha kufanya katika maisha yake. Kwa mfano, Silona alipokatiziwa masomo ili aolewe jambo hilo lilimtatiza kwa maana mawazo yake yalikuwa kinyume kabisa na ya wazazi wake. Yeye alitaka asome ahitimu ili apate kazi ya kufanya ili ajikimu. Kwa upande mwingine wazazi wake hasa baba yake alikuwa na pupa ya kuwa tajiri kwa sababu ya mahari yake. Silona ni mfano wa vijana na vijulanga wengi katika jamii ambao wanapitia changamoto za kuozwa mapema ili wazazi wao wanufaike. Vilevile mzee Ngoteku aliyetaka kumwoa Silona ni mfano wa wazee wanaotumia mali yao ili kuwadhaa vijana wa kike wanaobaleghe pamoja na wazazi wao.

*"Usilie sana Mwami Machengo," Ngoteku alimfariji. "Morungu amekupa watoto wengi. Hata mmoja akiharibika, una mahali pa kukimbilia. Morungu amekupa na yule binti ambaye Ngoteku amekufa juu yake. Nimekuja kwako kuposa yeye. Ukikubali, mambo ingine yote itakuwa sawa. Mahari niko nayo tayari. Mori sita na fahali ine. Kwa sababu ya uzuri ya mtoto, nitasindikiza hiyo mahari na mbuzi tano" uk 70*

Kutokana na dondoo hili tunajiuliza maswali kadha wa kadha kama vile ni kwa nini wazazi wa Silona waliamua kufanya mipango ya kumwoza binti yao kwa mzee aliyejaa mvi kichwani ambaye hakuwa rika yake? Je, ni kuwa Mzee Machengo aliona kuwa Silona hatapata mwanamume wa chaguo lake, amabye angemwoa, mpaka wakaamua kumwoza kwa mzee? Je ni kuwa Mzee Machengo alikuwa na tamaa ya mahari na kutaka kuwa tajiri? Je mwanamke ni kiumbe duni wa kufanyiwa maamuzi tu na kuwa kinyago cha kuwafurahisha wenye ngome? Bila shaka kuna majibu ya haya maswali na yanaweza kuwa na namna mbalimbali. Kwa mjibu wetu

tunaona kwamba Silona aliafanyiwa mpango wa kuozwa mapema kwa sababu alikuwa amepachikwa mimba na mjomba wake na walitaka kuficha ili wanakijiji wasijue jambo hilo.

Kutokana na dondoo hilo hapo juu ni wazi kuwa kuna ndoa za kulazimishwa katika jamii nyingi ikiwemo hii ambayo mwandishi wa riwaya hii teule anataja. Wazazi wanaamini kwamba wana mamlaka ya kumpangia na kumwamulia mtoto wao maisha ya usoni, kisha mtoto anasalia kuwa hana haki ya kuchagua maisha ya ndoa anayotaka. Kwa kawaida Silona angekuwa mtoto wa kawaida angekubali nasaha ya wazazi atii kila jambo na kwa hivyo angekuwa mke wa mzee Ngoteku. Angefanya hivyo kwa kuwafurahisha wazazi wake lakini Silona alikuwa amekaramka na kwa hivyo akasema kuwa afadhali kufa kujaribu kutoroka badala ya kuzimia uhai wake mwenyewe kwa kujitia kitanzi au kwa kuolewa na mzee aliyejaa mvi. Silona aliamini kwamba enzi ya ndoa za mapema na lazima ilikuwa imepita.

Hata hivi sasa katika jamii nyingi kuna baadhi ya wazazi ambao, huwachagulia watoto wao mume au mke hata kama si kwa kiasi kikubwa kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Wazazi wengine ni kama Mzee Machengo, huwa wanamchagulia mtoto wao mke au mume kwa sababu wanaona utajiri na hadhi ya familia. Wengine pia huwachagulia watoto wao wachumba kwa sababu ya kusema kuwa wao ndio wanaojua mtu aliye na maadili mema atakayemlinda mtoto wao vizuri. Licha ya kuwepo kwa hao wazazi, watoto wengi wamefunguka macho na kukaramka kama vile Silona, hawakubaliani na swala la kuchaguliwa wachumba na kulazimishwa katika ndoa za mapema.

Kutokana na utandawazi na kupiga hatua kiteknolojia watu wameweza kujifunza kupitia kwa mijadala ya mtandaoni na vyombo vya habari na mawasiliano kuwa hakuna haja ya kulazimisha mtoto katika ndoa ya mapema au kumchagulia mchumba. Wazazi na watoto kwa jumla wamepata elimu kupitia kwa kusikiliza redio, kuatazama runinga, video na mafundisho

mengi mitandaoni. Kwa hivyo riwaya hii ya vijana ya *Kimbilio la Silona* na riwaya zingine za vijana zianasaidia vijana na vijulanga kufahamu kuwa hakuna haja ya ndoa za mapema na za kulazimishwa.

Hata hivyo kuna sehemu za vijijini ambapo bado watu hawajapata elimu hii na kwa hivyo bado wana mtazamo kama ule wa Ugobo kuwa mwanamke ni kinyago cha kumfurahisha mwanaume. Kwa hivyo kuna bado asilimia fulani ya watoto wa kike wanaobaleghe wanaolazimishwa kuolewa mapema. Vilevile katika vijiji hivyo wazazi huchukua jukumu la kuwachagulia watoto wao wachumba kwa sababu zao kama vile utajiri na kufikiria kuwa watoto hao hawajakomaa kiakili. Kwa mujibu wa Lyatuu (2011) maisha ya ndoa yana changamoto si haba na kwa hivyo yana ugumu wake. Hivyo inampasa anayeingia katika ndoa awe ameamua mwenyewe na awe amekomaa kiasi cha kukabiliana na changamoto za ndoa. Kwa hivyo ni jambo la aibu ambalo Mzee Machengo alikubali kulifanya la kutaka kumwoza binti yake kwa mzee Ngoteku.

Vilevile maneno ya mzee Ngoteku yanaonyesha kuwa huyu mzee alikuwa na tamaa ya ngono kwa sababu ya urembo wa Silona. Wazazi wengine bila ya kutafakari zaidi, wanawaruhusu watoto wao wasichana wanaobaleghe kuolewa kwa lazima kwa wazee kama hao ambao huharibu maisha ya wasichana wadogo. Kwa kweli tamaa za ngono zina kikomo na zinapokwisha basi binti hawa wanaobaleghe huonekana si kitu chochote mbele za huyo mume mzee aliyesema anamfilia sana.

Silona alikuwa kijulanga wa miaka kumi na saba. Kwa hivyo, Silona alihitaji kijana barobaro wa rika yake ndipo wawe na uhusiano wa kimapenzi kisha waoane. Pendekezo la kuolewa na Mzee Ngoteku halikuwa wazo jema na kwa  kweli ni jambo ambalo linawakera na

kuwaudhi vijana wanaobaleghe kwa sababu ya kudhulumiwa na kunyanyaswa kimapenzi. Hili ndilo lilichukulia Silona kutoroka nyumbani kwao ili kuyanusuru maisha yake.

Lyatuu (2011) anasema kuwa wasichana ambao hulazimishwa kwa ndoa za mapema na wazee huwa na athari nyingi katika maisha yao. Kwanza kabisa athari mbaya ni ile ya kisaikolojia ambayo inaweza kumfanya msichana anayebaleghe kuchukua maamuzi ya kupoteza maisha yake. Kwa mfano Silona aliposika habari za kuolewa na Mzee Ngoteku na kuambiwa kuwa mahari yamekwisha tolewa alifikiria kujitia kitanzi ili kuuzima uhai wake. Hii ni hali ambayo huwafanya vijana na vijulanga wengi kukosa raha na tumaini katika maisha yao na huamua kufanya maamuzi magumu ambayo huelekea kumwathiri mhusika vibaya. Haya yanathibitika pale ambapo mwandishi anaposema:

*"Ndipo Silona alipotambua dharura ya kutoroka. Wazo la kuwa MKE WA NGOTEKU lilimfanya atake kujitia kitanzi. Lakini alighairi. Akaona heri kufa akijaribu kutoroka badala ya kuuzima uhai wake mwenyewe. Akamsihi mamake wa kambo amsaidie kutoroka." Uk 90*

Dondoo hili linaonyesha kuwa Silona aliposikia habari za ndoa ya lazima kwa mzee Ngoteku alikuwa na mawazo mengi yaliyokuwa yanapita akilini mwake. Mwandishi wa riwaya ya *Kimbilio la Silona* anajenga picha kwa wasomaji wake kuonyesha athari ya ndoa za mapema na za kulazimishwa bila ya msichana kupenda yeye mwenyewe. Zaidi athari za kiasaikolojia zinaonekena pale ambapo Silona alikuwa na hamu ya kutoka nyumbani na kukimbilia misheni ya Gitego. Mwandishi anasema:

*"Mama hakuna hatari iliyo kubwa kuliko ile inayonikabili sasa," Silona alisema kwa sauti iliyosheheni hisia. HATARI YA KUOLEWA NA ZIMWI. Nielekeze tu jinsi ya kufika Gitego. Nitasafiri usiku. Macheo yakinikuta barabarani, nitatumia njia ya msitu". Uk 91*

Dondoo hili na mengine hapo juu yanaonyesha kuwa ndoa za mapema zinamwathiri kijana anayebaleghe anapolazimishwa kuolewa. Baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yanapita akilini mwa kijana huyu ni pamoja na kuozeshwa mzee asiyemtaka, kurudishwa nyumbani kwao kwa kuwekewa dawa ya kulazwa, kukatiziwa masomo, na kuzimiwa ndoto yake ya maisha.

### 3.1.2 Mapenzi

Njogu na Chimerah (1999) wanaeleza kuwa mapenzi katika jamii hutazamwa na wengi kuwa mtu na mpenzi wake kama mume na mke, mtu na mzazi wake, mtu na ndugu yake, mtu na jamii yake na mtu na taifa lake. Kwa jumla mapenzi ni hisia nzito za moyoni zinazomfanya mtu athamini mtu mwingine, amjali, au avutiwe na mwenzake.

Mwandishi wa riwaya ya vijana ya *Kimbilio la Silona* anaikuza dhamira ya mapenzi kwa njia mbalimbali lakini namna kubwa ni mapenzi ya kiuhusiano baina ya mwanamke na mwanamme. Silona ni msichana mrembo na mzuri kama alivyopambwa na mwandishi. Silona alitamani sana kuwa na mapenzi baina yake na kijana wa umri kama yeye ili ayafurahie maisha. Na alipokutana na Bagondi ndoto yake ilitimia.

*"Sista Silona. Nakuomba uamini maneno nikuambiayo. Kukutana na kuzungumza nawe huwa kila mara kunaniletea furaha ambayo haina kifani. Mimi ni mtawa kama wewe. Hivyo mahusiano kati ya jinsia tofauti ni bahari kubwa kwangu.." Uk 125*

Katika dondoo hili, tunaona kwamba Silona anakutana na kijana ambaye anavutiwa naye kimapenzi na anafurahishwa naye. Ni kinyume na ilivyokuwa kwa mzee Ngoteku, Silona anasema kuwa kwa kweli ana hisia kama za Bagondi na alikuwa tayari kumpenda kwa dhati. Pia katika dondoo hili tunaona kuwa hawa vijana wawili walikuwa wamesumbuka kimapenzi kwa sababu hawakufanya uamzi wao kwa hiari kuwa watawa lakini ni kwa sababu ya hali ngumu

iliyowatorosha nyumbani. Hii ni hali ambayo inawakumba vijana wengi kwa kuwa wanafika umri ambapo wanataka yule ambaye watapendana naye kwa dhati.

Mwandishi wa riwaya hii pia anaonyesha katika ulimwengu wa hadithi kuwa umbo la mwanamke ni la muhimu sana kwa maana linaweza kumfanya mwanamke aweze kupendwa au kutopendwa na wanaume. Wanaume wengi huvutiwa na umbo zuri la mwanamke na sura yake nzuri, kwa upande mwingine mwanamke hawezi kupendwa na wanaume na hivyo huenda akapoteza bahati ya kumpata mwanaume anayempenda. Wanaume wa siku hizi hasa vijana wanaobaleghe huangalia sana umbo la mwanamke kwa hivyo hilo limechangia hata wasichana wanaobaleghe kutafuta mbinu za kuwa na umbo la kuvutia wanaume. Suala la tabia na haiba ya mwanamke vimekuwa si kipaumbele katika vijana wanaobaleghe. Hili linadhihirika wazi kwa sababu Silona alipendwa sana kwa sababu ya umbo lake zuri.

*"Ngoteku ….Alipomuona Silona mara ya kwanza, mwili wake uliyumbishwa na hisia yenye nguvu za ajabu. Alisimamisha gari kando ya barabara ili amwangalie vizuri. "Kama ni kuumba Mungu kafikia kikomo kwa msichana huyu" alikiri kimoyomoyo…Nikimpata kidosho huyu mzuri kama malaika, nitamwoa kama mke wa pili." Uk 19*

Katika dondoo hili inajitokeza wazi kuwa Ngoteku alivutiwa na Silona kwa sababu ya umbo lake na uzuri wake. Hii inatuonyesha wazi kuwa wakati mwingine wasichana wanaobaleghe huingia kwa mitego ya mapenzi kwa sababu ya maumbo yao mazuri baada ya kuvunja ungo. Silona ni mfano wa wasichana wengi ambao wanajikuta katika mtego wa aina hiyo. Kwa sababu wengine humalizia babaya kama vile kubakwa, kama alivyobakwa Silona na Arunde mjomba wake.

Kasisi Bagondi pia alivutiwa kwa sababu ya urembo na uzuri wa Silona. Hili linathibitishwa katika dondoo lifuatalo.

*“Kwa sababu fulani, alizidi kuvutiwa naye. Kweli Silona alikuwa matlai shamsi. Wanaume wengi walivutiwa naye. Lakini klichomvutia Bagondi sio uzuri wa sura tu. Ulikuwa kama mvuto wa kimaumbile..Uk 123*

Kwa hivyo katika dondoo hili mwandishi anaweka wazi kuwa wanaume wengi katika karne hii huvutiwa sana na wanawake ambao maumbile yao yanaonekana kuwa ni mazuri na ni kivutio cha macho. Kwa maoni yetu, tunaona kuwa ndio maana vijana wasichana na wana wa kike huchukua muda wao kujirembesha kwa kutumia vipodozi vya macho, makucha, midomo na zaidi hata kumeza vidonge ili waongeze kimo huku wengine wakinunua nguo za kuchora maungo yao ili waonekane vizuri na kuwavutia wanaume.

**3.1.2.1 Mapenzi ya Kasisi Bagondi kwa Silona**

Kasisi Bagondi alikuwa na mapenzi makubwa kwa Silona na pia Silona alimpenda huyo kasisi kwa dhati. Kasisi Bagondi alimpenda Silona kiasi cha kuamua kuasi dini na utawa ili amwoe binti huyo anayemwona kama malaika. Lilikuwa ni jambo gumu na uamuzi mzito lakini waliamua kufanya hivyo kwa nia ya kutakasa na kusafisha dini kwa sababu ya unafiki mwingi uliokuwa ukidhihirika kanisani.

Bagondi alimpenda Silona kiasi cha kumwita kwa mazungumzo hata kupitisha masaa ya kuenda kazini. Bagondi aliamini kuwa Silona alikuwa ameumbwa akaumbika na alikuwa na tabia nzuri na uwezo wa ajabu katika masomo yake. Katika kutuonyesha kuwa Bagondi walipendana na Silona, mwandishi anasema:

*Kwanza, walikiri kwamba wanapendana. Pili, walikubaliana kwamba wataoana baada ya kukamilisha uasi mwingine. Uasi ambao ulikuwa mwendelezo wa maasi waliyoyafanya tangu*

*utotoni mwao. Maasi ya kuvunja silisili ambazo walifungwa na mila na desturi zilizochakaa. Waliamua kuasi maisha ya utauwa baada ya kufanya maandalizi kabambe." Uk 145*

Dondoo hili, linaonyesha kwamba Bagondi alimpenda sana Silona na vivyo hivyo Silona alimpenda sana. Ndio maana wakaamua kufanya maasi ili waweze kuoana na kuwa mume na mke. Maelezo ya dondoo hii yanaonyesha kuwa wote waridhika na mapenzi yao na hakuna yule aliyesukumwa kwa kulazimishwa bali kila mmoja ilikuwa ni kwa hiari. Tunasema hivyo kwa sababu hatujaonyeshwa mahali ambapo Bagondi na Silona wanapigana au kulalamikia mapenzi yao bali wanapendana kwa dhati na kuishi kwa amani huku wakishirikiana kuleta mabadiliko katika jamii.

Pia tunaona upendo wa Silona kwa Swafiru. Silona alikuwa anampenda sana Swafiru kwa sababu ya ukarimu wake na uelekezi aliompa. Pamoja na hayo ni kuwa Swafiru alikuwa na bidii katika kazi yake ya kujaribu kumtetea mwanamke ili aweze kupata hadhi katika jamii. Vilevile Silona alimpenda Swafiru kwa kuwa alikuwa anampa ushauri wa mambo mengi yakiwamo ya ndoa. Haya yanathibitika katika dondoo ifuatayo.

*"Silona alijifunza mengi kwa Swafiru. Mara nyingine alishangaa jinsi wifi yake alivyopasua maneno. Mwanzoni aliogopa kuongea naye juu ya maisha ya ndoa. Kutokana na udogo wake, aliona haya kuzungumzia mada hiyo na mtu mzima kama vile Swafiru. Lakini walikuja kuzoeana kabisa. Uk 35*

Dondoo hili linaonyesha mapenzi ya Silona kwa wifi yake Swafiru kwa sababu alichukua muda kumfunza na kumweleza mambo muhimu kama maswala ya ndoa. Zaidi ni kuwa Swafiru alipenda kumwambia Silona ukweli bila kuwa na unafiki wowote. Kila mara Silona alipomkumbuka Swafiru alijawa na furaha kwa sababu Swafiru alikuwa ni kielelezo chema kwake. Hii inadhihirika wazi kuwa hata baada ya Silona kukimbilia katika misheni ya Gitego

alikumbuka kumwandikia Swafiru barua ili kumpasha habari ya mambo aliyokuwa amekumbana nayo na kumweleza jinsi hali ilivyokuwa kule Gitego.

*"Wifi, wewe ni mmoja wa watu walionifaa sana maishani. Siwezi kukulipa lakini Mungu atanilipia. Wewe na mumeo, endeleeni kuwasaidia akina Silona wa Ugobo. Mungu atawabariki. Nilikuwa na azma ya kuendelea na masomo hadi chuo kikuu. Nilikuwa na ndoto ya kusomea uandishi wa habari. Yote haya yameenda arijojo…" Uk 96*

Katika dondoo hili Silona anamkumbuka wifi yake kuwa mtu wa maana katika maisha yake. Hili ni wazi kwa sababu amemtetea na kumshauri kama msichana anayebaleghe na anayenyanyaswa na utamaduni wa Kigobo. Vilevile katika dondoo hii ametaja kuwa alikuwa na azma na kusomea uandishi wa habari ili awe kama Swafiru wa kuwatetea watoto wa kike ambao wananyanyaswa na utamaduni.

Silona alikuwa na mapenzi kwa Swafiru na ndugu yake Atweki kwa ukarimu waliomwonyesha ili kuokoa maisha yake ambayo yalikuwa hatarini hasa kuozwa kwa lazima na babake. Pia alimpenda mamake wa kambo kwa kumshauri akimbilie katika misheni ya Gitego. Licha ya kuwa kutokana na kumkomboa Silona kulipelekea Maria kupigwa hadi akafa baadaye kwa sababu ya maumivu makali aliyopewa na mume wake, Silona bado alimpenda na akahahidi kuchukulia babake hatua kwa kumuua mamake wa mdogo.

Dhamira hii ya mapenzi imeendelezwa sana na mwandishi wa riwaya ya *Kimbilio la Silona*. Kuna mapenzi ya ngono ambayo huwaathiri vijana wengi wanaobaleghe na ambayo mfano wake ni Silona na Bagondi. Pia kuna mapenzi ya mtoto na mzazi, ndugu na ndugu, marafiki na mapenzi kwa jumla yasiyo na hisia za ndoa kama vile mapenzi kati ya Swafiru na Silona.

### 3.1.3 Dhamira ya Utamaduni

Utamaduni ni jumla ya mambo yote yanayobuniwa na jamii ili kukidhi utashi na maendeleo yake. Jilala (2016) anasema kuwa utamaduni ni mwenendo wa maisha ya jamii fulani, jinsi ambavyo jamii hiyo hutazama mambo, na taratibu za jamii za kuendesha shughuli zao kila siku zinazowatofautisha na jamii nyingine. Kuna vigezo muhimu vya kutambulisha utamaduni wa jamii navyo ni mila na desturi, lugha, sanaa, kichezo na historia ya jamii. Katika kusoma kwetu tumegundua kuwa mwandishi wa riwaya ya *Kimbilo la Silona* ameonyesha athari za utamaduni hasa katika vijana na vijulanga. Ametumia mhusika Silona, kuonyesha jinsi ambavyo utamaduni wa mfumodume umemfanya kuwa mhasiriwa katika jamii yake.

Silona anapitia changamoto za kubakwa na mjomba wake kisha anapata mimba na kujifungua. Pia anakutana na changamoto ya kuachishwa shule na masomo yake kukatizwa kwa sababu ya ujauzito wake. Vilevile anapata changamoto ya kutaka kuozwa kwa lazima. Ndiposa Silona anaamua kutorokea kwa ndugu yake Atweki. Hapo ndipo Atweki alimwambia kuwa kutoroka nyumbani ni kuasi mila.

*"Kuasi babako ni kujitafutia laana."*

*"Mimi sijali tena hayo mambo. Ya sijui laana, mila, miiko…. Kwa nini vitu hivi havijanitoa katika mateso yote niliyopata? Ni miko gani niliyovunja nikapata niliyopata? Au nilikuwa nimelaaniwa? Silona alilalama kwa uchungu na ujasiri. Uk 5*

Katika dondoo hili Silona anaonekana kuenda kinyume cha utamaduni na kusema kuwa yeye hafuati mila na miiko ya jamii. Dhamira hii ni ya muhimu katika fasihi ya vijana kwa sababu vijana wengi wanaobaleghe wanajitenga na mila za kijadi na kuegemea kuwa hayo yamepitwa na wakati. Msingi wa Silona kukataa kutilia maanani mila ulimsaidia kuepuka madhila makubwa ambayo yalikuwa yanamkodolea macho. Kwa mfano, asingetoroka nyumbani

na kwenda kwa ndugu yake Atweki basi hangepata nafasi ya kuendelea na masomo yake tena. Kwa hivyo wakati mwingi tunaona vijana wakijitenga na utamaduni na wengi hunufaika kwa sababu kuna utamaduni mwingine hutumika kunyanyasa vijana wanaobaleghe.

*"Swafiru alielewa Silona alichomaanisha. Alitanabahi kwamba kweli hadithi ile ilizungumzia mambo yaliyowaathiri vijana wengi wa Ugobo. Silona alikuwa mwathiriwa mmojawapo wa mila na desturi za enzi ya mawe. Utamaduni wa mwanaume juu, mwanamke chini. Baba mfalme na familia watumwa. Mume bwana mke mtumishi." Uk 36*

Dondoo hili linaonyesha wazi kuwa kuna utamaduni ambao unawaathiri vijana kwa njia hasi. Pia dondoo linalofuata linaonyesha kuwa utamaduni kama vile kuwaoza wasichana kwa ndoa za mapema unaleta madhara mabaya kama vile kifo.

*"Katika pembe moja ya Ugobo, kumezuka shani. Tanzia ya ajabu na ya kusikitisha. Tumezoea visa vya watoto kujitoa uhai kutokana na suitafahamu kati yao na wazazi. Mtakumbuka kile kisa cha majuma mawili yaliyopita. Kuhusu msichana aliyejiua kwa kumeza dawa ya panya. Haya yalitokea katika kijiji cha Njukine…." Uk 26*

Bagondi pia ni kijana ambaye ameathiriwa kwa sababu ya utamaduni wa kuwarithisha watoto kazi duni. Dondoo lifuatalo inathibithisha hili

*"Kisa cha leo kinahusu kuwarithisha watoto kazi duni. Uajabu wake ni kuwa safari hii sio mtoto wa kike anayehusika. Pia, mwathiriwa ni baba badala ya mtoto wa kiume anayehusika. Marehemu Nchalelu alikuwa mganga maarufu katika Kijiji cha Muringonye. Watoto wake watatu walikuwa wasichana ambao waliolewa kitambo. Kitindamimba ni mvulana aitwaye Bagondi..." Uk 28*

Kisa hicho kinaonyesha utamaduni wa kurithisha watoto kazi za wazazi ulileta athari mbaya kwa Mzee Nchalelu na mwanaye Bagondi. Visa kama hivi hupatikana hata katika jamii

ya sasa. Baadhi ya wazazi huwaamulia watoto wao taaluma watakazofanya kwa lazima. Vijana wanaobaleghe kama Silona na Bagondi walikuwa na uwezo wa kuchagua taaluma lakini wazazi walitaka kuwarithisha kwa lazima kazi zao. Kwa hivyo mwandishi wa riwaya hii ya *Kimbilio la Silona* anatuonyesha kuwa vijana wanapaswa kupewa uhuru wa kuchagua taaluma na kazi wanazotaka kufanya.

Thibithisho lingine ni pale ambapo mamake Silona alikuwa anataka kumrithisha kazi ya ukunga.

*"Kama mzazi yeyote wa Kigobo, Nawila alitaka kumrithisha mtoto wake kazi yake. Mtoto aliyekuwa amemchagua ni kitindamimba wake, yaani Silona. Kwa hivyo alianza kumfunza vipengele vya kazi yake tangu akiwa mdogo." Uk 13*

Dondoo hili linaonyesha kuwa Nawila, mamake Silona, alikuwa mkunga hodari aliyetambulika na kupewa mafunzo na serikali. Mzazi huyu alikuwa na nia ya kumrithisha mtoto wake kazi hii yake. Hali kama hiyo huleta changamoto kubwa kati ya wazazi wengi na watoto wao kwa sababu huwalazimishia kazi bila kuwashauri. Kwa mujibu wa mwandishi wa riwaya hii anasema kuwa hii ilikuwa ni nguzo mojawapo ya utamaduni wa Ugobo. Wakati mwingi watoto hujifunza hizo kazi wakiwa na nia tofauti na wazazi. Kwa mfano, Silona alikwa na nia tofauti na ya mamake:

*"Sababu ya kujifunza kazi hii ilitofautiana na ile ya mamake kumfundisha. Mamake alinuia iwe ndiyo kazi ya maisha yake. Ajipatie riziki kwayo katika utu uzima. Lakini silona hakuwa na nia kama hiyo. Alitaka kuendelea na masomo. Lengo lake lilikuwa kuendelea mpaka afikie kiwango cha kuchagua taaluma aliyotaka kuisomea. Uk 13*

Atweki kijana wa Machengo pia alikutana na hii changamoto ya utamaduni wa wazazi kuwarithisha watoto kazi zao. Tunaonyeshwa kuwa Atweki aliamua kufanya kazi tofauti na ile

ambayo babake alikuwa anataka kumrithisha. Kwa sababu Atweki alipenda kazi yake mwenyewe ndio maana akapata ufanisi mkubwa katika biashara yake na kupiga hatua kimaisha. Hili ni funzo ambalo mwandishi wa riwaya hii ya vijana anatoa kuwa vijana wakipewa nafasi ya kuamua kazi wanayotaka kuifanya itakuwa ni vyema sana ili wasije wakalazimishwa na wazazi kwa sababu ya utamaduni wa jamii yao.

### 3.1.4 Dhamira ya Nafasi ya vijana wa kike katika Jamii

Nafasi ya vijana wa kike katika jamii ni miongoni mwa dhamira ambayo inajitokeza katika riwaya ya *Kimbilio la Silona*. Silona ni kijana wa kike ambaye amezaliwa katika jamii ambayo kijana wa kike amekandamizwa na mfumodume. Mwandishi ametumia jamii ya Wagobo kuonyesha wanawake kuwa viumbe dhaifu ambao hawastahili kusema lolote ila kutii mume kwa kila jambo. Katika aya ya kwanza ukurasa wa kwanza katika riwaya hii inaanza na kuonyesha nafasi ya kijana wa kike. Mwandishi anaonyesha kuwa kijana wa kike hakuwa na sauti. Na ikiwa atakuwa na sauti ataangukiwa na mkosi. Pili katika riwaya hii mwandishi anaonyesha wazi kuwa vijana wa kike ni watumwa wa ngomeni kwa hivyo ni kama wao hawana haki ila tu kufuata mashariti ya wakuu wao ambao ni wanaume. Tatu anaonyesha kuwa kijana wa kike ni kinyago cha kumfurahisha mume ambaye ndiye mwenye ngome. Hii ndiyo jamii Silona anamozaliwa na ndio maana anakatiziwa mwanga wa matumaini kwa sababu ya masaibu yanayomkumba kama msichana aliyezaliwa Ugobo. Riwaya hii ina mchango mkubwa katika FYV kwa sababu inaaonyesha wazi kuwa kuna vijana ambao wanapitia masaibu ya mfumodume na hivyo kupoteza mwanga wa matumaini maishani mwao.

Maneno ya Mzee Machengo yanaonyesha kuwa mwanamke ni wa kuzaa na kulea watoto ili mwanaume apate heshima. Katika dondoo lifuatalo anasema:

*"Ilikuwa imejengwa mtindo sawa na zile nyingine mbili. Nyumba ya kulia ilikuwa ya Nawila, mke wa kwanza wa Machengo. Ya kushoto ilikuwa ya mke wa pili, yaani Maria. Ile ya katikati ilikuwa ya watoto wakubwa. Yaani wasichana ambao walikuwa hawajaolewa na wavulana ambao walikuwa hawajaoa….." Uk 10*

Kutokana na dondoo hili ni wazi kuwa kazi ya mwanamke ni kuzaa ili mwanaume apate sifa na heshima za kuwa mwanamume. Machengo anaawaambia wake wake wawili kuwa wakishindwa kuzaa waseme ili alete mke wa tatu. Hii inaonyesha kuwa mwanamke hana kazi nyingine ya muhimu ispokuwa kumzalia mume ili aheshimiwe.

Tena baadaye Machengo anaonekana akilalamika kuwa mke wake wa kwanza alimzalia wasichana wengi kuliko wanaume. Mwandishi anatumia jazanda ili kueleza hoja hiyo. Anasema:

"*Machengo alimuoa Maria alipotambua kwamba baada ya kifunguamimba wa kiume alifuatwa na watoto watatu wa kike, mkewe wa kwanza alishindwa kutimiza matarajio yake. Alilalamika kwamba ni aibu kwa mtu wa hadhi yake "kuwa na bustani iliyojaa vipepeo na kukosa nyuki wa kutosha." Vipepeo walivutia lakini walikuwa mapambo tu. Nyuki walikuwa jeshi la kulinda boma. Pia walizalisha asali ambayo ilikuwa na manufaa mengi. Mkabala huu wa Machengo ndio uliotawala miongoni mwa wanaume wa Kigobo." Uk 11*

Dondoo hili linaonyesha kuwa mwanamke ni wa kuzaa na si kuzaa wasichana bali wavulana ambao Machengo anawafananisha na nyuki. Wavulana hawa watakuwa na jukumu la kulinda boma na pili ni kuzalisha asali yaani kutafuta mali na kujaza boma. Machengo, ambaye mwandishi amemtumia kuwakilisha wanaume wa Kigobo, anaona wasichana kuwa ni vipepeo yaani kuwa wanavutia tu na hawana faida kubwa kama wavulana. Mwandishi anaonyesha kuwa vijana wanaobaleghe hasa wa kiume wanaweza kuathirika na kuwa na mtazamo kama ule wa wazee wa Kigobo kuwa mwanamke ni kifaa cha kumzalia mwanaume. Pili vijulanga wanaweza

kuwa na mtazamo kuwa mwanamke sharti azae wasichana na wavulana. Vileveile mwandishi anaonyesha kuwa kuna wanaume ambao husingizia mke hapati watoto ili anaoa mwingine swala ambalo huelekea kuvunja ndoa nyingi.

Kijana wa kike ameonekana kudharauliwa hata kama amefanya jambo zuri katika jamii. Swafiru alikuwa mtetezi wa wanawake ili waweze kutambulika katika jamii. Dondoo lifuatalo linasema:

*"Kupuuzwa kwa maonyo na ushauri wake kulimgadhabisha swafiru. Aliandika makala kwenye gazeti la Msemakweli. Akawashambulia waliomdharau mwanamazingira mkuu ulimwenguni. Kwa sababu duni ya kwamba alikuwa mwanamke. Akamalizia makala yake kwa kunukuu Biblia. "...nabii hatambuliwi kijijini mwake." Sadfa ilimpeleka kufanya kazi katika gazeti hili alipomaliza chuo kikuu. Alipoandika makala kumtetea shujaa wa kitaifa aliyeelekea kupuuzwa kwa sababu ya jinsia yake, bado alikuwa mwanafunzi.*

Dondoo hili linaonyesha wazi kuwa mwanamke mwanamazingira mkuu aliyetambulika ulimwenguni kote alikuwa amedharauliwa kwa sababu moja tu kwamba alikuwa mwanamke. Hii inaonyesha kuwa jamii ya Ugobo haikuwa inawatambua wanawake kuwa wanaweza kufanya mambo makubwa na mazuri na kutambulika ulimwengu mzima. Mwandishi anatumia muhuska Swafiru ili kupigania haki za wanawake. Hili ni funzo hasa kwa vijana wanaobaleghe wajue na kufahamu kuwa wanawake wana umuhimu katika jamii hata wa kuwa viongozi wa nyadfa muhimu.

Mazungumzo ya Mzee Ngoteku na mke wake kuhusu kuoa Silona kuwa mke wa pili yanaonyesha wazi kuwa kijana wa kike amepewa nafasi ya kudharauliwa. Mwandishi anaonyesha jinsi ambavyo mke wa Ngoteku anatulia mume wake akimwambia ataoa mke wa pili. Hili linaonyesha kuwa mwanamke hawezi kufanya uamuzi mbele ya mume wake. Mke wa

Ngoteku hana uwezo wa kufanya uamuzi wa kutokaa na kijana wa kike ambaye mume wake anataka kumwoa wakae katika nyumba moja. Zaidi ni kuwa Ngoteku anamtishia na kumwambia kuwa ikiwa ataleta fitina atapigwa. Tena tunaona kuwa mwanamke kazi yake ni kuolewa ili aje kumfurahisha mwanamume. Mfano Silona ni kijulanga lakini Ngoteku mzee wa miaka sitini anataka kuenda kumwoa ili aje kufanya mapenzi naye ambayo hana uwezo wa kumridisha huyu kijana anayebaleghe. Ngoteku anajibu kwa kumdhalilisha mwanamke kuwa hakuhitaji lolote ili kuoa mke wa pili hata wa tatu ila tu kumwarifu.

Katika mazungumzo ya Mzee Machengo na Mzee Ngoteku wanawapa vijana wa kike nafasi ya kuwa wajanja na wadanganyifu. Dondoo lifuatalo linasema:

*"Mgeni wangu, wahenga walisema damu ni nzito kuliko maji. Lakini damu yangu ile, imetiwa maji na ujinga. Mara nyingine najiuliza kweli Atweki ni mwanangu, au mamake alinicheza kayamba."*

*Ngoteku alimkatiza kwa kicheko. "Wanaume tunadanganywa sana na wanawake. Wanajifanya wanyonge lakini ni wajanja kama sungura," alisema Uk 70*

Dondoo hili linaonyesha kuwa wanawake si waaminifu katika ndoa. Wanadokeza hoja kuwa mwanamke ndiye tu anajua ikiwa mimba aliyo nayo ni ya mume yupi. Zaidi katika mazungumzo ya hawa wazee wawili wanazidi kusema kuwa mwanamume lazima amdhibiti mke. Ikiwa mwanamke ana uhuru kama vile mke wa Atweki basi hiyo ni kuwa mwanamke ana kimbelembele na amemkalia mume wake.

Kisa cha Rebeka pia kinaonyesha kuwa mwanamke amedunishwa na kuteswa katika jamii. Mwandishi anaonyesha kuwa mwanamke anatendewa unyama kwa sababu ya mila na tamaduni zilizo katika jamii. Babake mdogo alimpiga vibaya sana na kumwacha hali maututi kwa sababu anataka kuchukua shamba la marehemu wazazi wa Rebeka. Pili anaonyesha vile

Rebeka anatendewa unyama kwa kufukuzwa kwa sababu ni tasa. Kwa kweli mtu hana uwezo wa kujiumba au kujifanya kuwa tasa. Kwa bahati mbaya Rebeka kuwa tasa alifukuzwa kutoka kwa ndoa iliyodumu kwa miaka tisa. Mwandishi anaonyesha kuwa kazi ya wanawake ni kuolewa ili wazae na kulea. La kusikitisha katika hoja hii ni kuwa hata baada ya *Mwami* kufanya uamuzi bado babake mdogo alipuuza na kuendelea kumtendea Rebeka unyama. Mwandishi ametumia muhuska Rebeka ili kuonyesha kuwa wanawake na vijana wa kike hunyanyaswa na kutendewa unyama kwa sababu ya mila na tamaduni zilizo katika jamii na mfumodume.

Wanawake na watoto wasichana walikuwa wamedhulumiwa sana. Walitendewa mambo mengi mabaya ambayo yalichukuliwa kuwa ni sehemu ya utamaduni. Kwa mfano, Wagobo walikuwa wengi na walikuwa wametambua umuhimu wa kuwapeleka watoto wao shuleni. Tatizo lilikuwa kwamba wengi waliamini kuwa elimu ya juu ilifaa watoto wa kiume pekee na sio wa kike. Waliona kuwa kumfunza mtoto wa kike ni hasara kwa sababu waliamini kuwa wa kike ataolewa na kuondoka. Wagobo walihusisha umuhimu wa watoto wa kike na mahari na ndio maana waliwaoza watoto wao mapema. Mfano wasichana wawili wa Machengo walioenda kufanya kazi na kuongeza masomo katika vyuo vikuu mjini walilaaniwa na baba yao kwa sababu walikataa kuolewa mapema ili apate mahari.

### 3.1.5 Dhamira ya Elimu ya Vijana

Elimu ni mfumo wa mafunzo yanayopatikana shuleni, vyuoni na maishani. Elimu ni ufunguo wa maisha na uti wa mgongo katika karne hii ya ishirini na moja. Vijana na vijulanga wakipata misingi mizuri ya elimu wataweza kujiendeleza katika maisha ya kila siku. Elimu huwafanya vijana wengi wajikomboe kimawazo na kuwa na uwezo wa kujitegemea. Pamoja na hayo, elimu hutekeleza jukumu muhimu la kuwapa vijana maarifa na maadili yafaayo katika maisha. Elimu huwatoa vijana wengi na familia zao katika hali duni za maisha. Hata hivyo kuna changamoto

ambazo zinawakumba vijana na hatimaye kukatiza masomo yao. Changamoto hizo ni pamoja na umaskini ambao huchangia ukosefu wa karo na vifaaa vingine vya kusomea, mimba kwa wasichana wakiwa bado shuleni, tamaduni zilizopitwa na wakati kama vile ndoa za mapema na za lazima, ukosefu wa malezi na uelekezi mwema kutoka kwa wazazi na mandhari anamokulia kijana pia huchangia masomo yake.

Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona*. Mwandishi ameonyesha baadhi ya mambo ambayo yanawafanya vijana kukatiza masomo yao. Jambo hili la vijana kutokamilisha masomo yao linakuwa changamoto kubwa kwa maana wengi wa vijana wanakosa kufuzu ili kufikia ndoto zao ili kuleta mabadiliko ya muhimu katika jamii zao.

Mfano wa kwanza Silona, alisononeka sana kwa sababu masomo yake yalikatizwa kwa sababu ya kubakwa na kutiwa mimba na mjomba wake Arunde. Silona alikuwa ameenda kumsaidia mke wa Arunde wakati wa likizo kwa sababu afya ya mke wa mjomba wake ilikuwa imeharibika. Silona alikuwa kidato cha pili akitarajia kuingia kidato cha tatu mwakani. Masomo yake yalikatizwa na ndoto yake kuzimwa kwa sababu alikaa hospitalini kwa miezi mitatu. Na aliporudi nyumbani aligunduliwa kuwa alikuwa na mimba. Silona alipata taabu kubwa kwa maana wazazi wake walimkinga mjomba wake asipate adhabu yoyote. Wazazi wa Silona walitaka tu aolewe. Mwandishi anasema:

*"Kwa wazazi wangu, jambo moja tu lilibaki katika maisha yangu. Niolewe. Kwa hivyo walitaka niendelee kukaa nyumbani mpaka nipate mume anioe. Nilikataa wazo hili katakata. Sikuwaruhusu waiue ndoto yangu ya kuendelea na masomo. Sikutaka wadhibiti maisha yangu. Nikapanga kutoroka kwa kakangu ili anirudishe shule. Mpango wangu ulifaulu. Kakangu akanirudisha shule. Nilivuka vizingiti kadha. Hatimaye nikafanya mtihani wa kumaliza kidato cha nne." Uk 138*

Isingekuwa kwa bidii na uamuzi wa Silona hangerudi shule na hivyo ndoto yake ingezimwa. Vijulanga wengi wa kike wanakatiziwa masomo kwa sababu ya mimba za mapema. Kwa hivyo mwandishi anatoa funzo kutoka kwa maisha ya Silona kuwa kuvunjika kwa mwiko si mwisho wa mapishi. Pia katika dondoo hili tunaona kuwa kuna wazazi ambao wanachangia kuzima ndoto za watoto wao. Wazazi wa Silona badala ya kutekeleza jukumu lao ipasavyo walimvunja moyo na wakaanza kumtafutia mume wa kumwoa.

Sababu nyingine ambayo huwafanya vijana kukatiziwa masomo ni kuozwa mapema. Kwa mfano Silona alikuwa na hamu ya kuendeleza masomo yake hadi chuo kikuu ili awe mmoja wa wanahabari. Ndoto hii ilikatizwa ghafla kwa sababu baba yake alitaka kumwoza kwa lazima kwa mzee Ngoteku. Hii ndio ilimfanya Silona kutorokea misheni ya Gitego kwa sababu hakutaka kuolewa na mzee kwa lazima. Tunaelezwa kuwa:

*"Baada ya siku chache nikafahamishwa kwamba mzee fulani alikuwa ameniposa kwa babangu. Posa ikakubaliwa na akalipa mahari. Wakati wowote, angetuma genge la vijana kuja kunitwaa na kunipeleka kwake. Ilibidi nibuni mpango mwingine wa kutoroka. Ilikuwa dharura." Uk 138*

Kando na Silona kuna mfano mwingine wa wasichana wawili ambao masomo yao yalikatizwa na wakaozwa kwa lazima. Tuaelezwa kuwa:

*"Kadri alivyowazia wazimu wa Ngoteku, ndivyo alivyotambua kuwa ulikuwa wazimu wa jumuiya nzima. Aliwakumbuka wasichana wengine wawili kijijini ambao hivi majuzi walitolewa shuleni na kuozwa kwa wazee wenye navyo..." Uk 78*

Dondoo hili linaweka wazi kuwa wasichana hawa walikatizwa masomo yao ili kuolewa na wale walivyo navyo. Ni changamoto ya jamii kwa sababu wapo wazazi wanowaoza watoto wao ili kupata mahari. Pia imeonekana kuwa serikali na wanasheria hawakuwajibiki katika

kukemea ndoa za mapema na za lazima. Ikiwa wangefanya kazi yao sawasawa na kwa haki wangewasaidia hawa wasichana. Vilevile tunaona kuwa utamaduni ulichangia sana kwa kukatiza maono ya wasichana hawa kwa sababu utamaduni wa Ugobo ulikuwa na nguvu kuliko sheria. Ndivyo ilivyo katika jamii zingine maana bado kuna wasichana wanaoozwa kwa sababu ya utamaduni. Dondoo lifuatalo linaongezea zaidi ambayo tumekwisha sema:

*"Wagobo wanathamini mali itokanayo na mahari wanayolipwa binti zao wanapoolewa kuliko elimu yao. Ndiyo sababu ndoa za mapema ni jambo la kawaida. Sheria zinazokataza jambo hili zipo, lakini hazitekelezwi. Maofisa ambao ni wajibu wao kuzitekeleza wanapurukusha uhalifu unaotendeka kila uchao. Sababu moja ni kuwa baadhi yao wanakula tonge na wahalifu. Hivyo, wanawaficha badala ya kuwachukulia hatua. Sababu nyingine ni uzembe wao. Kwa mfano, hata baada ya gazeti hili kuchapisha kisa cha tanzia kijijini Njukine, wazazi wanaohusika hawajachukuliwa hatua yoyote." Uk 26*

Jambo lingine linalochangia masomo ya vijana kukatizwa ni wazazi kutaka kuwarithisha kazi kwa lazima. Wazazi hawawapatii vijana wao uhuru wa kuchagua taaluma wanazozitaka. Wengine huwaachisha masomo na kuwaweka kufanya kazi fulani. Mfano mzuri ni wa kijana Bagondi. Ikiwa Bagondi hangesimama imara masomo yake yangefika kikomo baada ya kufanya mtihani wa darasa la nane na akafuzu vizuri. Baba yake Nchalelu alikuwa anataka kumrithisha uganga. Tunaelezwa kuwa:

*"Kisa cha leo kinahusu kuwarithisha watoto kazi duni. Uajabu wake ni kuwa safari hii sio mtoto wa kike anayehusika. Pia, mwathiriwa ni baba badala ya mtoto wa kiume anayehusika. Marehemu Nchalelu alikuwa mganga maarufu katika Kijiji cha Muringonye.." Uk 28*

Dondoo hili linaonyesha kuwa kuna wazazi huwalazimisha vijana wao kuacha masomo ili warithi kazi fulani. Kwa mfano kuna vijana wengine huachishwa masomo ili kuingia idara ya

polisi uanajeshi na zingine. Mwandishi anatoa fundisho kwa vijana kuwa wana uwezo wa kukataa na kufanya uamzi imara wa kuendelea na masomo yao. Vilevile ni onyo kwa wazazi wasiwalazimishe vijana wao kufanya kozi fulani au kutaka kuwaritisha kazi wazipendazo.

### 3.2 Dhamira Katika Riwaya ya *Majilio ya Mkombozi*

Katika sehemu hii, tutaangalia dhamira zinazojitokeza katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* ili kuonyesha namna dhamira hizo zinavyoweka misingi ya masuala ya vijana na kuchangia ukuaji wa FYV. Kama ilivyodhihirika hapo mwanzo katika uchambuzi wa dhamira katika riwaya ya *Kimbilio la Silona*, mwandishi pia amebuni kisa katika ujenzi wa dhamira zinazohusu masuala ya vijana na vijulanga. Dhamira zilizopo katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* zimesheheni masula ya vijana. Dhamira hizo ni pamoja na matumizi ya teknolojia, mapenzi, elimu, malezi, ndoa za mapema, matumizi ya dawa za kulevya na ukombozi unaopatikana katika jamii kutokana na vijana.

#### 3.2.1 Dhamira ya Mapenzi

Mwandishi wa riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* ameonyesha dhamira hii ya mapenzi kati ya vijana. Vijana wengi huathirika kwa njia mbalimbali kwa sababu ya mapenzi wakiwa shuleni. Wengine humalizia kuwa na mimba za mapema, wengine huuwawa kwa sababu ya kudanganya katika mapenzi yao, wengine hupata magonjwa ya zinaa, na wengine hukatiza masomo yao kwa sababu mapenzi haya huchangia mimba za mapema.

Mwandishi ameonyesha kuwa kulikuwa na vijana ambao walikuwa wanapendana. Anasema:

*"Emira alikuwa msichana mweusi mwenye macho makubwa. Alisoma kidato cha kwanza katika shule ya Wasichana ya Agundekocha. Akiwa na umri wa miaka kumi na mitatu, alikuwa*

*mdogo kuliko Getukwa kwa miaka miwili. Walipendana sana. Shida yao ilikuwa jinsi ya kuendeleza uhusiano wao bila kuwaudhi wazazi..” Uk 59*

Dondoo hili linaonyesha wazi kuwa vijulanga huwa wanajiingiza katika mapenzi huku bado wakiwa ni wanafunzi. Mapenzi haya yana changamoto zake kama vile mimba za mapema kwa maana mwandishi anasema kuwa kijijini kulikuwa na wasichana wengi waliokuwa wametiwa mimba. Pia ni mapenzi ambayo yanawaletea wazazi na walezi balaa nyingi kwa sababu vijana w a umri huu wanaingia tu katika mapenzi bila kuchukua tahadhari zozote. Kwa hivyo mwandishi ametumia huu mfano kuonyesha kuwa suala la mapenzi ni mojawapo ya changamoto zinazowakumba vijana wanaobaleghe. Riwaya hii ya vijana ni ya muhimu katika FYV kwa sababu inawasaidia vijana kuzinduka na kuwajibika wasiingie katika mapenzi ya kiholelea ambayo yataleta balaa kubwa.

Emira mwanafunzi wa kidato cha kwanza, kando na kumpenda Getukwa alikuwa akipokea barua za mapenzi kutoka kwa Ilonkundemi. Tunaelezwa kuwa:

*“Nikwambie kitu?” Emira aliuliza huku akichekacheka na kuonyesha meno yake meupe. “Niambie,” Getukwa aliitikia. “Wavulana wengine siwaelewi!” “Gani hao?” Getukwa aliuliza kwa hamu. “Ilonkundemi,” Emira alijibu. Getukwa alishangaa. Emira alikunja uso kuonyesha kuchukizwa. “Amefanyaje?” Getukwa aliuliza. “Kunisumbua kwa barua za mapenzi. Utoto mtupu! Eti silali nikikuwaza. Wewe tu ndio dawa ya moyo wangu. Nitibu kwa kujibu barua hii. Upuuzi kama huo,” Emira alijibu. Uk 63*

Dondoo hili linaonyesha hali halisi ambayo vijana wanaobaleghe wanapitia. Kutokana na kupiga hatua za kiteknolojia, wengi wa wanafunzi wanawasiliana kupitia kwa vifaa vya kidijitali vya mawasiliano. Wengine huandikia baruapepe, arafa za simu, wengine mitandaoni kama vile

facebook, whatsapp, Imo, Instagram, Telegram, Tiktok na zingine. Vijana huandikiana jumbe za kimapenzi ambazo huwa na athari mbalimbali katika maisha yao.

Katika mazungumzo ya kina Getukwa na Emira walitaja suala la harusi kuonyesha kuwa uhusiano wao ulikuwa wa dhati. Tunaelezwa kuwa:

*"Naamini tukifikia umri ufaao tutaoana. Tutafanya arusi kama ile niliyoona ndotoni," Getukwa alijibu. Sauti yake ilionyesha kwamba hakufanya mzaha.*

*Emira alicheka. "Hayo ni mambo ya watu wazima. Mtoto wa shule unafikiria mambo ya ndoa?" Uk 65*

Dondoo hili linaonyesha kuwa vijana hawa wanafahamu fika kuwa wao ni vijana lakini wana matumaini kuwa watakuwa watu wazima na kuoana. Getukwa anatoa ahadi nyingi za mapenzi kwa Emira. Hii ndiyo hali halisi katika maisha ya vijana. Wengi ni wanafunzi lakini wanapeana ahadi za ndoa na kutarajia mambo mengi hapo baadaye.

Mwandishi anaonyesha kuwa kuna vijana ambao huwatusi na kuwadhuru wasichana wakati ambapo wamekataa kuitikia mapenzi yao. Mfano ni Ilonkundemi, alimtusi sana Emira kwa sababu ya kukataa urafiki wake. Jambo hili lilileta athari kwa baba yake kwa sababu alilazimika kutoa faini. Tunaelezwa kwamba:

*"Unaringa kwa sababu ya ujinga. Unaniona mimi mtu wa tabaka lako? Mimi ni mkwasi. Nani anataka urafiki na kisichana cha familia ya walalahoi? Nenda kwa Getukwa wako. Haikosi ametumia dawa za mamake kukuzuzua mpaka huna akili; hata kidogo! Unafikiri atakupa nini?". Uk 171*

Dondoo hili pia linaonyesha kuwa vijana wengine hutumia mali kuwadanganya wasichana. Mfano, Ilonkundemi anataka kutumia mali ili kumchanganya Emira awe mpenzi wake. Licha ya kuwa Emira alikataa katakata kuna wasichana wengine ambao hukubali

kudanganywa kwa sababu ya mali. Pili ni kuwa wanawatishia na kudhalilisha wasichana wanapokataa urafiki na wao. Ndio maana katika jamii ya sasa tunaona wasichana wengi hasa wa shule za upili na vyuo vikuu wanauwawa kinyama na wengine kuachwa na majeraha mabaya kwa sababu uhusiano wao wa kimapenzi umeenda arijojo. Pia wengine huamini katika dawa za waganga katika masuala ya mapenzi. Mfano Ilonkundemi anaamini kuwa Getukwa ametumia dawa za Shahiruzode ambaye ni mamake ili kumzuzuza Emira.

### 3.2.2 Dhamira ya Vijana na Ukombozi

Ukombozi ni jitihada ya kuokoa watu kutoka katika hali mbaya yenye mateso, unyanyasaji, ukandamizaji au hali ya unyonge. Kuna ukombozi wa kibinafsi na ukombozi wa kijamii. Katika ukombozi wa kibinafsi mtu binafsi ana uwezo wa kujikomboa kutoka kwa hali mbaya yenye mateso inayomnyima haki zake. Ukombozi wa jamii unahusisha watu wanaokaa katika jamii. Katika utafiti wetu tunaangalia jinsi ambavyo vijana wanahusika katika kuwasaidia watu kujinasua kutoka kwenye udhalimu na hali zinazowazuia kuishi vyema. Kuna aina za ukombozi ambazo vijana katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* walitimiza. Aina hizo ni pamoja na ukombozi dhidi ya umaskini, ukombozi wa kiuchumi, ukombozi wa maadili yasiyokubalika katika jamii, ukombozi kutoka kwa ufisadi, ukombozi kutoka kwa uchawi na aina nyingi za ukombozi. Kwa jumla tunaangalia jinsi ambavyo vijana wametumika ili kuleta ukombozi katika jamii. Mada ya riwaya ni *Majilio ya Mkombozi* kuonyesha kuwa jamii hii ilikuwa inasubiri mkombozi ambaye angewakomboa kutoka kwa dhuluma mbalimbali katika jamii yao.

#### 3.2.2.1 Ukombozi dhidi ya Umaskini

Mwandishi ametumia wahusika vijana kuonyesha jinsi ambavyo wanatia bidii ili kuwakomboa watu wa jamii yao kutokana na umaskini. Getukwa na Nkundikelo ni marafiki ambao

wamejitolea mhanga ili kupigana na unyanyasaji ambao unafanya watu wa jamii yao kuwa maskini kila kuchao. Mwandishi ametuonyesha jamii ya Miwambo watu wakiwa katika hali ya umaskini hata kukosa mahitaji ya muhimu kama vile maji ya kunywa na nyasi ya kulisha mifugo wao. Hali hii ya ukata wa watu wa Miwambo ni kioo cha jamii nyingi barani Afrika. Na pia wahusika hawa wawili ambao ni vijana wa kupigania ukombozi wanawakilisha vijana wengine katika jamii nyingi ambao wako mbioni kuwakomboa watu wa jamii zao kutoka kwa umaskini. Watu wa Miwambo walikuwa katika hali ya maisha magumu kwa sababu ya imani yao juu ya Nguvumapembe. Kupitia kwa wakala wake mchawi mkuu Wapukorengonyi watu walilazimishwa kutoa kodi ya boma hata kama hawakuwa nayo. Mwandishi anatueleza kuwa:

*"Wazee walipokuwa njiani wakirudi kijijini, waliongea kwa sauti za chini. Hawakuwa na furaha. Walielewa hali ya umaskini iliyotawala. Walijua kwamba agizo la kila boma kutoa beberu mmoja lilikuwa jambo zito lakini pia walijua ukali wa Nguvumapembe. Alikuwa na uwezo wa kuiangamiza jumuiya nzima. Ilikuwa lazima watu wafanye alivyotaka." Uk 112*

Dondoo hili linaonyesha kuwa watu wa Miwambo walikuwa na maisha magumu sana. zaidi ni kuwa hawakuruhisiwa kufaidi katika visima, mito, misitu, malisho ya mifugo kwa maana waliamini kuwa ilikuwa ni mali ya Nguvumapembe. Watu wengi walihangangika na hata wengine kufa kwa sababu ya kuumwa na walinzi wa Wapukorengonyi yaani nyoka wabaya wa uchawi wake.

Getukwa alikuwa kijana wa kuleta ukombozi. Pindi tu alipotajwa mwana wa Miwambo alianza kuwakomboa watu kutoka kwa umaskini wao. Tunaelezwa kuwa:

*"Jambo la kwanza kubwa alilofanya lilikuwa kutembelea sehemu zote zilizotoa huduma muhimu kwa watu; visima, chemichemi, mito na vijito, misitu ambamo watu walienda kutafuta kuni na uwanja wa Miwambo ambako watu walienda kulisha mifugo. .." Uk 175*

Dondoo hili linaonyesha kuwa Getukwa ni kijana aliyejitolea kuleta ukombozi katika jamii yake ya watu wa Miwambo. Ni funzo ambalo mwandishi anatoa kwa vijana kuwa licha ya kuwepo kwa changamoto za utamaduni na imani mbalimbali kama vile watu wa Miwambo walivyoamini Nguvumapembe bado vijana wanaweza kuleta ukombozi katika jamii. Getukwa aliboresha maisha ya watu wa Miwambo kwa maana waliacha kupoteza mali yao kwa pepo mwovu asiyetosheka. Vivyo hivyo vijana wa jamii ya sasa wana uwezo wa kuboresha maisha yao ikiwa watakuwa na ujasiri kama ule wa Getukwa.

#### 3.2.2.2 Ukombozi Kutokana na Ufisadi

Ufisadi ni ugonjwa ambao umezikumba nchi nyingi hasa zile ambazo zinakua. Ufisadi ni tatizo ambalo huangaziwa kila kuchao na vyombo vya habari lakini bado unazidi kuwa donda sugu. Taifa lolote ambalo viongozi wake uhusishwa na ufisadi huwa lina shida ya kupiga hatua hasa za kiuchumi. Kuna vijana ambao wameonekana wakijitokeza wazi na kupinga uovu huu ambao unawaangamiza wanajamii. Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* mwandishi anatumia wahusika vijana Getukwa na Nkundikelo kuonyesha vita dhidi ya ufisadi. Halikuwa jambo rahisi kulifanya lakini walijikaza wakajitolea mhanga ili kuleta ukombozi dhidi ya ufisadi. Watu wengi walijua ukweli lakini waliogopa kwa sababu mhusika alikuwa ni mchawi. Mwandishi anatueleza kuwa Getukwa alikuwa na lengo la kukomesha ufisadi:

*"Sheria zilizotumika katika mashindano ya wakulima zilikuwa kama za mashindano ya kupiganisha mafahali. Yaani, kifunguamimba ndiye aliwaongoza wakaguzi katika shamba la babake. Mpwa pia aliweza kuwapeleka wakaguzi kwenye shamba la mjomba wake. Getukwa ndiye aliwapeleka wakaguzi kwenye shamba la babake. Alikuwa amefanya hivyo mara tatu sasa. Kila mara, babake alishindwa. Kuponyoka kwa ushindi mara tatu kulimuuma sana. Hivi ni kwa*

*sababu alijua fika kuwa wakaguzi walikuwa mafisidi. Sasa aliamua kuukomesha ufisadi wao." Uk 24*

Kulingana na dondoo hili Getukwa aliamua kukomesha ufisadi. Halikuwa jambo jepesi kwa kijana umri wa miaka ya Getukwa kupigana na ufisdai lakini aliamua. Getukwa alikuwa amesoma habari za watu mashuhuri kama vile Mwalimu Nyeree, Kwame Nkurumah, na George Washington. Habari za hawa watu zilimtia moyo ili apiganie jamii yake na kukomesha ufisadi. Getukwa alihitaji data za kuthibithisha ufisadi na hilo alikuwa rahisi kwa maana lazima angeingia kwa shamba la yule mchawi Wapukorengonyi. Hata hivyo ukombozi ni wa kujitolea, vijana hawa wawili walipanga mipango yote na ikaingiliana. Waliamua kuingia katika shamba la Wapukorengonyi ili wakahesabu idadi ya mibuni. Pia walipanga wakaenda kwa kiwanda cha buni ili wakapate mizani ya wakulima misimu mitatu iliyopita. Baada ya vijana hawa kupata habari zaote na kuwa na idhibati za ufisadi waliandika barua kwa Gavana kumweleza ufisadi uliokuwa ukiendelea katika ukulima wa buni. Gavana alipopata barua alijibu na akamtuma Ofisa aliyekuja kusikiliza malalamishi ya Getukwa. Ofisa alikubali kuja kusimamia ukaguzi ili kuthibitisha madai ya Getukwa. Baada ya ukaguzi ilionekana wazi kuwa kulikuwa na ufisadi. Tunaelezwa kuwa:

*"Shamba la Baikungi lilikuwa bora kuliko lile la Wapukorengonyi. Ofisa wa kilimo akamtangaza kuwa msindi wa mwaka huo. Baadaye alirudi ofisini mwake kuandika ripoti juu ya udanganyifu wa wale wakaguzi. Akampekelekea Gavana ripoti hiyo. Gavana aliisoma kwa makini. Aligundua kwamba yale maelezo ya Getukwa juu ya ufisadi yalikuwa kweli. Akaagiaza wakaguzi wale wafutwe kazi mara moja. Uk 49*

Ni wazi kuwa vijana hawa walipitia changamoto si haba lakini walijitolea mhanga kuukomesha ufisadi. Getukwa na rafiki yake walifanikiwa kuleta ukombozi dhidi ya ufisadi. Ni

funzo kwa vijulanga kuwa wana uwezo wa kuleta ukombozi wa ufisadi katika jamii. Sekta mbalimbali zinapitia changamoto za ufisadi lakini vijana wakiungana na kutetea haki watamaliza ufisadi.

### 3.2.2.3 Ukombozi Dhidi ya Uozo wa Jamii

Uozo wa jamii umekuwa ni donda sugu katika jamii nyingi barani Afrika. Uozo mbalimbali kama vile mauaji, ubakaji, uasherati, uzinzi na uchawi. Haya ni mambo ambayo yanakandamiza wanajamii na kwa hivyo jamii inahitaji kukombolewa dhidi yake. Katika sehemu hii tutaangalia jinsi ambavyo vijana wanajishughulisha kukomboa wanajamii dhidi ya uchawi. Tutaangalia jinsi ambavyo mwandishi wa riwaya teule amesawiri wahusika vijana kuonyesha ukombozi dhidi ya uchawi na ushirikina. Katika riwaya hii tunaaonyeshwa, kuwa kulikuwa na mzee Wapukorengonyi aliyekuwa mchawi hatari sana. Aliwatesa watu wengi na hata kugeuza wengine vizuu. Kutokana na uchawi wake aliwatesa watu wengi na kuleta hasara nyingi kwa wanajamii. Kwa mfano, alitumia uchawi wake akaleta hasara kwa familia ya Baikungi kwa kuwaua ng’ombe wake wa maziwa. Hasara hii ilimfanya huyu mchawi kulipa fidia ya milioni tano. Pia alikuwa na walinzi yaani nyoka ambao walimlinda na kulinda mashamba yake na mali yake. Nyoka hawa wa uchawi walikuwa wanawauma watu na kusababisha kifo.

Getukwa na rafiki yake walinuia kuleta ukombozi dhidi ya uchawi huu uliofanya jamii yao kuwa ya uozo. Getukwa alipopata nguvu baada ya Mzee Msemangikweli kusema kuwa Getukwa ndiye mwana wa miwambo alianza kupigana na walinzi wa mchawi Wapukorengonyi. Tunaelezwa kuwa:

*"Jambo la kwanza kubwa alilofanya lilikuwa kutembelea sehemu zote zilizotoa huduma muhimu kwa watu; visima, chemichemi, mito na vijito, misitu ambamo watu walienda kutafuta kuni na uwanja wa Miwambo ambako watu walienda kulisha mifugo. Uk 174*

Dondoo hili linaonyesha kuwa kijana huyu alifanya kazi kubwa ya kukomboa watu kutoka kwa uchawi kwa kuyaangamiza majoka ambayo yaliwavizia watu. Majoka ya huyu mchawi hayakumtisha tena. Alipoyaelekeza kifimbo yalikauka kana kwamba yalikuwa yamepigwa na radi. Mengine yalitekea moto. Sasa wachawi walimwogopa zaidi ya vile walimwogopa mamake. Hii ilikuwa na mwanzo wa ukombozi dhidi ya uchawi.

Baada ya Getukwa kumalizana na majoka ya uchawi. Aliazimia ukombozi wa kuwasaidia watu waliokuwa wameathirika na uchawi hadi wakawa vizuu. Dondoo lifuatalo linasema:

*"Mawazo ya Getukwa sasa yalilenga hatua nyingine ya ukombozi. Alitaka kuwaachilia wale vizuu. Alitaka watoke utumwani kwa Wapukorengonyi. Warudi kuishi katika jamii kama zamani. Warudi kwa wapendwa wao." Uk 175*

Getukwa aliaaanza mpango wa ukombozi muhimu wa kuweka wale vizuu huru. Haikuwa kazi rahisi kuwatoa vizuu kule shambani mwa mchawi Wapukorengonyi. Lakini wakati wa ukombozi ulikuwa umewadia na alihitaji kuwakomboa. Kulikuwa na maswali sufufu kama vile watawatoa vipi vizuu shimoni, watawaweka wapi, watafanya vipi kurudi katika hali yao ya kawaida na maswali mengine mengi. Baada ya kufikiria kwa kina na kutafuta ushauri jinsi ya kuleta ukombozi wa vizuu alipata majibu murwa kutoka kwa rafiki yake Nkundikelo, Padre, na mama yake. Mwandishi anatuonyesha kuwa mipango yote ilifanywa na hatimaye wale vizuu walikombolewa. Zaidi tunaonyeshwa kuwa vijana maskauti wasichana kwa wavulana walishirikiana kuleta ukombozi. Tunaelezwa kuwa:

*Walijitolea kumsaidia maisha yao yote kuikomboa jumuiya nzima. Hivyo ndivyo jeshi la ukombozi la Getukwa lilivyoendelea kuimarika."* Uk 186

Dondoo hili linaonyesha kuwa watu wa Miwambo walikuwa wameonja utamu wa kukombolewa. Muujiza wa Getukwa kuwakomboa vizuu ilikuwa sawa na kuwafufua wafu. Watu wa Miwambo waliona kuwa hakukuwa na cha kuwarudisha nyuma katika utumwa wa uchawi na umaskini. Ukombozi ulikuwa umeng'oa nanga na kupiga hatua kwa kasi sana. Mwandishi anatuonyesha kuwa vijana wakiwa na ujasiri wataleta ukombozi wa kukomesha uozo katika jamii. Getukwa na Nkundikelo walikuwa ni vijana lakini kwa sababu ya kujitolea walileta ukombozi mkubwa katika jamii yao ya watu wa Miwambo.

### 3.2.3 Dhamira ya Malezi ya Vijana

Malezi ni jambo muhimu kwa watoto na vijana ili kuwaandaa katika maisha ya utu uzima. malezi ni njia ya ukuzaji wa mtoto kwa kutarajia kufuata tabia na mwenendo unaostahiki. Pamoja na hayo malezi huhusisha makuzi, mafundisho, uelekezi na uangalizi anaopewa mtoto. Malezi yakiwa mema na bora huwa yanachangia katika tabia nzuri kwa kijana. Kwa upande mwingine malezi yakiwa mabaya bila shaka kijana atakuwa na tabia mbaya. Wazazi ambao wanawapa watoto wao malezi bora huwa wanajikakamua kuwaonyesha watoto wao njia ifaayo zaidi. Pamoja na hayo wazazi hawa huakikisha kuwa wanawakirimia watoto wao mahitaji ya kila siku kama vile chakula, mavazi, malezi, elimu na matibabu pamoja na mahitaji mengine. Malezi mema aghalabu uhusisha wazazi wote yaani baba na mama. Wazazi wote wanapochukua muda na kuongea na wanao vizuri na kwa uwazi unaojenga uhusiano mwema huwa ni rahisi wawe marafiki na hatimaye kuwalea watoto wao ipasavyo.

Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* mwandishi anaonyesha vijana ambao wamepata malezi mema na hatimaye wakawa wazuri na upande mwingine anaonyesha kijana aliyekaidi

malezi ya wazazi wake na hivyo akaangamia. Getukwa ni kijana aliyepata malezi mazuri na akatii maonyo na maelekezi ya wazazi wake. Getukwa alikuwa kijana wa msaada katika jamii yake kwa sababu alipata malezi mema katika maisha yake. Mwandishi anasawiri mhusika Getukwa kuwa kijana mtiifu, mnyenyekevu, mpole, anayetekeleza majukumu yake na mwenye utu. Wazazi wake yaani Baikungi na mama yake Shahiruzode walitekeleza jukumu lao la kumpa malezi mema na kumkirimia mahitaji yake kama kijana anayebaleghe. Kwa mfano wazazi wake walitetekeleza jukumu la kumpeleka shuleni, kumnunulia mavazi, na alikuwa na malazi mazuri. Mwandishi pia anamwonyesha Getukwa kuwa kijana anayewasidia wazazi wake kwa kutekeleza shughuli na kazi za nyumbani zinazohusu kijana wa rika yake. Pia tunaona babake Getukwa anatekeleza jukumu la kumhimiza asome kwa bidii na hata kumshauri achague vizuri taaluma anayonuia kusomea maishani. Tunaelezwa kuwa:

*"Vizuri," babake alimpongeza, "lakini sasa uwe na tahadhari, mwanangu. Huu ni mwaka wa kukamilisha masomo yako ya Sekondari. Ni kipindi muhumimu sana cha maisha yako. Sina wasiwasi juu ya uwezo wako masomoni. Ni lazima hata hivyo ujitayarishe vizuri. Uk 131*

Dondoo hili linaonyesha wazi kuwa babake Getukwa alikuwa amejali maslahi ya elimu ya mtoto wake. Zaidi katika mazungumzo anamuuliza:

*"Umefikiria kozi ambayo ungependa kusomea baada ya kidato cha nne?" Aliuliza mwishowe. Swali lake lilimtatiza Getukwa. Hakuritarajia. "Kusema kweli sija…nahitaji muda wa kufikiria," alijibu.*

*"Kunazo fomu mtajaza muhula ujao ili kuchagua taaluma. Ni vizuri ufikirie mapema ili wakati ukifika, ujaze ifaavyo," Baikungi alimshauri. "Sawa baba. Nitafikiria halafu nitakupa jibu," Getukwa alisema. Uk 132*

Dondoo hili linaonyesha wazi kuwa baba alikuwa anampa kijana wake malezi mema ili awe mtu wa muhimu maishani. Hii ni changamoto kwa vijana wanaobaleghe wajifunze kukaa na kushaurina na wazazi wao juu ya mambo ya elimu na kozi wanazonuia kuzifanya maishani.

Mfano mwingine wa malezi bora ni ule wa Emira. Licha ya kuwa walikuwa maskini mama yake alihakikisha kuwa amempa malezi bora na msingi mzuri wa kumfanya awe msichana anayewajibika. Tunaelezwa kuwa:

*Emira aliporudi nyumbani, mamake alimpa kazi ya kuchambua maharage. Alipomaliza kazi hiyo, alitoa ombi lake. "Mama, Getukwa amenialika kwa karamu ya nyama ya mbuzi nyumbani kwao. Naweza kwenda?"*

*Mambo ya kufuatana na wavulana mimi siyataki. Unataka kutuletea balaa hapa na huu umaskini wote? mama alimzomea. Uk 60*

Dondoo hili linaonyesha kuwa mama yake Emira alikuwa anajukumika kumpa msichana wake malezi bora. Hata kama alimpa ruhusa alitoa na sharti pia kuwa asichelewe na akafika baada ya saa kumi na mbili. Mama anaonyesha kumtahadharisha msichana wake kuepuka balaa za wavulana kama vile kupata mimba za mapema. Riwaya hii ya vijana inafaa zaidi kwa sababu inashauri jinsi ambavyo wazazi wanapaswa kuwalea watoto wao.

Kwa upande mwingine Ilonkundemi ni mfano wa kijana ambaye hakupata malezi mema wala kutilia maanani malezi ya babake. Vilevile tunaona kuwa baba na mamake Ilonkundemi hawakubaliani katika malezi yao. Babake ana msimamo tofauti wa kumkanya kijana wake abadilishe mienendo ilihali mama yake anamwambia aendelee kusikia ya mjomba wake na kupuuza ya babake. Hali hii ilichangia maisha ya Ilonkundemi yakawa mabaya kwa sababu ya malezi mabaya. Mara nyingi tunaona Ilonkundemi akifuata ushauri wa mjomba wake Wapukorengonyi aliyekuwa mchawi wa kupindukia. Ilonkundemi alionywa na wazazi wake

lakini alitia masikio yake nta kwa sababu mlezi na mkuzi wake alikuwa ni mjomba wake. Kwa mfano usiku ule alioenda kunyunyuzia dawa ili kuua ng'ombe wa Baikungi mamake alimwonya lakini hakusikia. Tunaelezwa kuwa mama alijaribu kumwelekeza mtoto wake kwa njia ipasayo lakini alitia masikio yake nta. Mwandishi anatueleza kuwa usiku huo ndio aliumia vibaya kwa kushambuliwa na fisi katika boma la Baikungi. Ni funzo nzuri kwa wale vijana wanaokaidi malezi ya wazazi wao. Usiku huo Ilonkundemi alikuwa afe kwa sababu ya kufuata malezi mabaya na ushauri potovu wa mjomba wake. Kisa kinapoendelea tunakutana na kija Ilonkundemi amekataa kuwa chini ya malezi ya babake. Hii ilichukulia hatua kali ya Ntoibuguta kukataa kuwa Ilonkundemi si mwanawake tena.

### 3.2.4 Muhtasari

Katika sehemu hii tumeshughulikia dhamira mbalimbali ambazo zinasawiriwa na mwandishi Mwenda Mbatiah, katika riwaya za vijana za *Kimbilio la Silona* na *Majilio ya Mkombozi.* Miongoni mwa dhamira hizo ambazo zinahusiana na vijana wanaobaleghe na zinazoakisi sifa za FYV ni umuhimu na kukatizwa kwa elimu ya vijana, umaskini katika jamii, utamaduni na athari zake katika maisha ya vijana, nafasi ya mwanamke katika jamii, jukumu la vijana katika kuleta ukombozi katika jamii, mapenzi na masuala ya malezi. Dhamira hizi zinaonyesha kuwa na umuhimu mkubwa katika kuelekeza vijana, kufunza, na kuadilisha jamii ya vijana wa kileo. Pamoja na hayo sura hii imetoa maelezo jumla jinsi ambavyo maendeleo ya vijana yanapatikana kwa kurejelea riwaya teule. Kutokana na utafiti wetu tumegundua kwamba dhamira zilizojadiliwa zinachangia mabadiliko na maendeleo ya vijana katika jamii.

# SURA YA NNE

## USAWIRI WA WAHUSIKA: *MAJILIO YA MKOMBOZI* NA *KIMBILIO LA SILONA*

### 4.0 Utangulizi

Katika sura hii tutaangazia usawiri wa wahusika katika riwaya za vijana. Pia tutauweka msingi wa uchunguzi wa usawiri wa wahusika kwa kurejelea wataalamu mbalimbali wanaozungumzia usawiri wa wahusika. Baadhi ya misingi ya uchunguzi wa usawiri wa wahusika na uhusika utakaofanywa kwa kina ni pamoja na: Wahusika na Umri, Wahusika na Mgogoro, Wahusika na Dhamira, Wahusika na Muktadha/Mazingira, Wahusika na Msuko, Wahusika na Lugha, Wahusika na Mtazamo.

### 4.1 Maelezo ya Wataalamu kuhusu wahusika katika Fasihi ya Vijana

Katika fasihi yoyote huwa kuna wahusika ambao mwandishi hutumia ili kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa. Wahusika hawa huwa ni wanadamu, wanyama, vitu fulani, au viumbe vyovyote ambavyo msanii huchagua kutumia ili kuandika juu yao. Hata kama katika kazi zingine za kifasihi ploti na mtiririko wa matukio huongoza kazi hizo, kuna kazi zingine, ambapo usawiri murwa wa wahusika huleta mvuto mkubwa kwa msomaji. Ikiwa kazi ni ya FYV na mwandishi atumie wahusika ambao ni vijana inakuwa rahisi kwa wasomaji kujitambulisha kwa urahisi na wahusika hao na hatimaye wanajihusisha na matukio na visa vilivyo katika kazi hiyo ya fasihi. Wamitila (2002), anazungumzia kuwa waandishi wa kazi ya fasihi huwa wanasawiri wahusika kwa njia mbalimbali kwa kutumia vigezo mbalimbali kama vile: yale mambo ambayo wahusika huyasema, wanayoyafikiria, vitendo wanavyofanya, na ni mambo gani ambayo wahusika wanasema na

kufikiria kuhusu wahusika wengine au wahusika wana uhusiano upi na ufafanuzi wa msimulizi kuhusu mhusika.

Njogu na Chimerah (1999), wanaeleza kuwa ni muhimu kuchunguza namna wahusika wanavyosawiriwa na namna wanavyochangia katika uendelezi wa maudhui na dhamira. Kwa mujibu wao wanasema kwamba kuna wahusika wa aina nyingi kama vile mhusika mkweza ambaye ana sifa za kiutendaji na ni hodari na shujaa. Mhusika wa aina hii huwa anapitia changamoto nyingi lakini habadiliki licha ya mpito wa wakati. Pia kuna mhusika wa kisaikolojia ambaye anakumbana na matatizo chungu nzima ya kijamii na anaibusha hisia za huruma kwa wasomaji. Mhusika wa kimapinduzi ambaye anaelewa historia, siasa, na hali ya kiuchumi ya jamii yake. Aghalabu mhusika huyo ako tayari kutenda mambo yasiyo ya kawaida ili kubadilisha maisha ya wanyonge katika jamii. Pia kuna mhusika jumui ambaye hupatikana katika fasihi ya kidhanaishi na ni mhusika mmoja anayekuwa na sifa za wahusika wengi. Kando na hayo Njogu na Chimerah (khj) wanazidi kusema kuwa katika riwaya wahusika pia huweza kugagwanya katika matapo matatu ambayo, kupitia kwayo, dhamira na maudhui ya mwandishi hujibainisha. Matapo hayo ni wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi. Wahusika wakuu huwa ndio nguzo katika kazi ya fasihi na ndio wanaotawala hadithi nzima. Wahusika hawa ndio wanasukuma kazi ya fasihi mbele, kwa maana migogoro na matukio muhimu huwahusu. Mwandishi wa kazi ya fasihi hutumia wahusika wakuu kuwasilisha dhamira yake. Wahusika wasaidizi wana jukumu la kumsaidia msomaji wa kazi ya fasihi kuwaelewa vyema wahusika wakuu. Wahusika wajenzi hutumiwa na mwandishi ili kukamilisha dhamira na maudhui yake. Pamoja na hayo ni kuwa wanajenga na kukamilisha wahusika wasaidizi na wakuu. Wahusika wajenzi ndio wanawakilisha jamii pana ambayo mwandishi anazungumzia kwa kuonyesha matendo yao.

Fauka ya hayo, wanazidi kusema kuwa katika mijadala ya riwaya kuna matapo mawili makubwa ya wahusika. Matapo hayo ni wahusika wa miraba minne ambao wana sifa nyingi ambapo zimechanganyika zile nzuri na mbaya. Wahusika wa aina hii huwa na maisha mapana na matukio mengi yanayowahusu moja kwa moja. Tapo la pili katika uainishaji huu ni wahusika wa mraba mmoja ambao wana sifa moja tu na mara nyingi huwa hawabadiliki katika riwaya tangu mwanzo hadi mwisho. Ikiwa watabadilika huwa wanabadilika mara moja katika kisa kizima. Wahusika wakuu mara nyingi ndio huwa wa mraba mmoja.

## 4.2 Wahusika katika *Kimbilio la Silona* na *Majilio ya Ukombozi*

### 4.2.1 Wahusika na umri

Umri wa wahusika katika fasihi ya vijana ni msingi muhimu sana katika kuelezea na kuelewa hadithi za vijana. Fasihi ya vijana inajikita katika maisha na uzoefu wa vijana, mara nyingi wakiwa katika umri wa kati ya miaka 12 hadi 21. Wahusika katika fasihi hii wana umri huo au wanakaribia umri huo. Kwa hivyo, wahusika katika fasihi ya vijana wanapaswa kuwa na umri unaowafaa ili kuwafanya wasomaji waweze kuhusiana nao na kuelewa changamoto na matatizo yanayowakabili. Hii inasaidia kujenga uhalisia katika hadithi.

Pia fasihi ya vijana inazingatia safari ya ukuaji na kubadilika kwa wahusika. Wahusika wanaweza kuanza kama watoto na kujifunza na kukua kadiri hadithi inavyoendelea. Umri wa wahusika unaweza kuwa sehemu muhimu ya kuonyesha mabadiliko haya. Vilevile, wahusika katika fasihi ya vijana wanaweza kuwa vyanzo vikubwa vya kuwasilisha mada na masuala yanayowahusu vijana, kama vile urafiki, mapenzi, ubunifu, ujasiri, na changamoto za kujitambua. Umri wa wahusika unaweza kutumiwa kuelezea hizi mada kwa njia inayoeleweka kwa wasomaji wa umri huo.

Mwandishi wa riwaya teule za *Kimbilio la Silona* na *Majilio ya mkombozi* amesawiri wahusika walio kati ya hii miaka. Katika *Kimbilio la Silona* mwandishi amesawiri msichana Silona kuwa mhusika mkuu. Hadithi ikianza Silona ana miaka kumi na saba. Tunaelezwa kuwa:

*"Alikuwa msichana wa miaka kumi na saba. Pamoja na udogo wake, dharuba aliyopigwa na maisha ilimpevusha mapema. Sasa alianza kuyafikiria maisha yake. Vile angejitoa katika shimo alimotumbukizwa. Shogake Sonkisa alimhurumia sana, lakini hakuweza kumsaidia. Mamake mzazi alijitia kutoelewa kilichomtia tumbo maji." Uk 1*

Dondoo hili linaonyesha kuwa Silona alikuwa msichana wa miaka kumi na saba. Hata hivyo alikumbana na changamoto zilizompevusha mapema. Silona pia alikuwa na rafiki yake Sonkisa ambaye ni mhusika mjenzi na alikuwa na umri sawa na Silona. Ni kweli kuwa riwaya hii ya *Kimbilio la Silona* inaakisi hii sifa kuwa wahusika wakuu katika FYV ni vijana wanaobaleghe.

Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* mwandishi amesawiri wahusika wakuu kuwa vijana wanaobaleghe. Vijana hawa wana vipawa vipevu na kila mmoja anajiamini. Nukuu ifuatayo inaonyesha miaka ya hawa vijana:

*"Hakuna vile mtoto wa miaka kumi na saba anaweza kujua mambo kama hayo. Ni lazima yupo mtu mzima anayemtumia akiwa na nia mbaya. Huyo mtu mzima, mi' naona ni mjombake tu. Sio mwingine alisema.*

*"Mimi pia nafikiria hayo, mpenzi, lakini sababu yake nini?" Uk 14*

Dondoo hili linaonysha kuwa Ilonkundemi mpwa wa mchawi Wapukorengonyi alikuwa na umri wa miaka kumi na saba. Mambo ambayo aliyafanya kama vile kuleta mazingaombwe katika uwanja wa Miwambo wakati wa kupiganisha mafahali halikuwa tendo la kijana wa rika yake. Kwa hivyo riwaya hii pia ina wahusika wanaoakisi sifa za kimsingi za FYV.

Tunaambiwa kuwa Getukwa, ambaye ndiye mhusika mkuu wa riwaya, alikuwa kijana mwenye umri wa miaka kumi na mitano wakati huo na baadaye akawa mwana wa Miwambo na mkombozi wa jamii.. Nukuu inaonyesha:

*"Ndoa ni hatua muhimu maishani, Emira. Sisi sio watoto wadogo vile. Mwakani, mie nitakuwa na umri wa miaka kumi na sita. Nitaingia kidato cha nne. Nawe utakuwa na umri wa miaka kumi na minne. Utaingia kidato cha pili," Getukwa alieleza. Uk 65*

Pia tunaelezwa juu ya mhusika Emira ambaye ni kijulanga. Dondoo linaonyesha:

*"Emira alikuwa msichana mweusi mwenye macho makubwa. Alisoma kidato cha kwanza katika shule ya Wasichana ya Agundekocha. Akiwa na umri wa miaka kumi na mitatu, alikuwa mdogo kuliko Getukwa kwa miaka miwili. Walipendana sana. shida yao ilikuwa jinsi ya kuendeleza uhusiano wao bila kuwaudhi wazazi." Uk 59*

### 4.2.2 Wahusika na Mgogoro

Kuufumbua mgogoro katika FYV ni hatua muhimu ambayo huwapa wasomaji fursa ya kufuatilia kwa karibu mabadiliko ya wahusika na kuona jinsi wanavyokabiliana na changamoto na matatizo yaliyowakumba. Hii ni sehemu ya hadithi inayosubiriwa kwa hamu na wasomaji kwa sababu inatoa ufumbuzi wa masuala yaliyokuwa yakiwakabili wahusika, na hivyo kuwapa suluhisho kwa changamoto zao.

Aidha, kuufumbua mgogoro huonyesha ukuaji wa wahusika, jinsi wanavyojifunza kutokana na makosa yao au kubadilika katika mtazamo na tabia zao. Kadhalika, ni katika sehemu hii ya hadithi ambapo mwandishi anaweza kutoa ujumbe wa kina kwa wasomaji. Kupitia njia ambazo wahusika wanatumia kutatua matatizo yao, mwandishi anaweza kuonyesha thamani ya mambo kama vile kujitolea, ushirikiano, na kujiamini. Hii inaweza kuwa fursa ya kutoa mafunzo

au kuhamasisha wasomaji kuhusu maadili au njia za kukabiliana na changamoto katika maisha yao.

Kwa hiyo, kuufumbua mgogoro katika FYV si tu kuhitimisha hadithi, bali pia ni kipengele muhimu kinachowapa wasomaji mwanga juu ya njia za kutatua matatizo, ukuaji wa wahusika, na ujumbe uliotolewa na mwandishi.

Kama tulivyoona hapo juu katika hizi riwaya teule wahusika ni vijana. Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* mhusika mkuu ni Silona. Matukio mengi yanamhusu Silona na pia ndiye mhusika ambaye mwandishi amemsawiri ili kutatua migogoro mikuu. Matukio hayo ndiyo yanasukuma riwaya mbele na ndio maana yeye ndiye mhusika mkuu. Riwaya inapoanza tukio la kwanza ni kuwa Silona anajikuta amekatiziwa masomo yake ghafla na ndoto yake kuzimwa kutokana na kubakwa na mjomba wake na kupata mimba. Mhusika huyu anajaribu kutatua mgogoro huu na tunaona kuwa anapanga kutoroka nyumbani ili aende kwa ndugu yake kuendeleza masomo yake. Silona anafanikiwa kwenda kwa ndugu yake Atweki na hivyo mgogoro huo unatatuliwa.

Pia Silona akiwa kwa ndugu yake mgogoro mwingine unatokea kuhusu masomo yake. Ilikuwa vigumu kuendelea kukaa kidato cha tatu kwa sababu idadi ilikuwa juu ya kiasi kilichohitajika. Wakati ndugu yake alimuuliza kuhusu jambo hilo Silona alitatua ule mgogoro kwa sababu alikubali kuingia kidato cha nne jinsi ambavyo mwalimu alivyoshauri.

Baadaye tunaona mgogoro mwingine mkubwa pale ambapo Silona anatekwa nyara na kurudishwa nyumbani kwa nguvu ili aozwe kwa lazima kwa Ngoteku. Silona anapojipata kwa hali hii aliweza kupanga kubadilisha mazingira ili kutatua mgogoro ule. Kupitia kwa usaidizi wa mamake mdogo Maria akaweza kutoroka kuelekea Misheni ya Gitego. Kitendo cha kutoroka kinatatua mgogoro na hadithi inasonga mbele.

Baada ya kutoroka nyumbani alipita katika eneo la Wachitula. Mgogoro mwingine unatokea kwa sababu ilikuwa ni hatia kwa mtu yeyote kupita katika msitu wa Wachitula. Walinzi walimshika na kumpeleka katika kitala cha mfalme. Silona alipewa adhabu ya kufanya kazi kwa mwezi mmoja. Mgogoro huu unatatuliwa Silona alipotumia ujuzi aliokuwa nao wa ukunga akamsaidia malkia kujifungua salama.

Baadaye Silona anajiunga na misheni ya Gitego huku anapopata masomo. Akiwa huko kasisi Bagondi aliletwa kufanya kazi kama kasisi na daktari. Wote wawili walivutiwa na hisia za mapenzi zikaota katika maisha yao. Huu ulikuwa ni mgogoro mkubwa kwa maana ulihitaji uasi mkubwa. Hata hivyo Silona anaamua kumpenda Bagondi na kwa hilo wanakubaliana kuasi mafunzo ya kanisa na ufisadi wa WASKA yaani Watunza Siri za Kanisa.

Kutokana na mifano hiyo hapo juu ni wazi kuwa riwaya ya *Kimbilio la Silona* inaakisi sifa za FYV kuwa mhusika mkuu ambaye ni kijana migogoro mingi huwa inamhusu na matukio makuu humzunguka. Tunaona kuwa Silona ndiye anakumbwa na migogoro mingi na pamoja na migogoro hiyo kuna njia ambayo anaitatua.

Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* mhusika mkuu ni Getukwa. Matukio mengi huwa yanamhusu mhusika huyu na kujaribu kutatua migogoro. Katika riwaya hii mgogoro mkuu ni kugongana kwa malengo na jinsi ya kufikia malengo hayo. Vijana wawili wanagongana kwa maana kila mmoja wao ana lengo la kuwa mwana wa Miwambo. Riwaya hii inapoanza tukio kubwa linamhusu Getukwa na Ilonkundemi. Suala zima linahusu kupiganisha mafahali. Getukwa alitekeleza wajibu wake ipasavyo kumwandaa fahali wake kwa mashindano hayo. Ilonkundemi analeta mazingaombwe uwanjani Miwambo na kuwashangaza watu wengi. Getukwa ambaye ni mhusika mkuu anajaribu kadri ya uwezo wake ili aone kuwa haki inatendeka na ushindi wa halali

kupatikana. Ni wazi kuwa baadaye kesi iliamuliwa na mhusika huyu Getukwa akapata haki na kuonyesha ujasiri wa kuleta ukombozi.

Baada ya hayo tunamwona mhusika mkuu Getukwa akitafuta haki na kupinga ufisadi katika sekta ya ukulima. Halikuwa jambo rahisi lakini Getukwa na rafiki yake Nkundikelo walijikakamua na kujitolea mhanga kuleta ukombozi. Walitafuta idhibati ya kutosha kama vile kuingia shambani kwa Wapukorengonyi na kuhesabu mibuni, kuenda kiwanda cha kahawa kutafuta uzani wa mbuni, na pia kumtafuta Gavana ili kutoa malalamishi yao. Kwa hivyo hili ni tukio kuu ambalo linamhusu mhusika mkuu amabaye ni kijana.

Tukio lingine kuu ni kuwa Getukwa alilazimika kutunza siri kati yake na rafiki yake Nkundikeleo. Katika harakati za kutafuta ithibati za kupinga ufisadi, Nkundikelo aliumwa na walinzi wa mchawi Wapukorengonyi yaani nyoka. Tunawaona vijana hawa wakitunza siri hadi Nkundikelo akapaona na mpaka mipango yao ya kumaliza ufisadi ikatimia. Kando na hayo tukio lingine kubwa ni lile linalohusu Mwana wa Miwambo. Watu katika kijiji cha Miwambo walitaka sana kujua Mwana wa Miwambo ni nani. Ilonkundemi na mjomba wake walipanga kudanganya kuwa Ilonkundemi ndiye mwana wa Miwambo lakini hayo yote yaligonga mwamba. Getukwa aligonjeka na kusumbuka alipoitwa kuwa mwana wa Miwambo. Baada ya Mzee Msemangikweli kuweka wazi kuwa Getukwa ndiye mwana wa Miwambo, Getukwa alianza shughuli ya ukombozi. Aliangamiza walinzi wa yule mchawi Wapukorengonyi, akaleta uhuru katika mali ya jamii na kuweka vizuu huru na kuwarudisha katika hali yao ya kibinadamu. Kutokana na mifano hii ambayo tumetoa ni wazi kuwa katika FYV riwaya za vijana huwa na mhusika mkuu kijana ambaye matukio mengi yanamzunguka na anajaribu kutatua migogoro.

### 4.2.3 Wahusika na Mtazamo

Wahusika vijana na mtazamo wao ni mambo muhimu katika riwaya za vijana. Mtazamo huu huleta uhalisia na ushirikiano wa kipekee katika hadithi. Wahusika vijana mara nyingi hujikuta katika mazingira yanayowakabili na changamoto za kipekee, na mtazamo wao unawaruhusu wasomaji kuona ulimwengu kama wanavyouona na kuhisi hisia kama zinavyohisi. Hii inafanya riwaya za vijana kuwa chombo cha kuvutia na cha kujifunza kwa wasomaji wa kizazi cha vijana.

Aidha, mtazamo wa wahusika vijana katika riwaya za vijana huwa na nguvu katika kuleta sauti za kizazi cha vijana katika fasihi. Kwa kuwa wahusika hawa ni mara nyingi wasimuliaji wa hadithi, wana uwezo wa kueleza uzoefu wao kwa undani na kuwaonyesha wasomaji changamoto, matumaini, na ndoto zao. Hii inaweza kuwahamasisha vijana wenzao na kutoa sauti kwa masuala muhimu yanayowahusu.

Pamoja na hayo, mtazamo wa vijana katika riwaya za vijana unaweza kuleta mabadiliko katika jamii kwa kuibua majadiliano na kuwahamasisha wasomaji kutafakari juu ya masuala muhimu kama utamaduni, maadili, na mwelekeo wa kizazi kijacho. Kwa njia hii, riwaya za vijana zinaweza kuwa zana ya kuchochea mawazo na kuchangia katika mabadiliko chanya katika jamii. Kwa hiyo, wahusika vijana na mtazamo wao wanaweza kuleta nguvu na uhalisia katika riwaya za vijana na kuzifanya ziwe na athari kubwa kwa wasomaji.

Katika riwaya teule ya *Kimbilio la Silona* , mtazamo wa wahusika unaletwa kwa njia ya kusisimua. Moja kati ya wahusika wakuu katika riwaya hii ni Silona, msichana mdogo wa kijiji cha Ugobo, anayelazimika kuhama kutoka kijijini mwake kutokana na mazingira hatarishi na ya vurugu. Hasa changamoto ya kukatiziwa masomo na ndoa za mapema za lazima. Mtazamo wa Silona unawasilishwa kwa njia ya kwanza yaani nafsi ya kwanza, ambapo msomaji anapata ufahamu wa ndani wa hisia, mawazo, na uzoefu wa moja kwa moja wa Silona. Kupitia mtazamo

wake, msomaji anaweza kuhisi kile anachohisi, kujua kinachomtia wasiwasi, na kuelewa changamoto zinazomkabili katika safari yake ya kutafuta kimbilio.

Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona*, tunaweza kutumia mfano wa Silona mwenyewe ili kuonyesha mtazamo wake wa kipekee. Katika sehemu moja ya riwaya, Silona anasimulia jinsi alivyoanza kuona ulimwengu tofauti baada ya kuhama kutoka kijijini mwake na kuelekea kwa kaka yake. Anasema: Alipoondoka kijijini na kuanza safari yake ya kuelekea kwa ndugu yake na baadaye misheni ya Gitego, ulimwengu uliokuwa ukimtazama ulionekana kubadilika kabisa. Mtazamo wake wa ulimwengu ulibadilika na kuanza kuwa wa kutatanisha, lakini bado alikuwa na matumaini ya kupata kimbilio.

Katika mfano huu, mtazamo wa Silona unaonyesha jinsi anavyohisi na anavyoona mazingira mapya ya misheni ya Gitego baada ya kuondoka kijijini. Kupitia maneno yake, tunaweza kugundua mchanganyiko wa hisia zake za wasiwasi na matumaini, na jinsi anavyobadilisha mtazamo wake wa ulimwengu. Hii inaonyesha jinsi mtazamo wa wahusika unaweza kuathiri uzoefu wa kusoma na jinsi riwaya inavyoweza kuonyesha ulimwengu kupitia macho ya wahusika wake.

Sifa nyingine ya wahusika katika FYV ni kuwa wazazi mara nyingi hawahusiki na ikiwa wanahusika huwa wanakinzana na vijana. Moja ya kinzani kubwa katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* ni tofauti za kizazi na tamaduni kati ya wazazi na vijana. Wazazi wengi katika riwaya wanawakilisha kizazi kilichopita, ambacho kinazingatia utamaduni wa zamani na maadili ya jadi.

Vijana, kama Silona na marafiki zake, wanawakilisha kizazi kipya kilichosheheni mawazo mapya na mitazamo ya kisasa. Wanavutiwa na mabadiliko na kufanya jitihada za kuleta mabadiliko katika jamii yao. Hili ni wazi katika riwaya teule ya *Kimbilio la Silona*. Wazazi katika riwaya hii wamehusika na kuwa baadhi ya wahusika katika riwaya hii. Wazazi wa mhusika mkuu

Silona wanaonyeshwa wakiwa na mtazamo kinzani na ule wa kijana wao Silona. Ukinzani unatokea kati ya ndoto za Silona za kuchagua mwenzi wake wa maisha kwa mapenzi yake na shinikizo la wazazi wake na jamii inayotaka kufanya maamuzi kwa niaba yake. Kwanza mfano mzuri ni mtazamo tofauti kuhusu ndoa za mapema na za lazima. Kwa mujibu wa kijana Silona ana mtazamo kuwa asome amalize masomo yake ili aafikie ndoto yake maishani. Hata baada ya Kubakwa na mjomba wake akapata mimba, silona alikuwa tayari kurudi shuleni ili aendelee na masomo yake. Silona alijaribu kadri ya uwezo wake akatorokea kwa kaka yake Atweki ili aendelee na masomo. Licha ya bidii zake zote mwandishi anatuonyesha kuwa mtazamo wa wazazi ulikuwa ni tofauti kabisa. Mtazamo wao ulikuwa Silona apate mume wa kumwoa. Tunaelezwa kuwa:

*"Alikuwa msichana wa miaka kumi na saba. Pamoja na udogo wake, dharuba aliyopigwa na maisha ilimpevusha mapema. Sasa alianza kuyafikiria maisha yake. Vile angejitoa katika shimo alimotumbukizwa. Shogake Sonkisa alimuhurumia sana, lakini hakuweza kumsaidia. Mamake mzazi alijitia kutoelea kilichomtia kitumbo maji. "utaolewa na mume atakayekutunza. Babako atatengeneza kila kitu," alimhakikishia." Uk 1*

Dondoo hili linaonyesha wazi kuwa mtazamo wa wazazi ulikuwa kinyume kabisa na ule wa kijana silona. Agahalabu, wazazi huwa na mtazamo tofauti na vijana. Baadaye baba yake Silona alikubali mahari kutoka kwa Mzee Ngoteku ili aweze kumwoza binti yake. Ndani ya riwaya, suala la ndoa pia linahusiana na masuala ya kifedha na kijamii. Wazazi wanaweza kuona ndoa kama fursa ya kuimarisha uhusiano wa kifamilia au kuongeza utajiri wa familia. Vijana kama Silona wanaweza kuwa na mtazamo tofauti, wakitafuta ndoa inayojengwa juu ya upendo na hisia, badala ya masuala ya kifedha au kijamii. Pamoja na hayo ni kuwa wazazi wa Silona hasa baba yake wanakinzana naye kwa mambo mengi hasa yale ya Mila na tamaduni. Vijana katika riwaya teule hawakubaliani na ubaguzi wa kijinsia. Wao wanaamini katika usawa wa kijinsia na

wanakataa kutumika kwa wanawake kama chombo cha kuzaa au kutumikishwa kwa faida ya wanaume. Silona anapinga kabisa mila za Ugobo zilizopitwa na wakati kama zile za kumdhalilisha mwanamke na kumwona kama chombo cha kumtumikia mume. Tunaelezwa kuwa:

*"Masaibu ya mwaka jana yaliondoa mwanga wa matumaini maishani mwa Silona. Sasa maisha yake yaligubikwa na giza. Bado uchungu ulikuwa haujamtoka. Bado alikuwa amechanganyikiwa. Lakini pia alipata mafunzo kadha. Funzo mojawapo lilikuwa kwamba Ugobo ilikuwa ngome ya mwanaume. Wanawake walikuwa watumwa ngomeni. Walikuwa vinyago vya kuwafurahisha wenye ngome. Kama mwanamke angekuwa na sauti mkosi uliomwangukia haungetoka. Hata baada ya kutokea ungetafutiwa dawa. Lakini hakuna aliyeshughulika. Aliachwa aubebe mzigo wa shida zake peke yake. Jamaa wote walimvalia miwani. Uk 1*

### 4.2.4 Wahusika na Dhamira

Jambo lingine la wazi kuhusu wahusika katika FYV ni kuwa wanatenda na kuendeleza dhamira zinazowahusu vijana. Masuala ya vijana wanaobaleghe ni pamoja na mapenzi, elimu, ndoa za mapema, mimba za mapema, matumizi ya dawa za kulevya, kuenda kinyume na mila zilizopitwa na muda katika jamii, matumizi ya mtandao, kujaribu kuleta mabadiliko katika jamii na masuala mengine.

Mwandishi wa riwaya teule za vijana amesawiri wahusika kwa njia inayoakisi sifa hii ya FYV. Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* tunawaona wahusika vijana hasa wanahusika na masuala yanayowahusu vijana. Kwa mfano mhusika mkuu Silona amesawiriwa na mwandishi kuonyesha umuhimu wa elimu ya msichana. Silona anang'ang'ana kadri ya uwezo wake licha ya kuwa anapitia changamoto nyingi hadi hatimaye anafanikiwa. Baada ya kukatiziwa masomo yake baada ya kubakwa na kutiwa mimba na mjomba wake bado alisoma akamaliza shule ya upili, na akajiunga na shule ya misheni ya Gitego aliposomea ualimu na mafunzo ya utawa. Mhusika

Sonkisa rafiki yake Silona pia ni msichana anayesawiriwa ili kuonyesha suala la elimu ya wasichana wanao baleghe. Pia kuna vijana wengi wanaosoma pamoja na Silona katika shule ya msingi, shule ya upili na katika Misheni ya Gitego.

Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* mhusika Getukwa, Ilonkundemi ni wanafunzi. Getukwa anaonyeshwa kuwa na bidii masomoni kinyume na mwenzake Ilonkundemi. Hadithi inapoendelea Getukwa anaonyeshwa kujipanga kufanya mtihani wa kitaifa. Hili linaonyesha wazi kuwa elimu ni mojawapo ya maswala yanayowahusu vijana.

Wahusika katika FYV husawiriwa kuonyesha suala la mapenzi. Vijulanga maranyingi huathirika na mapenzi wakiwa shuleni na hata baada ya kumaliza masomo yao ya shule ya upili. Kwa mfano Silona anaingia katika mapenzi hasa baada ya kukutana na Kasisi Bagondi.

*"Sista Silona. Nakuomba uamini maneno nikuambiayo. Kukutana na kuzungumza nawe huwa kila mara kunaniletea furaha ambayo haina kifani. Mimi ni mtawa kama wewe. Hivyo mahusiano kati ya jinsia tofauti ni bahari kubwa kwangu. Sina mbinu za mapenzi na utongozaji. Wala hayana nafasi katika maisha tuliyochagua kuishi. Lakini lazima nikiri kwamba kukuwaza, kuwa nawe, kuongea nawe kunaleta ujoto fulani mtamu moyoni mwangu. Kwa miaka ishirini na sita niliyoishi ulimwenguni, nilikuwa sijawahi kupata hisia kama hii. Mpaka nikakutana na kuongea nawe wakati ule wa mahafali. Hisia hii inaendelea kuwa kila kuchao. Sina uwezo wa kudhibiti. Sijui itanipeleka wapi. Na sijui kama ni ya upande wangu tu"*

*Silona alitulia tuli huku akiwa ameinamisha kichwa. Aliwaza kwamba maneno ya Bagondi yalieleza hali yake mwenyewe. Lakini hakuwa na ulumbi wala ujasiri kama wake. Alimwona kama aliyempiku kwa mambo mengi. Umri, elimu, upevu wa akili na ujasiri wa kuyatoa mambo yaliyo mvunguni mwa moyo…." Uk 125*

Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* Emira na Getukwa wanakuwa katika uhusiano wa kimapenzi. Vilevile rafiki yake Getukwa anajihusisisha katika mapenzi. Katika riwaya hii dhamira ya mapenzi imejadiliwa kwa kina.

Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* wahusika vijana wamesawiriwa kuonyesha kuwa katika FYV masuala yanayozungumziwa kwa mapana ni yale yanayowahusu vijana wanaobaleghe. Kwa mfano, mhusika Getukwa ameonyesha masuala ya matumizi ya teknolojia. Tunaelezwa kuwa Getukwa ana rafiki pepe. Hii inaonyesha uwezo wake wa kutumia teknolojia kama kijana. Tunaelezwa kuwa kompyuta aliyokuwa akiitumia alitumiwa na rafiki yake Ptomivalunsky. Vijana wa siku hizi wana uwezo wa kutumia teknolijia. Wengi wao wako katika mitandao ya kijamii kama vile Twitter, Whatsapp, Facebook, Tiktok, Imo, Instagram, Snapchat na mitandao mingine mingi ya kijamii.

### 4.2.5 Wahusika na Lugha

Lugha katika riwaya za vijana ni jambo muhimu sana, kwani inaweza kuathiri jinsi wasomaji wanavyojihusisha na wahusika na hadithi kwa ujumla. Pia lugha huwa msingi wa kuwasawiri na kuwabainisha wahusika wenyewe na kuwa kigezo muhimu cha utambulisho wao. Wahusika katika riwaya za vijana wanapaswa kuwa wa kuvutia na wa kuvutia kwa wasomaji wa kizazi hicho, na lugha inaweza kuchangia sana katika kufikia lengo hili. Hapa kuna mambo muhimu ya kuzingatia katika kueleza wahusika vijana na lugha katika riwaya za vijana na kazi ya fasihi ya vijana kwa jumla.

Kwanza kabisa ni jinsi wahusika wanavyoongea. Mara nyingi wahusika vijana wanapaswa kuongea kwa njia inayolingana na umri wao na utamaduni wao. Lugha wanayotumia inapaswa kuwa ya kisasa na kufuata mtindo wa mawasiliano wa kizazi chao. Hii inaweza kujumuisha matumizi ya maneno mapya, slang, au lugha ya mitandaoni. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kimbilio*

*la Silona* wahusika wanatumia lugha ya umri wa vijana. Kwa kutaja ni kuwa Lugha ya Silona ni ya kijana aliyesoma vizuri. Pia anachanganya na kuhamisha ndimi kama vile; iwe top secret, very good, kufinya swichi, spishi. Kutumia lugha ya mtandaoni kama vile; tarakilishi ilikuwa imeunganishwa na mtandao wa intanenti. Katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* hilo pia limetokea. Kwa mfano, kutumia utohozi kama vile kaunta, pedali ya baiskeli.

Lugha pia hutumiwa kuonyesha utamaduni wa wahusika vijana. Hii inaweza kujumuisha matumizi ya maneno au lugha maalum ya kikanda au kitamaduni. Kuelewa utamaduni wa vijana na jinsi wanavyoongea ni muhimu kwa waandishi wa riwaya za vijana. Kwa mfano katika *Kimbilio la Silona* inaonyesha utamaduni wa Ugobo. Vilevile katika riwaya ya *Majilio ya Mkombozi* inaonyesha utamaduni wa Miwambo kama vile vijana kupiganisha mafahali katika uwanja wa Miwambo.

Lugha pia inaweza kutumiwa kuonyesha hisia na uzoefu wa wahusika vijana. Kwa mfano, unaweza kutumia lugha ili kuonyesha furaha, huzuni, upendo, au hofu wanayohisi. Lugha inapaswa kuwa njia ya kuwafanya wasomaji waweze kuhusika kihisia na wahusika. Mwandishi wa riwaya teule amezingatia hoja hii. Kwa mfano katika Kimbilio la Silona lugha ambayo imetumika inaonyosha huzuni aliyo nayo Silona. Katika Uk 5 “sikatai ni mzazi wangu. Lakini nataka kutoka mikononi mwake,” Silona alijibu kwa sauti iliyosheheni hisia. Katika majilio ya Mkombozi sura ya kwanza Getukwa amejawa na hisia kutokana na yale yanatendeka katika uwanja wa Miwambo. Mfano ndume wake alipoumia kutokana na mazingaombwe ya Ilonkundemi anasema: “Pole Mbogo wangu. Mama atakutibu.

Riwaya za vijana zinaweza kutumia lugha kwa njia ya ubunifu, kama vile mashairi, nyimbo au maneno ya kisanii, na hadithi ndani ya hadithi ili kuchangia katika uzoefu wa kusoma. Hii inaweza kuongeza kiwango cha kuvutia cha riwaya na kufanya kusoma kuwa uzoefu wa kipekee.

Riwaya teule zimetumia mbinu hii ipasavyo. Katika *Kimbilio la Silona* mwandishi ametumia nyimbo na mashairi. Mfano katika Uk 26-28 kuna hadithi ndani ya hadithi. Hii ni hadithi ambayo imeandikwa katika gazeti ambalo Silona alikuwa anasoma akiwa kwa ndugu yake Atweki. Pia katika riwaya hiyo Uk 2 mwandishi ametumia mbinu ya barua. Hii ni barua ambayo Silona anamwandikia ndugu yake Atweki.

Kwa kuwa riwaya za vijana zinalenga kundi maalum la umri kati ya miaka 12 hadi 21, lugha inapaswa kuwa inayoeleweka na kuvutia kwa wasomaji wa kizazi hicho. Inapaswa kuwa na usawa mzuri kati ya kuwa ya kisasa na kusisimua bila kuwa ngumu sana kueleweka. Ni wazi kuwa riwaya teule zimetumia sentesi sahili na msamiati unaoeleweka kwa urahisi. Pia ni lugha ya kuvutia hasa kimapenzi, kielimu na kiteknolojia.

Kwa kumalizia, lugha katika riwaya za vijana ni chombo muhimu cha kuwasiliana na wasomaji wa kizazi hicho na kuwafanya wajisikie wanahusika na wahusika na hadithi. Inapaswa kuwa ya kuvutia, ya kisasa, na kuonyesha utamaduni na uzoefu wa vijana.

### 4.2.6 Mazingira na Wahusika

Mazingira na wahusika ni vipengele muhimu katika riwaya za FYV. Riwaya hizi aghalabu hujikita katika maisha ya vijana na jinsi wanavyokabiliana na changamoto za kujitambua, kujielewa, na kujumuishwa katika jamii. Mazingira, kwa upande mwingine, yanaweza kuwa yale ya kijamii, kitamaduni, au kijiografia ambayo huathiri maisha na uzoefu wa wahusika vijana. Kwa hivyo, katika sehemu hii, tutajadili jinsi wahusika vijana wanavyounganishwa na mazingira katika riwaya za FYV

Wahusika vijana mara aghalabu hujikuta katika safari ya kujitambua na kujielewa. Mazingira yao yanaweza kuwa changamoto katika kujenga utambulisho wao wa kibinafsi. Kwa mfano, katika riwaya teule ya *Kimbilio la Silona*, mhusika Silona anajaribu kuelewa jinsi

anavyostahili katika jamii na jinsi anavyojisikia kuhusu mazingira yake. Tunaona haridhiki na mazingira anayolelewa hasa utamaduni wa Ugobo. Silona anaona mazingira yake yana mdhalilisha mwana wa kike na kumpa mwanaume nguvu kupita kiasi. Pia mazingira ya Silona hayampi ruhusa ya kupata masomo. Hili ni sawia na wasichana ambao wamezaliwa huko Ugobo.

Mazingira ya kijamii na marafiki wa wahusika vijana ni sehemu muhimu ya riwaya za FYV. Wahusika wengi hukutana na marafiki wanaowasaidia kukua na kujifunza maisha. Mazingira haya ya kijamii yanaweza kuathiri tabia na maamuzi ya wahusika. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* na wahusika wa Silona, Sonkisa na Bagondi, urafiki wao na uhusiano wao unaweza kuchangia katika kuelewa mafundisho ya haki za wanawake na kupinga mila zilizopitwa na wakati. Hasa pale ambapo Silona na Bagondi wanapoasi dini na kufunga ndoa. Katika riwaya ya Majilio ya Mkombozi Getukwa anakutana na rafiki pepe ambaye anamsaidia kufahamu mambo mengi ya mtandao. Vilevile Getukwa ana rafiki wake Nkundikelo anayemsaidia kuwa na ujasiri na mwisho wake anatimiza mpango wake wa ukombozi.

Wahusika vijana wanaweza pia kuathiriwa na mazingira ya kijiografia wanamoishi. Muktadha wa kijiografia unaweza kuwafanya wahusika wakutane na changamoto na fursa tofauti. Kwa mfano, katika riwaya teule ya *Kimbilio la Silona*, Silona, na wasichana wengine mazingira yao ya Ugobo na mvutano kati ya vikundi tofauti vya wazazi na vijana ni sehemu muhimu ya hadithi. Kwa mfano wazazi wa Kiume wa Ugobo wanawawaoza wasichana wao wakiwa wadogo.

Riwaya za fasihi ya vijana mara nyingine hujadili jinsi mazingira ya kitamaduni yanavyoathiri wahusika. Mazingira ya kitamaduni yanaweza kujumuisha tamaduni za familia, dini, na maadili ya kijamii. Kwa mfano, katika *Kimbilio la Silona*, mhusika anajikuta akigongana na tamaduni mbili tofauti za Wkristo alivyopata habari kutoka kwa Swafiru na Ugobo

wanazoshikilia wazazi wao. Pia katika *Majilio ya Mkombozi* Getukwa anapata changamoto wakati wa kupiganisha mafahali kwa maana yeye si mzaliwa asili wa Miwambo.

Riwaya za fasihi ya vijana pia zinaweza kuonyesha jinsi mazingira yanavyobadilika na jinsi mabadiliko haya yanavyoathiri wahusika. Kwa mfano, riwaya kama *Kimbilio la Silona* inaonyesha jinsi mazingira ya Ugobo yanavyobadilika na kuwa hatari kwa wahusika vijana kama Silona Sonkisa na wasichana wengine.

Katika baadhi ya riwaya, mazingira yanaweza kuwa kikwazo au changamoto kwa wahusika. Mifano ni pamoja na mazingira yenye umaskini, ukosefu wa elimu, na unyanyasaji wa kijinsia au kibaguzi. Wahusika wanaweza kuwa na jukumu la kubadilisha mazingira haya au kujitetea. Kwa mfano, katika *Kimbilio la Silona*, mazingira yake ya familia yenye shida na unyanyasaji wa kijinsia yanamfanya ajitafutie njia ya kujiletea furaha na kujiamini. Hapo ndipo Silona anaamua kukimbia kuenda kwa ndugu yake Atweki. Hali inapozidi na anaridishwa nyumbani anaenda katika misheni ya Gitego.

## 4.3 Hitimisho

Kwa kumalizia, riwaya za fasihi ya vijana zinachora taswira za kuvutia za wahusika vijana wanaopitia mabadiliko na kukua katika mazingira tofauti. Uhusiano wao na mazingira, umri wao, dhamira zao, na mtazamo wao huchangia kuunda hadithi za kusisimua na zenye ujumbe wa kina. Kupitia riwaya hizi teule za *Kimbilio la Silona* na *Majilio ya Mkombozi*, wasomaji wanaweza kujifunza kuhusu maisha ya vijana na kugundua changamoto na fursa wanazokabiliana nazo katika ulimwengu wao wa kipekee.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia muhtasari wa utafiti tulioufanya na matokeo ya utafiti ambayo yanatokana na data tuliyoikusanya maktabani na mtandaoni. Vilevile, inaangazia mchango wa utafiti huu, changamoto za utafiti huu, na mapendekezo kutokana na utafiti tuliofanya. Matokeo yote ya utafiti huu yamewasilishwa na kutolewa kwa kuzingatia malengo, maswali ya utafiti na mihimili ya nadharia. Nadharia ya Tanzu imetumika kuonyesha jinsi ambavyo FYV ni utanzu unaoshughulikia masuala ya vijana na ni tawi la fasihi ambalo linalenga vijana wanaobaleghe. Pamoja na hayo mihimili ya nadhari hii ya Tanzu imetumika kuonyesha sifa za FYV na kutokana na hayo tukatoa mifano kwa kurejelea riwaya teule za *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona.*

### 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafitu huu uliangazia dhamira na wahusika katika FYV kwa kurejelea riwaya teule za *Majilio ya Mkombozi* (2016) na *Kimbilio la Silona* (2021). Utafiti huu uliongozwa na malengo matatu yafuatayo. Kwanza, tuliangalia dhamira zinazowahusu vijana kama vile elimu, mapenzi, ndoa za mapema, matumizi ya teknolojia na ukombozi wa vijana katika FYV kama sifa ya kimsingi inayohitaji kushirikishwa katika ufafanuzi wa fasihi ya vijana katika fasihi ya Kiswahili. Pili, kuonyesha usawiri na aina za wahusika katika fasihi ya vijana kwa kuzingatia vipengele kama vile umri wa wahusika, changamoto za jamii, mtazamo wa wahusika, na mandhari kwa kurejelea riwaya teule za *Kimbilio la Silona* na *Majilio ya Mkombozi*. Tatu, kuonyesha jinsi dhamira na wahusika zinavyoakisi sifa za kimsingi za FYV.

Katika sura ya kwanza, masuala ya kimsingi ya pendekezo la utafiti yameshughulikiwa. Katika sura hii ya kwanza tuliangazia usuli wa utafiti ambao ulitusaidia kuweka msingi wa utafiti huu kwa kuonyesha nafasi ya FYV katika jamii. Sura hii ya kwanza vilevile ilieleza suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada na nadharia iliyoongoza utafiti huu. Yaliyoandikwa kuhusu mada yalijadiliwa kwa kina ili kubainisha mchango wa kazi ambazo zimetajwa na kurejelewa katika utafiti huu. Nadharia iliyotumika katika utafiti huu ni ile ya Tanzu. Pamoja na hayo sura hii ya kwanza imejadili mbinu za utafiti ambazo zilitumika. Utafiti huu ulikuwa ni utafiti wa maktabani na mtandaoni kwa kusoma na kurejelea maandishi ya awali. Sampuli lengwa, ukusanyaji wa data na uwasilishaji wa data pia ulijadiliwa. Riwaya teule ziliteuliwa kwa kutumia mbinu-kusudio kwa sababu lengo letu lilikuwa kuchunguza FYV kwa kurejelea riwaya za Kiswahili. Riwaya ziliteuliwa kwa misingi mikuu kwamba wahusika ni vijana wanaobaleghe kati ya umri wa miaka 11 hadi 21. Mambo ya kimsingi yaliyojadiliwa ni dhamira zinazowahusu vijana na usawiri wa vijana katika FYV kwa kuzingatia sifa za FYV. Masuala yote yamewasilishwa na kuchanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti huu. Kwa mfano, lengo la kwanza lilitusaidia kubainisha dhamira zinazowahusu vijana na jinsi ambavyo zinajitokeza katika FYV. Lengo la pili lilitusaidia kuchunguza usawiri wa wahusika vijana katika riwaya za FYV. Mwishoe, lengo la tatu lilitusaidia kuonyesha jinsi ambavyo dhamira na wahusika katika riwaya teule zinaakisi sifa za FYV.

Sura ya pili imeangazia mihutasari ya riwaya teule zinazowahusu vijana wanaobaleghe kwa kurejelea riwaya za *Majilio ya Mkombozi* na *Kimbilio la Silona*. Dhamira zinazohusu masuala ya vijana zimejadiliwa kwa kina katika sura ya tatu. Vijana wanaobaleghe wa kike na wa kiume wamesawiriwa kuendeleza dhamira zinazowalenga vijana. Dhamira ambazo zimejadiliwa ni pamoja na mapenzi, elimu ya wasichana, ndoa za mapema na za kulazimishwa, unafiki wa dini,

nafasi ya vijana katika kuleta ukombozi katika jamii zao, vijana kupigana na ufisadi, vijana kupinga mila na desturi za jamii ambazo zimepitwa na wakati na dhamira zingine. Mihimili ya nadharia ya nadharia ya tanzu ilitumika kubainisha dhamira hizi zinazowahusu vijana.

Katika sura ya nne utafiti huu umeshughulikia usawiri wa wahusika katika FYV. Wahusika wamesawiriwa kwa kuzingatia sifa za utanzu wa FYV. Kwa mfano, mhusika mkuu ni kijana anayebaleghe kati ya umri wa miaka 11 hadi 21. Pili wahusika hawa huwa na mtazamo kinyume na wazazi wao ikiwa wametajwa katika riwaya. Vilevile wahusika wakuu huendeleza maswala yanayowahusu vijana wanaobaleghe kama vile mapenzi, elimu, ndoa za mapema na mengine. Wahusika husawiriwa ili wawe kielelezo kwa vijana wanaosoma FYV. Sura hii pia imeonyesha jinsi ambavyo riwaya teule zinaakisi sifa za FYV kwa kutumia kigezo cha usawiri wa wahusika.

Sura ya tano ambayo ni ya mwisho imeshughulikia muhutasrai wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo ya utafiti na changamoto za utafiti huu.

### 5.2 Matokeo ya utafiti

Riwaya bunilizi za vijana zina mchango mkubwa katika fasihi na pia katika jamii kwa jumla. Riwaya hizi za vijana zinatekeleza majukumu kama vile kuburudisha, kuelimisha, kufunza maadili, kuonya, kukemea, kuzindua wazazi, vijana na jamii kwa jumla kuhusu masuala yanayowahusu vijana. Pia wahusika vijana wanadhihirisha dhamira zinazowahusu vijana katika jamii. Dhamira hizi huwaathiri vijana kwa njia chanya au hasi. Dhamira chanya ni zile ambazo zinakuza maadili na kuwatia vijana motisha wa kuendelea katika maisha. Dhamira hizi hukuzwa na mwandishi wa kazi ya fasihi akiwa na lengo la kuwakuza vijana kwa njia inayostahili. Kwa mfano katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* mhusika mkuu amedhihirisha dhamira chanya ambazo vijana wengine wanafaa kuiga ili kuleta mabadiliko katika jamii. Silona alisimama kidete kama msichana na kupigania elimu yake licha ya kuwa ilikuwa na changamoto si haba. Silona

alijikakamua akasoma hadi akatorokea misheni ya Gitego alikosomea ualimu na kuwa mtawa wa kanisa. Kando na hayo Silona amesawiriwa na kupigana na ndoa za mapema na za lazima. Silona pia ni kielelezo cha vijana wengine kwa sababu alipinga ufisadi na unafiki wa dini, aliamua kuasi kanisa na chama cha watunza siri kanisani na akaanza kutetea haki za watu kwa kweli. Nafasi ya mwanamke katika jamii ilibadilika kwa sababu Silona alileta mtazamo kuwa mwanamke si chombo wala kinyago cha kumfurahisha mume. Silona alibakwa na mjomba wake na akapata mimba lakini hata kwa changamoto hizo bado kijana huyu aliweza kupiga hatua mbele kwa kujikubali na kuendelea na maisha. Kwa mjibu wa nadharia ya tanzu ni kuwa utanzu wowote uakisi sifa zake ipasavyo. Kwa kurejelea riwaya teule zimeakisi sifa za FYV.

Imebainika kuwa vijana wasichana wanaobaleghe huwa wanaathirika sana hasa wanapobaguligwa na kulazimishwa katika mila na tamaduni zilizopitwa na wakati. Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* kuna wengi ambao waliozwa mapema na kwa lazima kwa wazee waliokuwa na pesa. Hali hii iliwaathiri wasichana wengi kwa sababu lilikuwa ni tendo la kulazimishwa. Wasichana hao ndoto zao zilizimwa kwa sababu ya umasikini na wazazi wao kuwa na pupa ya mali. Wazazi wa ugobo pia walikuwa na imani kuwa mtoto wa kike kazi yake ilikuwa kama maua ya nyuki yaani kuvutia tu bila kuwa na umuhimu kama vile nyuki yaani kijana wa kiume. Hivyo wasichana wengi walilazimishwa kuolewa mapema na hawakuelimishwa ili kupata elimu ya juu kama ilivyokuwa kwa wavulana. Pamoja na hayo Rebeka ni mfano wa wasichana wanaokandamizwa na kunyimwa haki ya urithi. Baada ya Rebeka kufukuzwa na mume wake kwa sababu ya kuwa tasa alirudi kwao. Wazazi wake walipokufa Rebeka alipigwa vibaya na mjimba wake kwa sababu ya kutaka kuchukua shamba yote. Ni kisa ambacho kilikuwa kibaya zaidi kwa sababu Rebeka aliumizwa vibaya sana. Hivyo basi ni dhahiri kuwa FYV inashughugulikia masuala ambayo yatawazindua wazazi na vijana ili kujua haki zao na kufanya mambo yote kwa njia halali.

Pia imedhihirika kuwa wazazi huwa wanawalazimisha watoto wao hasa vijulanga ili kurithi kazi wanazozifanya. Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* tunaona kijana Bagondi analazimishwa na baba yake ili aache kuendelea na masomo yake ili amritishe uganga. Hili ndilo jambo lililopelekea Bagondi kutoroka nyumbani na kisha baba yake akajitia kitanzi. Kando na Bagondi ni kuwa mamake Silona alikuwa anataka kumritisha kazi ya ukunga. Silona alikuwa na maoni tofauti na yale ya mamake. Licha ya kuwa Silona alijifunza ukunga alikuwa na maoni ya kuendeleza masomo yake ili atimize ndoto zake. Vilevile Mzee Machengo alikuwa na nia ya kumritisha kijana wake Atweki kazi ya ukulima. Atweki alikataa na akaenda kufanya biashara ambayo ilimfanya akafanikiwa zaidi. Kwa hivyo hili ni funzo murwa kwa wazazi na vijana wao kuwa si vyema kuwalazimisha watoto kufanya kozi au kazi ambazo hawazipendi, bali vijana wapewe nafasi na uhuru wa kuchagua kozi wazipendazo kwa usaidizi na uongozi wa wazazi wao.

Katika riwaya ya *Majilo ya Mkombozi* mwandishi ameonyesha kuwa vijana wanatekeleza jukumu kubwa la kuleta ukombozi katika jamii. Getukwa ambaye ni mhusika mkuu pamoja na rafiki yake Nkundikelo wanajitolea mhanga katika harakati za kukomboa jamii yao. Getukwa anapigana na ufisadi ulioka katika ukulima wa mbuni. Halikuwa jambo rahisi lakini kijana huyu pamoja na rafiki yake walijikakamua wakaweka maisha yao hatarini na kuhakikisha kuwa ufisadi huo umeisha. Hatimaye Gavana aliwapiga kalamu wafisadi na ukulima wa mbuni ukaendelea vizuri. Pamoja na hayo ni kuwa Getukwa aliwakomboa watu kutoka kwa janga kubwa la mchawi mkuu Wapukorengonyi. Imani ya Nguvumapembe ilikuwa imewatesa watu na kuwasukuma katika lindi la umaskini. Getukwa alipokuwa Mwana wa Miwambo alifukuza walinzi wa Wapukorengonyi na kuondolea watu wa Miwambo kodi ya lazima. Mabadiliko haya yalibadilisha maisha ya watu wa Miwambo kwa sababu walipata uwezo wa kuenda katika visima kuteka maji, misitu kutafuta kuni, na viwanjani kulisha mifugo wao. Getukwa pia alileta ukombozi kwa

kuwasaidia watu ambao walikuwa wamegeuzwa vizuu na Wapukorengonyi. Getukwa na rafiki yake wakishirikiana na masikauti waliwaokoa vizuu na wakarudi hali yao ya kawaida. Tendo hili lilikuwa kama kuwa na nguvu ya kufufua watu.

Pia imebainika kuwa katika riwaya ya vijana ya *Majilio ya Mkombozi* dhamira ya mapenzi inajitokeza na kukuzwa na mwandishi. Kwa mfano, Emira msichana wa umri wa miaka kumi na tatu anapendwa na Getukwa. Tunaambiwa kuwa Getukwa alimpenda Emira hadi akaota kuhusu harusi yao. Ni hali ambayo inawakumba vijana wanaobaleghe katika hali ya sasa. Kando na kupendwa na Getukwa pia tunaonyeshwa kuwa Ilonkundemi pia alimpenda Emira na kumwandikia barua za mapenzi lakini Emira alizikataa. Pamoja na hayo, imetajwa katika riwaya hii kuwa kulikuwa na wasichana wengine waliokuwa katika mahusiano ya kimapenzi wakiwa shuleni. Mahusiano ya kimapenzi ya mapema huchangia wasichana kupata mimba za mapema. Wasichana wengi kijijini walikuwa na mimba. Hii inaonyeshwa wazi wakati ambapo mamake Emira anamwambia aache kutembea na Getukwa asije akapata mimba ya mapema na umaskini wote uliokuwa kwao. Ni hali ambayo inadhihirika katika maisha ya vijana wa sasa wanaobaleghe. Katika jamii tumeona vijana wengi ambao ni wanafunzi wa shule ya upili wakijiingiza katika mapenzi na hatimaye wengi kupata mimba na kukatiza masomo yao. Kwa hivyo riwaya hii inaakisi sifa muhimu za FYV.

Utafiti huu umegundua kuwa vijana wana nafasi kubwa katika jamii wanamoishi. Licha ya kuwa kuna tamaduni zinazowakandamiza vijana wa jamii mbili za riwya teule yaani jamii ya Ugobo katika *Kimbilio la Silona* na Jamii ya Miwambo katika *Majilio ya Mkombozi* wanajikakamua na kuleta mabadiliko makubwa na ya muhimu katika jamii zao. Vijana wana uwezo wa kutekeleza mambo makubwa na ya ajabu. Kijana Silona alileta mabadiliko makubwa katika jamii yake. Alichangia mtazamo wa wanawake kubadilika katika jamii yake. Wazee wa

Ugobo waligundua kuwa mwanamke si chombo wala kinyago cha kumsifia mume. Pia kijana Silona alionyesha kuwa wasichana wana uwezo wa kusoma na kupata elimu ya juu. Vilevile kisa cha Rebeka pia kilionyesha kuwa wasichana wanafaa kurithi mali ya wazazi wao.

Utafiti huu umebainisha kuwa usawiri wa vijana katika riwaya za vijana unazingatia sifa kimsingi za FYV. Sifa ambazo riwaya hizi teule za *Kimbilio la Silona* na *Majilio ya Mkombozi* zimeakisi ni kama zifuatazo. Kwanza mhusika mkuu huwa ni kijana. Katika riwaya ya *Kimbilio la Silona* mhusika mkuu ni Silona na ni kijana wa umri wa miaka kumi na saba. Katika *Majilio ya Mkombozi* wahusika wawili wakuu ni Getukwa na Ilonkundemi ambao ni vijana wa miaka kumi na sita na kumi na saba mtawalia. Pia dhamira zinazozungumziwa huwahusu vijana wanaobaleghe. Dhamira ambazo zimeshughulikiwa katika riwaya teule ni pamoja na mapenzi, elimu, ndoa za mapema, matumizi ya teknolojia na kupinga mila zinazokinzana na matakwa ya vijana. Sifa nyingine ni kuwa FYV inawalenga wahusika vijana kati ya umri wa miaka 12 hadi 21.

### 5.3 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umelenga kuwafaidi watafiti wa fasihi ya Kiswahili kuhusu dhamira na wahusika katika FYV na jinsi ambavyo riwaya za vijana zinaakisi sifa za FYV. Watafiti wa fasihi watatumia mchango wa utafiti huu ili kukuza utafiti wao kwa msingi ulio bora. Pamoja na hilo utafiti huu utawasaidia wasomi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kwa kukuza usomi wa fasihi hasa ya vijana. Hili litawezekana kwa sababu tasnifu hii itakuwa kazi ya kurejelewa na wasomi na wahakiki wa fasihi. Vilevile, utafiti huu utaweza kuchangia katika kuelimisha jamii juu ya mchango na umuhimu wa fasihi ya vijana. utaweza kuonyesha jinsi kazi za fasihi ya vijana inavyoweza kuwa kioo cha mwenendo wa kijamii na jinsi zinavyoathiri mawazo na mitazamo ya vijana. Pia utafiti huu utaweza kutoa ufahamu wa kina katika mada na masuala yanayowahusu vijana. Unaweza kufichua jinsi kazi z a fasihi za vijana zinavyojibu masuala ya kijamii,

kitamaduni, na kisiasa, na jinsi zinavyosaidia kujenga utambulisho wa vijana. Hii ni kwa sababu utafiti huu umeonyesha sifa za kazi ambayo ni ya vijana wanaobaleghe. Imeonyesha dhamira zinahusiana na vijana wanaobaleghe na zaidi kuonyesha usawiri wa wahusika katika FYV.

## 5.4 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto kama vile ukosefu wa vitabu vya Kiswahili vya nadharia ya tanzu na FYV. Ilitulazimu kusoma vitabu vya Kiingereza na kufasiri ili kupata dhana mbalimbali na maelezo ya kina hasa ya nadharia ya Tanzu. Haikuwa kazi nyororo kutafsri huku ikitiliwa maanani kuwa kuna misamiati ya Kiingereza ambayo ni vigumu kuipata katika Kiswahili. Kwa mfano, dhana Young Adult Literature imetafsiriwa kama Fasihi ya Vijana ambayo inajumuisha vijana wa umri wa kubaleghe hadi miaka 40. Taarifa nyingi tulizopata kutoka mtandaoni zilikuwa zimeandikwa kwa lugha ya kiingereza hivyo ikatubidi kusoma na kufasiri.

Changamoto nyingine ni kuwa upatikanaji wa nakala sahihi za riwaya za fasihi ya vijana ilikuwa changamoto kubwa katika utafiti wetu wa maktabani. Riwaya za fasihi ya vijana zilikuwa adimu, na wakati mwingine, hazipatikani katika maktaba za kawaida. Hii iliweza kuathiri uwezo wetu wa utafiti kupata vyanzo sahihi.

## 5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Utafiti huu umeangazia dhamira na wahusika katika FYV kwa kurejelea riwaya teule za *Kimbilio la Silona* na *Majilio ya Mkombozi*. Mtafiti alieleza dhana ya dhamira na wahusika katika FYV kwa kurejelea riwaya teule. Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi kwa kutumia vigezo vingine vya fani na maudhui ya vijana wanaobaleghe kati ya umri wa mika 12 hadi 21.

Pia kuna haja ya kutafiti masuala mengine yanayowahusu vijana wanaobaleghe kama vile swala la mpito katika maisha ya vijana jinsi mapito hayo hujitokeza na umuhimu wake katika jamii. Mapito kama vile ya kisaikolojia, kimwili, kiafya na ya kijamii.

Kutokana na utafiti wetu tuligundua kuwa vitabu vingi vinavyosomwa na wanafunzi wa shule za upili hasa riwaya za Kiswahili si za FYV. Hivyo kuna haja ya wakuza mitaala kuhakikisha kuwa riwaya zinazosomwa shuleni ni za vijana wanaobaleghe ili vijana waweze kujifunza moja kwa moja kutokana na masuala yanayowahusu. Mfano wa riwaya hizo ni kama vile *Majilio ya Mkombozi*, *Vipanya vya Mahabara* na *Kimbilio la Silona*. Hii itawasaidia vijana hawa kwa sababu wahusika ni vijana wa umri kama wao, lugha inayotumika inaingiana sawasawa na wao, urefu wa riwaya za vijana unawafaa zaidi, maudhui yanayokuzwa yanawahusu vijana wanaobaleghe kati ya mambo mengi.

Katika utafiti wetu tuliangalia riwaya za mwandishi mmoja, kuna haja ya kutafiti kuhusu waandishi wengine wa FYV ili kuona jinsi ambavyo kazi zao zinaakisi sifa muhimu za fasihi ya vijana.

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani, mtandaoni na kusoma kazi za awali. Pana haja ya kufanya utafiti wa ana kwa ana baina ya mwandishi na mtafiti ili kupata ladha na azma ya mwandishi katika utunzi wake wa riwaya hizo.

Utafiti huu ulitumia riwaya, pana haja ya kutumia tamthilia, mashairi ili kutafiti zaidi kuhusu dhana ya dhamira na wahusika katika FYV.

# MAREJELEO

Ali, A. M. (2019). *Kuchunguza Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya Kamwe si Mbali Tena* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, The Open University of Tanzania).

Haji, M. D. I. (2018). *Uhalisia wa Utabaka katika Tamthilia ya Janga la Werevu na Kitumbua Kimeingia Mchanga (*Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, The State University of Zanzibar (SUZA). http://repository.suza.ac.tz:8080/handle/123456789/138

Jilala, H. (2016). Misingi ya Fasihi Linganishi. Nadharia Mbinu na Matumizi. Dar es Salaam: Daud Publishing Company.

Kerre, E. (2020). *Maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika riwaya za Chozi Langu na Dunia Mashaka Makuu* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Kenyatta).

Kihara, S. (2016). *Nafasi ya vijana katika riwaya za Pendo La Karaha na Kovu Moyoni* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi)

Kimani, N. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi, Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.

Kinoti, T. M. (2019). Umbuji wa Wahusika katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano Kutoka kwa Diwani ya Jicho la Ndani (SA Mohamed, 2002). *East African Scholars Journal of Education, Humanities and Literature, 2*(6), 1-6. http://repository.embuni.ac.ke/bitstream/handle/embuni/2179/Kinoti%20-%20Umbuji%20wa%20Wahusika%20katika%20Ushairi%20wa%20Kiswahili%20Mifano%20Kutoka%20kwa%20Diwani.pdf?sequence=1&isAllowed=y

Lyatuu, J. (2011). “Usawiri wa Wanawake katika Fasihi ya Kiswahili: Ulinganifu wa Waandishi wa Kike na Kiume: Uchaguzi katika Riwaya Teule,” Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Maguo, O. M., & Alhabib, E. A. (2021). Mtindo na Wahusika katika Diwani za Dhifa na Wasakatonge. *Mulika Journal, 39*.50-65 http://www.journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/4023/3637http://www.journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/4023

Manoti, J. N. (2012). *Dhamira ya Uozo na Athari Zake kwa Jamii, Katika Riwaya ya Upotevu.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi

Mlacha, S.A.K. (1996), “Utamaduni wa Mwafrika katika Riwaya ya *Bwana Myombekere* na *Bibi Bugonoka*,” katika, *Mulika* namba 23, Dar es Salaam: TUKI, Kur. 24-35.

Msokile. M. (1993). *Misingi ya Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi, EAEP,

Mutua, J., Chimerah, R., & Ngowa, N. (2017). Mitazamo ya Kusawiri Wahusika wa Kike katika Tamthilia za Kiswahili: Posa za Bikisiwa na Mama Ee. *Mara Research Journal of Kiswahili, 2* (1), 1-11. http://ir.mksu.ac.ke/handle/123456780/4300

Nalika, R. (2012), *Uhakiki wa hali ya vijana katika riwaya ya Vipanya vya Maabara* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Ndungo, C. Y. na Wafula, R. M. (1993), *Tanzu za Fasihi Simulizi*, Nairobi: University of Nairobi.

Njogu, K. & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa fasihi*: Nadharia na mbinu. Jomo Kenyatta Foundation.

Nkonge, G. (2006). *Athari za udhanaishi katika Kichwa Maji na Nguvu ya Sala* (Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi)

Ramadhani, S. K. (2013). "Usawiri wa Mwanamke Katika Taarab ya Mipasho: Mfano Kutoka Nyimbo za Mzee Yussuf Mzee". Tasinifu ya M.A. Kiswahili, Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam.

Rowlett, J. (2017). *Genre theory and historical change*: *Theoretical essays of Ralph Cohen*. University of Virginia Press

Sanga, A. N. (2021). Athari za mkengeuko wa ujumi wa kiafrika katika hadithi fupi andishi za Kiswahili. *Kioo cha Lugha*, *6*(18), 1-14. http://196.44.162.39/index.php/kcl/article/view/4003

Simala, I., & Chacha, L. (Eds.). (2014). *Miaka hamsini ya Kiswahili nchini Kenya*. Nairobi, Kenya: Twaweza Communications.

Wamitila, K. (2002). Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake. Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi, Kenya: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W., (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*, Nairobi: Vide-Muwa.

Wanjala, J. A. (2015). *Usawiri wa malezi unavyoathiri utambulisho wa vijana katika riwaya ya kiswahili* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Nairobi).

Wasike, C. K. (2020). Mtindo wa Uwasilishi wa Dhamira za Ukimwi Katika Kazi za Fasihi: Kielelezo cha Tanzu Teule za Fasihi Andishi (Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu, Chuo Kikuu cha Moi).